# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TANO

**Kikao cha Kumi – Tarehe 13 Novemba, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mnasalimiwa sana na Wabunge wa Canada ambako nilikwenda na wako tayari kushirikiana na Bunge letu la Tanzania kama tukifanya maandalizi yanayostahili ambayo mojawapo ni kuandika mpango mahsusi wa kuweza kuimarisha Bunge letu. Kwa hiyo, wako tayari kufanya kazi na sisi. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 124

**Watumishi wa Idara ya Afya Waliojilipia Gharama za Masomo**

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa watumishi wa Idara ya Afya waliochukua mafunzo mwaka 1995-1998 na Halmashauri zao hazikuwalipia gharama za masomo yao badala yake walijilipia wao wenyewe:-

Je, Serikali haioni sasa kuwa Halmashauri hizo hazikuwatendea haki wafanyakazi hao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zimekuwa zikiwasomesha watumishi wao kwa njia moja au nyingine. Njia hizo ni pamoja na:-

(i) Mtumishi wa Halmashauri kulipiwa na Serikali Kuu;

(ii) Ruzuku ya Serikali Kuu inayopelekwa kwenye Halmashauri kama matumizi mengineyo;

(iii) Kusomeshwa na Wizara za Kisekta;

(iv) Kusomeshwa kwa kutumia fedha zilizokusanywa na Halmashauri zenyewe;

(v) Kusomeshwa na Wafadhili; na

(vi) Mtumishi kujilipia mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu kuwa uwezo wa Halmashauri zetu kifedha sio wa kuridhisha na watumishi wanaohitaji kusoma ni wengi. Hivyo, baadhi ya watumishi wanapoona kuwa wamepata nafasi ya kusoma kozi wanazozitaka na Halmashauri haina uwezo kwa wakati huo wanaamua kujilipia wenyewe. Aidha, Halmashauri inachofanya ni kutoa ruhusa kwa mtumishi ili akahudhurie mafunzo hayo. Kwa hiyo, Halmashauri imewatendea haki kwa kuwaruhusu kuhudhuria masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujiendeleza ni jambo muhimu kwa mtumishi ili apate ujuzi, kuongeza ufanisi kazini, kupanda cheo kulingana na fani aliyosomea, matokeo yake na kuwa ni mshahara mkubwa au mshahara mzuri. Hivyo napenda kuzishauri Halmashauri zote nchini kuwa na programu ya mafunzo kwa watumishi wake, na kuhakikisha kuwa inatenga fedha za kutosha kila mwaka ili kuwapeleka watumishi wake masomoni awamu kwa awamu.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa waganga wengi walikuwa wakichukua mafunzo ya *up grading* katika Chuo cha Maweni Kigoma *Clinical Officers,* Halmashauri zingine zilikuwa zikiwalipia watumishi hao na wengine walikuwa hawalipiwi. Sambamba na hilo katika chuo hicho waganga waliokuwa wakisoma wakati huo walikuwa wakijilisha wenyewe hawalishwi na Chuo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipia gharama zao ambazo walizitumia wakati huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzoni kwamba kuna njia mbalimbali ya kujisomesha na kujiendeleza kwa watumishi wa Halmashauri. Sasa iwapo Halmashauri inakosa fedha na mtumishi anaona kuna ulazima wa kwenda kozi inayohusika anajilipia mwenyewe na Halmahsauri inatoa kibali. Kwa kweli kwa wale watumishi ambao wamejilipia wenyewe chakula na matumizi mengineyo kwa sasa Halmashauri haina mpango wa aina yoyote wa kuwarudishia fedha zao.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuniona. Kwa kuwa kuna wafanyakazi wengi wakiwemo walimu ambao wamejisomesha wenyewe katika vyuo mbalimbali hapa nchini, wengine wamesoma masuala ya jinsia, wengine masuala ya mipango. Lakini wanaporudi kwenye ajira wanaendelea kubaki na cheo kile kile bila nyongeza ya mshahara. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba kama wale wamesoma taaluma nyingine wawahamishie Idara nyingine zinazohusika na taaluma walizosomea na kuhakikisha kwamba wanawapandisha madaraja wanayostahili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale watumishi ambao wanajiendeleza katika fani husika kwa mfano mtumishi wa afya anajiendeleza katika fani ya afya atapandishwa cheo au atapewa nyongeza kulingana na mujibu wa sheria. Kwa wale watumishi wanabadilisha *field* kabisa, inategemeana na nafasi ya Halmashauri husika.

Kwa mfano, mtumishi wa Afya ameenda kusomea fani labda ya Mipango, ina maana kwamba amebadilisha fani *complitely* inabidi kule upande wa Afya ile nafasi aliyoiacha inabidi uweke mtumishi mwingine. Kwa hiyo, yule ambayo ameenda kwenye fani nyingine inabidi tuangalie kama uwezekano au nafasi ipo katika Halmashauri husika. Kama Halmashauri husika haina nafasi hiyo inabidi abaki pale pale mpaka hapo Halmashauri husika au Wizara husika itakapopata nafasi na itakapopata nafasi ya kumwajiri au kumweka kwenye makisio yao.*(Makofi)*

Na. 125

**Ukarabati wa Barabara ya Marangu-Kilema-Kitowo**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ni nyenzo muhimu katika kuinua uchumi wa nchi yoyote na kwa kuwa kuna maeneo mengi ambayo hayana barabara zinazopitika kwa majira yote ya mwaka:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuikarabati barabara ya kutoka Marangu Mtoni – Kilema hadi Kitowo, ili iweze kupitika kwa nyakati zote?

**NAIBU SPIKA:** Yaani ulikuwa unaongeza swali. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumhakikishia Mhesimiwa Mbunge, kwamba Serikali inafanya kazi kulingana na uwezo wa upatikanaji wa fedha na si vinginevyo. Ni azma ya Serikali kwamba kuwe na maisha bora kwa kila Mtanzania na si vinginevyo. Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imekuwa ikiifanyia matengenezo ya kawaida sehemu ya barabara ya Marangu – Kilema ambayo ina urefu wa (km 4.5) ambayo iko chini ya Halmashauri ya Wilaya na iko kwenye hali nzuri ya wastani *(fair condition)* na inapitika wakati wote wa mwaka. Matengenezo ya kawaida yaliyokwishafanywa katika sehemu hizo kuanzia 2003 – 2005 ni kama ifuatavyo:-

- Mwaka 2003 zilitumika Sh.6.3 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo;
- Mwaka 2004 zilitumika Sh. 6.2 ; na
- Mwaka 2005 zilitumika Sh.3.3 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya barabara ya Kilema – Kitowo ni barabara ya Jumuiya *(Community Road),* ambayo inahudumiwa na wananchi kwa kuwa Serikali haina uwezo wa kutengeneza barabara zote pamoja na barabara za Jumuiya. Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Moshi inawahamasisha wananchi kutumia nguvukazi ili kuboresha barabara zao za Jumuiya.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri amesema kwamba Serikali hujenga kuendana na uwezo wake na kwa kuwa Serikali hii ilinunua lami kuanzia mwaka 93 na mpaka leo hii lami ile haijatumika na imebaki ikiibiwa na vibaka. Je, Serikali inatueleza nini kuhusu hilo na kwa nini lami ilinunuliwa mpaka leo haijatengeneza barabara kwa zaidi ya miaka 12?

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala aliloliulizia Mheshimiwa Susan Lyimo tulishalipata tena hapa Bungeni tukalitolea maelezo ya kina kabisa kueleza ni kwa nini jambo hili bado halijawezekana. Ninaloweza mimi kumsihi kwa leo kwa sababu ameanzisha jambo hili kwa mara nyingine hebu kaeni kwenye Halmashauri yenu wenyewe. Jaribuni kuchukua historia ya mgogoro wa lami hiyo. Jaribuni kujiridhisha kama lami hiyo baada ya miaka yote hii bado inaweza ikafanya kazi tena kama lami inayoweza kuwekwa kwenye barabara, kisha tuwasilishieni hiyo taarifa yenu halafu kwa pamoja tutashirikiana tuone kama tuna namna ya kusaidiana. *(Makofi)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais moja ya ahadi alizotoa ni kujenga barabara ya Marangu-Kilema hadi Kirua. Je, ina maana Serikali haina mpango wa kutimiza ahadi hiyo ya Rais? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kweli Rais akishatoa ahadi ni lazima itatekelezwa

ingawa inawezekana isiwe mwaka huu. Kwa hiyo, jambo hili ni kweli tutalifanyia kazi tutalitengenezea utaratibu ambao utawezesha ahadi ya Rais kuweza kutimizwa. Lakini ni budi niseme kwamba lazima Halmashauri na yenyewe isikaye tu kwa sababu Rais alitamka basi mkadhani jambo hili ni la upande mmoja. Lazima na Halmashauri na yenyewe mjishughulishe tuone programu ikoje kwa maana ya kuwasilisha jambo hili rasmi sasa ili tuweze kuanza kufanya kazi hiyo ambayo Rais aliahidi.

Na. 126

**Ukarabati wa Barabara Jimbo la Kigamboni**

**MHE. MUSA Z. AZZAN (k.n.y. MHE. MWINCHOUMO A. MSOMI)** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara nyingi katika Jimbo la Kigamboni ni mbovu hali inayohatarisha maendeleo ya wakazi wa jimbo hilo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga na kupanua barabara kutoka Feri-Pemba Mnazi kwa kiwango cha lami?

(b) Kama ujenzi na upanuzi huo utafanyika na kupita katika nyumba na mazao ya wananchi. Je, watalipwa fidia husika?

(c) Je, Serikali ina mipango gani juu ya ujenzi wa barabara kutoka Feri Kisarawe II – Tundwi Songani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoumo Abdulrahaman Msomi, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia wakala wa barabara *(TANROADS)* inahudumia jumla ya kilomita 139.4 za barabara zilizoko katika Jimbo la Kigamboni. Barabara hizo ni Kivukoni-Mjimwema-Pembamnazi (km 56.4), Dege-Mbutu-Gomvu (km 11.2), Buyuni-Tundwisongani (km 15.5), Kibada-Kisarawe II, Chekenimwansonga-Tundwisongani (km 31.6), Kivukoni-Tungi-Vijibweni (km 6.7) na barabara ya mwisho ni Kongowe – Mjimwema (km 18.0).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 kiasi cha shilingi 64.9 kilitengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Kivukoni – Mjimwema – Pembamnazi (km 56.4). Matengenezo haya yalihusu kuchonga kwa greda, kusafisha mifereji na *culverts,* kufyeka majani, kuweka kifusi katika sehemu korofi pamoja na matengenezo ya dharura ya daraja la Kimbiji lililoathiriwa na mvua za mwaka jana. Kazi za barabara hiyo ziligharimu jumla ya Sh.39.1 na kazi ya dharura ya ujenzi wa daraja imegharimu shilingi milioni 25 kazi zote hizi zimekamilika. Aidha katika mwaka

2005/2006, kiasi cha Shilingi 33.4 zilitengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Kibada – Kisarawe II – Tundwisongani (km. 31.6) na shilingi milioni 110 zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa daraja la pili katika mto Sangatini unaokatisha kwenye barabara hii. Kazi zote hizi zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kivukoni – Mjimwema – Pembamnazi ina kilomita 9.4 ambazo ni za lami na katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 *TANROADS* ina mpango wa kuongeza kilomita nyingine mbili za lami kwa gharama ya Shilingi 400 na vile vile wataendelea kuzifanyia matengenezo ya kawaida kilomita 45 za sehemu iliyobakia ambayo haina lami. Mpango wa Serikali ni kuiwekea barabara hii lami kila mwaka kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana hadi kuikamilisha.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria za barabara *(Highway Ordinance)* ya mwaka 1967 kipengele namba 52, jumla ya kilomita 17.4 toka Kivukoni mpaka Gezaulole (Mboa maji) katika barabara ya Kivukoni – Pembamnazi zilikwisha milikishwa na Serikali kisheria kwa upana wa mita 45, yaani kilomita 22.5 kila upande toka katikati ya barabara. Kwa Sheria hii, wale wote watakaokuwa wamejenga au kupanda mazao ndani ya eneo hili hawatalipwa fidia wakati eneo hilo litakapohitajika kwa matumizi ya barabara mpaka sasa Wakala wa barabara *TANROADS)* wameshawapa *notice* wote waliovamia hifadhi ya barabara kuanzia Kivukoni mpaka Gezaulole.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara itaendelea kuifanyia matengenezo ya kawaida pamoja na kuiwekea changarawe kwenye sehemu korofi barabara ya Feri-Kibada hadi Tundwisongani.

**MHE. MUSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ni pamoja na vivuko. Naipongeza Serikali kwa kuweka Bajeti kwa mwaka huu kununua kivuko kipya cha Kigamboni. Lakini kivuko hiki kitapatikana baada ya miezi 12. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kivuko cha sasa hivi kinafanya kazi kwa usalama ili wananchi au wakazi wa eneo lile wasipate madhara kama wanayoyapata sasa hivi wa kivuko kuzimika katikati ya maji?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya juhudi za kuhakikisha kwamba feri zile mbili Kigamboni na Alina zinaendelea kufanya kazi wakati ambapo juhudi za kuagiza feri nyingine zinafanyika na kama alivyosema ni kweli kwamba feri hiyo mpya kwa sababu inajengwa upya na mkataba tumeshasainiana na pamoja na huyo anayeleta feri itakuja baada ya mwaka mmoja. Lakini wakati tukisubiri feri hiyo juhudi zinafanyika kutengeneza feri hizi ambazo zipo na kwa ujulisho tu ni kwamba *World Bank* tayari wiki iliyopita wametoa *no objection* ya kukarabati kwa kiwango kikubwa feri ya *MV Kigamboni.* Lakini hata hivyo injini kwa ajili ya feri hizi mbili ambazo zilikuwa ziagizwe tayari zilishaagizwa na kufikia Mei mwaka kesho zitakuwa zimefika na hii itaweza kuboresha hali ya zile feri mbili pale. *(Makofi)*

Na. 127

**Malengo ya Milenia**

**MHE. ANNE KILANGO MALECELA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wakuu wa nchi 189 zilizo wajumbe wa Umoja wa Mataifa, Tanzania ikiwa ni mojawapo walifanya kikao maalum kwenye Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, Jijini New York kati ya tarehe 6 na 8 Septemba, 2000 na kupitisha kwa kauli moja Maazimio 8 muhimu yanayojulikana kama *UN Millennium Development Goals* na kwa kuwa kati ya maazimio hayo yote muhimu, azimio zito kuliko yote ni lile la kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2015 nchi zote (189) zihakikishe umaskini na tatizo la njaa linaondolewa kwa asilimia 50. Je, Serikali ya Tanzania imeandaa mikakati gani endelevu kuhakikisha kwamba, inatimiza maazimio yote 8 yaliyoazimiwa ifikapo mwaka 2015.

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Katika kuhakikisha kuwa Tanzania inatimiza maamizio yote 8 ya Maendeleo ya Milenia *(Millenium Development Goals)* ifikapo mwaka 2015, Serikali imejidhatiti kwa kuandaa Mkakati wa Kukuza uchumi na Kuondoa umaskini Tanzania (MKUKUTA) ambao umejielekeza katika kutekeleza malengo hayo.Kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kutoa maelezo kuhusu mikakati ya utekelezaji wa MKUKUTA katika lengo la kwanza la *MDG* ambalo ni kutokomeza umaskini uliokithiri na njaa kwa asilimia 50 ifikapo 2015. Serikali imeanza kutekeleza programu ya maendeleo ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Program (ASDP)* ambayo pamoja na mambo mengine inalenga katika kuboresha kilimo kwa kuimarisha upatikanaji wa pembejeo kwa urahisi, upatikanaji na utumiaji wa zana bora za kilimo, kufufua na kuendeleza mafunzo ya watalaam wa huduma za ugani, kuandaa mkakati wa kuboresha huduma za maji mijini na vijijini pamoja na kuboresha huduma za umwagiliaji. Sanjali na hayo.

Serikali imeaanda mpango wa kuimarisha na kuboresha ushirika, kuendeleza fursa za kuboresha mtandao wa masoko, kuimarisha mfumo wa teknolojia sahihi za uhifadhi wa chakula katika ngazi ya Kaya, kuongeza kiwango uwezo wa uhifadhi wa chakula katika ngazi ya Taifa, kutoa kipaumbele katika upatikanaji wa ajira na kuboresha fursa na mazingira ya kufanya biashara na kurasilimisha biashara na mitaji katika maeneo yasiyo rasmi, ili kutoa fursa za upatikanaji wa mitaji na ajira pamoja na Mpango mzima wa Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Aidha, mradi wa kijiji cha mfano cha millennia umeanzishwa katika kijiji cha mbola Wilaya ya Uyui, Mkoani Tabora ina lengo la kufanya majaribio kuhusu utekelezaji wa malengo ya millennia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na mikakati niliyoieleza Serikali pamoja na mafanikio yote yaliyokwishapatikana katika lengo hili zito kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, mafanikio mengine yameanza kuonekana katika malengo mengine ambayo ni pamoja na lengo la pili la

la Elimu ya msingi kwa wote:-

- Kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi katika shule za msingi kimepanda kutoka asilimia 77.6 mwaka 2000 hadi kufikia asilimia 109.9 mwaka 2005 ambayo ni zaidi ya kiwango kilichowekwa cha malengo ya millennia. Aidha, miundombinu mbalimbali inazidi kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kuongeza madarasa na nyumba za walimu katika shule zote za msingi nchini. Waheshimiwa Wabunge ninyi ni mashahidi wa ruzuku ambayo imetumwa hivi karibuni.

- Usawa wa Kijinsia na Fursa sawa kwa wanawake: Fursa sawa kwa wanawake zimeendelea kuongezeka ikiwa ni pamoja na asilimia 30 kwa wanawake katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

- Kupunguza Vifo vya watoto wachanga, idadi ya vifo vya watoto wachanga chini ya miaka mitano imepungua kutoka vifo 147 mwaka 1999 hadi kufikia vifo 112 mwaka 2004 kwa kila vizazi hai 1000. Aidha, vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka vifo 199 mwaka 1999 hadi vifo 68 mwaka 2004 kwa kila vizazi hai 1000. Hii imetokana na kuimarika kwa huduma za matibabu na chanjo kwa magonjwa yanayozuilika.

- Upatikanaji wa huduma bora za uzazi: Lengo la tano, kwa kuzingatia ukubwa wa vifo vya akina mama wanaojifungua, Serikali inatekeleza mkakati wa huduma ya afya ya uzazi ya mama na mtoto 2006/2010 ni matumaini yetu kuwa hadi kufikia mwaka hapo 2010 tatizo hili litakuwa limepungua kwa kiasi kikubwa kama siyo kumalizika kabisa.

- Mkakati wa kupambana na UKIMWI, Malaria na magonjwa mengine. Kasi ya kupambana na maambukizi ya Ukimwi, kifua kikuu na programu mbalimbali na upatikanaji wa huduma za afya majumbani imeongezeka. Huduma za kupambana na malaria zinaendelea kuimarika kwa kuondolewa kodi za malighafi za utengenezaji wa vyandarua, kuendeleza kuviboresha vituo vya utafiti wa malaria, kuhamasisha mpango wa kuondoa mazalia ya mbu, pamoja na mpango mzima wa hati punguzo, ambao unaratibiwa ili kuweza kuondokana na tatizo la malaria na lengo la mwisho la saba ni

- Kulinda Mazingira yetu. ambayo Mkakati wa kimataifa umeandaliwa wa kuhakikisha kwamba unazingatia masuala mazima ya kulinda mazingira kwa kulinda vyanzo vya maji, kuvuia shughuli za kilimo na ufugaji katika maeneo ambayo yanaweza yakaleta madhara kwa mazingira pamoja na kubaini vyanzo mbalimbali vya nishati mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizi kama nchi tunakwazwa katika utekelezaji wetu ni kutokana na ukweli kwamba nchi tajiri katika kipindi kirefu zimeshindwa kutimiza ahadi yao walizojiwekea ya kutoa asilimia 0.7 ambayo sasa asilimia 0.5 ya mapato la Taifa ili kusaidia nchi maskini.

Kwa hivyo, jitihada hizi Tanzania kama nchi tunashindwa kufikia jitihada zetu. Aidha, mafanikio makubwa yanaweza tu yakapatikana iwapo utekelezaji wa MKUKUTA utaimarika katika ngazi za Serikali za Mitaa kwa kuwahusisha wananchi kwa ujumla katika kuibua fursa na vikwazo, na kupanga mikakati ya utekelezaji. *(Makofi)*

**MHE. ANNE KILANGO MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri Dr. Batilda Buriani, lakini mimi naomba maswali yangu mawili ya nyongeza nijikite kwenye Azimio la kwanza la Umoja wa Mataifa ambalo ni lile la kupunguza njaa na umaskini katika nchi kwa kiwango cha asilimia 50 ifikapo 2015. Naomba kuuliza maswali kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa katika nchi duniani ambazo zimebarikiwa kuwa na rasilimali za kutosha Tanzania ni nchi mojawapo katika nchi hizo duniani na hivyo hatustahili hata kuitwa maskini. Nchi yetu ina mikoa kama Rukwa, Ruvuma, Mbeya, Iringa, Manyara, Kigoma, Kilimanjaro, Arusha na Wilaya za Kongwa na Mpwapwa, ambayo Mikoa hii na Wilaya hizi zenyewe tu hali ya hewa zina mvua ya uhakika, zina vyanzo vya maji vya kutosha ambavyo vinawezesha Mikoa hii kuzalisha mahindi ya kutosha kulisha nchi nzima na hata kuuza nje. *(Makofi)*

Je, sasa Serikali kwa nini haioni umuhimu wa yenyewe kama Serikali, kwenda kujikita katika sehemu hizi na kuhakikisha kwamba inalima mapori yote ambayo wananchi wameshindwa kuyalima, ili tuweze kupata chakula na kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisikia nchi yoyote duniani, imeendelea kiuchumi, ni kwamba ni lazima iliendelee kiteknolojia kwanza. Tukiangalia kinachodhoofisha uchumi wa nchi yetu ni kwa sababu kwanza sisi hatujajiendeleza katika teknolojia, nikiwa na maana, hatujajiendeleza kwenye vifaa vya kilimo. Mashine za kwenye viwanda na kadhalika. Je Serikali haioni umuhimu wa kwanza kujikita na kufunga mkanda na kuendeleza kwanza teknolojia kama vile mamshine za kutusaidia kwenye kilimo. Za kutusaidia kwenye viwanda kuliko ambavyo sasa tunajikita zaidi kwenye uwekezaji, ambapo ifikapo mwaka 2015 siyo wao watakaotusaidia kuondoa njaa na umaskini by 50%? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kwamba tunao wajibu kabisa kama nchi, kuhakikisha ya kwamba tunajitosheleza kwa chakula, na vile vile ni kweli kwamba tunayo ardhi ambayo inaweza ikazalishachakula cha kutosha. Lakini lazima tukiri ya kwamba unaweza kuwa na rasilimali, lakini kablda hujawekeza na kuweza kuzitumia hizo rasilimali, unaweza kuendelea kuwa na rasilimali na bado ukaendelea kuwa na matatizo. Ndiyo maana mpango wa *Agricultural Sector Development Programme,* umekusudia kuwekeza rasilimali katika kilimo kwa kiwango kikubwa, tumesema katika Bunge hili kwamba, katika muda wa miaka saba ijayo.

Serikali imekusudia kuwekeza 2.5 *trilionn* shilingi za Tanzania katika kilimo kama njia moja ya kufikia malengo ya kujitosheleza kwa chakula, ikiwa ni pamoja na

kukuza uchumi na kupambana na umaskini. Mikakati ambayo tumeiweka katika kufikia lengo hilo. Moja ni kwamba kuanzia msimu huu na kuendelea, kwanza tutaimarisha zaidi huduma za ugani, ili kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanaongeza uzalishaji katika kila ekari. *(Makofi)*

Nimewahi kujibu swali katika Bunge hili kwa kusema, kilimo chetu msingi wake mkubwa ni wakulima wadogo. Ukiboresha wakulima wadogo, ukaongeza uzalishaji. Tunaweza hata kwa kufanya hivyo tukajitosheleza kwa chakula. Lakini bado tunatia mkazo na kuwakaribisha wakubwa kwa ajili ya mashamba makubwa, ili kuhakikisha ya kwamba mashamba makubwa yanasaidina na wakulima wadogo kufikia lengo lililokusudiwa.

Hatua nyingine ambayo tunaishughulikia ni umwagiliaji. Tunayo rasilimali, tunayo maji. Lakini tunahijtaji kuwekeza katika umwagiliaji. Katika mpango wetu wa *SDP,* asimilia 80 ya fedha hizo zinakusudiwa kuwekezwa katika Wilaya kwa ajili ya Miradi midogo midogo ambayo inasaidia wakulima kuwa na uhakika wa kupata chakula katika mashamba yao. Kwa sababu hali ya hewa vile vile imekuwa tatizo kubwa ambalo mwaka ambao mvua nzuri tunajitosheleza. Mwaka ambao hali ni mbaya tunakuwa na matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuondokane na hiyo *risk* tunahitajika tuwekeze zaidi katika umwagiliaji. Vile vile tunachukua hatua ya kuhakikisha ya kwamba tunatumia zana za kisasa kulingana na uwezo uliopo. Zana hizo ni pamoja na majembe yanayokokotwa na ng'ombe na siyo kwa ajili ya *ploughing* tu, lakini kwa ajili ya *planting,* kwa ajili ya kupalilia na kadhalika.

Viko vituo vinavyotoa mafunzo ya namna hiyo nchi nzima, kwa ajili ya kutaka kuboresha kilimo panapowezekana tunaingiza *tractor* na kuanzisha vituo mahususi, vya kilimo ili wakulima wadogo waweze kusaidiwa na vituo hivyo katika kupanua mashamba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali mkakati huo vile vile tunatoa ruzuku kwa mbolea na tutaendelea kutoa ruzuku kwa madawa ili kuhakikisha kwamba kilimo chetu, kinakuwa cha tija, na kinaongeza ubora, ili kupunguza gharama za mkulima na kuongeza mapato yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushuku sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali limekuwa refu. Jibu limekuwa refu. Mmemaliza muda wote kwa hiyo ninakwenda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Na. 128

**Ugonjwa wa Kifafa cha Mimba**

**MHE. KHADIJA S. NGOZI** aliuliza:-

Kwa kuwa vifo vingi vya akina mama wazazi husababishwa na ugonjwa wa kifafa cha mimba na maradhi mengine wakati wa kujifungua; na kwa kuwa tatizo hilo ni kubwa sana nchini ikilinganishwa na nchi zilizoendelea, kwa mfano hapa nchini zaidi ya wanawake wazazi 800 hufa kwa mwaka kwa tatizo hilo.

(a) Je, ugonjwa wa kifafa cha mimba husababishwa na nini?

(b) Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kutafuta chanzo cha ugonjwa huo wa kifafa cha mimba ili tiba au chanjo itolewe kwa akina mama hao kabla ya kujifungua?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la Mhesihmiwa Khadija Salehe Ngozi, Mbunge wa Kuteuliwa, naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifafa cha mimba ni ugonjwa unaowapata wanawake wajawazito, hasa wenye mimba za kwanza. Kwa walio wengi, ugonjwa huu hutokana na kupanda kwa msukumo wa damu *(High blood pressure).* Ugonjwa huu utokeapo, mgonjwa hupatwa na degedege *(convulsions)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Sababu kamili za ugonjwa huu hazijukani. Hata hivyo kuna sababu mbalimbali ambazo zinaweza kusababisha uwezekano wa kupata ugonjwa huu zikiwemo:-

(i) Mimba ya kwanza, hususan katika umri mdogo chini ya miaka 20 na umri mkubwa zaidi ya miaka 35.

(ii) Wenye mimba ya mapacha hupata zaidi kuliko mimba ya mtoto mmoja.

(iii) Ugonjwa wa shinikizo la damu au kisukari kabla ya kubeba mimba.

(iv) Kuwa na ugonjwa wa figo kwa mama mjamzito.

(b) Hakuna chanjo wala tiba ya kuzuia ugonjwa huu, bali nguvu huelekezwa katika kuchukua hatua za kuepuka tatizo hili kwa kuwashauri wanawake wasibebe mimba katika umri mdogo au mkubwa sana. Aidha mama wajawazito wanatakiwa kuwahi kliniki ambako watafuatiliwa maendeleo

yao ili kubaini dalili za mwanzo za kifafa cha mimba na kushauriwa kwenda hospitali kwa uangalizi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifafa cha mimba kikisha tokea nguvu huelekezwa katika kupunguza madhara yatokanayo na kifafa hicho. Kwa mfano kuzuia degedege isirudie rudie kwa kutoa dawa za kuzuia degedege. Kutoa dawa za kuteremsha msukumo wa damu, iwapo uko juu, na vile vile kumsaidia mama ajifungue mapema mara itakapoonekana mtoto amefikia umri wa kuzaliwa. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA M. BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ushauri mzuri wa Madaktari, husaidia kuondoa vifo na matatizo tofauti kwa akina mama pale wanapojifungua. Kwa kuwa pia wakina mama wengi wajawazito wengi hudharau kwenda *Clinic* pale wanapokuwa wajawazito hasa katika hatua za mwanzo, kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri.

Je, Serikali, ina mkakati gani wa kueneza elimu ya uzazi, hasa kule vijijini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA WAFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba vifo vingi hutokana wakati akinamama hawakufanyiwa uchunguzi, au hawakufuata masharti yale ambayo wameambiwa na Madaktari. Lakini Serikali kwa kupitia Wizara ya Afya, huwa tuna mkakati ambao akina mama wote wanatakiwa waende ku-*report,* katika vituo vya kutolea huduma ili waweze kupimwa mara tu wanapojitambua kwamba ni wajawazito.

Aidha kupitia Serikali, Wizara ya Afya, ni kwamba huwa tunatoa mafunzo kabla hatujaanza kutoa matibabu kuna utaratibu katika vituo vyote vya afya, kuanza kutoa elimu ya afya kwa akinamama na kwa jamii, na kwa wagonjwa wote wanapofika hospitalini, ili kuweza kuwaambia yale yanayojiri katika matatizo mazima ya afya zao.

Kwa hiyo, wito wangu ninautoa kwamba katika vituo vyote vya kutolea huduma. Ili kuweza kuwakumbusha siyo akinamama wajawazito tu, lakini hata wale akina baba na jamii kwa ujumla. Tunaomba waendelee kutoa elimu na tunaomba pia wananchi wawe wanasikiliza maelezo wanayopewa na wataalam wa afya, ili kuzuia siyo matatizo ya wakinamama tu, lakini hata yale ambayo yanaweza yakaikumba jamii kwa jumla. *(Makofi)*

Na. 129

**Serikali Kuwatambua Wakunga wa Jadi**

**MHE. NURU A. BAFADHILI** aliuliza:-

Kwa kuwa wapo Wakunga wa Jadi ambao wanawasaidia akinamama wanaojifungualia majumbani kabla ya kufika hospitali; na kwa kuwa baadhi ya wakunga hao wanawazalisha akinamama wajawazito katika mazingira yasiyo safi na salama:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatambua wakunga hao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyakagua maeneo wanayotumia wakunga hao katika kuwazalisha wajawazito ili kuhakikisha kuwa yanawekwa safi na salama kwa kazi hiyo?

(c) Je, Serikali ina mpango wa kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa Wakunga hao wa Jadi ili uzalishaji wao uende na wakati?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Wakunga wa Jadi hutambuliwa kwanza na jamii waliyomo na Serikali ya Kijiji, ambapo kazi zao husimamiswa na Mkunga aliyeopo Zahanati au Kituo cha Afya kilichoko karibu. Katika ngazi ya wilaya na mkoa, hufanya kazi kwa kushirikiana na Waratibu wa Afya ya Mama na Mtoto, ngazi ya Wilaya au Mkoa.

Kwa ujumla kazi za Wakunga wa Jadi zinaratibiwa na kusimamiwa na Wizara yangu chini ya kittengo cha Afya ya Mama na Mtoto *(Reproductive and Child Health Unit)* na Kitengo cha Tiba Asili na Tiba Mbadala *(Tradition and Alternative Medicine Unit).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi wa maelezo nilyoyatoa hapo juu naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inawatambua Wakunga wa jadi inauthamini mchango wao katika utoaji huduma za uzazi.

(b) Wakunga wa ajadi hawana maeneo maalumu wanayoyatumia kuzalisha wajawazito. Mara nyingi huduma ya kuzalisha huifanyia majumbani kwa wajawazito wanaohitaji huduma ya mkunga wa jadi. Hivyo ni vigumu kufanya ukaguzi kwa kuwa maeneo yanayotumika sio rasmi.

Aidha ili kuhakikisha kuwa wakunga wa jadi wanafanya kazi kwa ufanisi zaidi Serikali huwapatia mafunzo maalum ya uzazi salama na vifaa tiba vya uzazi *(Delivery Kits).*

(c) Serikali itaendelea kutoa mafunzo na kuratibu shughuli za wakunga wa jadi nchini ili kuboresha uzazi salama *(safe motherhood)* hadi hapo azma ya kuwa zahanati zenye vifaa na watumishi wa kutosha katika kila kijiji itakapotimia.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wajawazito wengi, kina mama wajawazito wengi wanaishi vijijini, na vijijini kuna

matatizo ya miundombinu, kiasi cha kuwafanya kwamba hawahudhurii *clinic* wanajifungulia majumbani.

Je, Serikali ina mpango gani, wa kuwapelekea angalao *Mobile Clinics* ili wapate ushauri na wakati wanapotaka kujifungua waweze kuhudhuria *Clinic* ili waweze kusaidiwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna upungufu wa Vituo vya Afya, na ni kweli kwamba akina mama wengi huwa hawaendi kupata huduma ya kwanza wanapokuwa wajawazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu nitoe rai. Ni kwamba ninawaomba akinamama, sasa hivi tuna uhaba wa vituo vya kutolea huduma. Serikali sasa hivi inafanya mpango ili ikiwezekana tuweze kuwa na vituo vya kutolea huduma katika kila kijiji.

Wakati Serikali inajipanga vizuri, tunawaomba wananchi wote huko waliko, watumie hizi huduma ambazo zipo katika maeneo yao sasa hivi, ili waweze kwenda kupimwa na kushauriwa vizuri, kwa sababu sasa hivi ni kwamba akinamama wengi au kwa kutumia labda mazoea, huwa wanaamini kwamba hawezi kwenda hospitali mpaka aone mtoto anacheza tumboni.

Mimi ninaomba kutoa raia kwamba mara unapojiona kwamba wewe umepata ujauzito, nenda hosptali, kwa sababu hata kama una tatizo la miundombinu. Katika kipindi cha miezi tisa, haijambo unaweza kufika kituo kile cha karibu pale unapoishi.

Kwa hiyo, mimi ninawaomba akina mama wote nchini, twende katika vituo vya kutolea huduma vilivyo karibu yetu, wataalamu tunao ili tuweze basi kushauriwa ni wapi tutaweza kujifungulia na hatimaye tupunguze vifo vingi vinavyotokea. *(Makofi)*

Na. 130

**Ujenzi wa Mabwawa ya Gumba na Titu**

**MHE. ADAM K.A. MALIMA (K.n.y. MHE. ATHUMANI S. JANGUO)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipojibu swali langu Na. 45 tarehe 5 Novemba, 2002, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo wa wakati ule aliahidi kwa niaba ya Serikali kushughuliikia ujenzi wa Mabwawa ya Gumba na Titu katika Wilaya ya Kisarawe, ambayo usanifu wake ulishakamilika katika miaka ya sabini:-

(a) Kwa kuwa sasa ni miaka minne (4) imepita na wananchi wa Kisarawe wanasubiri bila ya matumaini yoyote na wanaendelea kuteseka kutokana na uhaba wa

maji safi na salama. Je, Serikali inaweza kuwaeleza wananchi wa maeneo hayo kwamba ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake.

(b) Kwa kuwa Mradi wa Bwawa la Gumba ulitarajiwa kueneza maji katika vijiji vya Gumba, Masaki, Sungwi, Kisanga, Kazimzumbwi, Mji Mdogo wa Kisarawe, Shule ya Minaki na ziada kupelekwa Jijijini Dar es Salaam; na kwa kuwa wananchi wa Kisarawe na wanafunzi wa shule ya Minaki wanateseka kwa ukosefu wa maji safi na salama. Je, Serikali inaweza kuwaeleza wananchi hao kuwa ina mpango gani mbadala wa kulitatua tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mbunge wa Kisarawe lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kujenga mabwawa ya Gumba na Titu katika wilaya ya Kisarawe ulianza mwaka 1970 wakati ambapo Serikali kwakushirikiana na Shirika la Maendeleo la Canada *(CIDA)* iliandaa *Water Master Plan* katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Kazi kubwa iliyofanywa na kukamilika wakati huo ilikuwa ni uchunguzi na usanifi wa awali. Kwa kuwa usanifu ulifanyika miaka ya sabini, ni dhahiri kuwa kumetokea mabadiliko mengi katika maeneo husika kimazingira na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 Serikali ina mpango wa kufanya mapitio ya usanifu wa Bwawa la Titu na kuanza ujenzi katika kipindi cha mwaka 2007/2008 na baadaye itaendelea kushughulikia Bwawa la Gumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kufanya usanifu wa miradi ya maji katika vijiji vya Chakenge, Mfazi, Masaki, Kiluvya "A", Kibuta, Kihare, Vikumburu, Kwala, Msanga na Boga katika mwaka huu wa 2006/2007 na kuanza ujenzi katika kipindi cha mwaka 2007/2008. Aidha, chini ya msaada wa Serikali ya Japan vijiji vya Chole na Msimbu vitajengewa miradi ya maji ambapo usanifu wa awali umeshakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendela kusambaza huduma ya maji katika Wilaya ya Kisarawe kupitia Programu ya Kitaifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inakiri kwamba ilianza usanifu wa jinsi ya kuchimba mabwawa hayo toka mwaka 1970 na wakati kabla ya hapo, katika Wilaya ya Mafia ujenzi wa Mabwawa kama hayo yalijengwa katika kijiji cha Jibondo na Juani Mafia. Mfano kijijii cha Jibondo kunako mwaka 1965 wananchi wa kijiji hicho walikuwa wapatao 1,000, sasa hivi kuna wakazi zaidi ya 4,000. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ukubwa wa Mabwawa hayo ili yaweze kukithi haja ya wananchi ambao wako sasa hivi katika kijiji cha Jibondo, zaidi ya wakazi 4,000 na kijiji cha Juani, kulitengeneza upya bwawa hilo ambalo lilikwisha haribika karibu miaka 10 iliyopita, ili nalo liweze kukithi mahitaji ya wananchi wa kijijiji cha Juani katika Wilaya ya Mafia? *(Makfoi)*

**NAIBU SPIKA:** Pamoja na kwamba ni swali jipya, Naibu Waziri unaweza kujibu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa Serikali ina mpango ufuatao kwa ajili ya Jimbo la Mafia. Katika mwaka huu wa fedha Jimbo la Mafia litapewa Miradi ifuatayo: Mbweni, Kanga, Kungwi, Chole, Jimbo, Kiageni, Banja, Juani, Kirongwe na Mirongo. Pia katika mwaka huu wa fedha ambapo utaendelea mpaka katika ya mwaka ujao 2007, Serikali itakarabati miradi ifuatayo Jimbo la Mafia. *(Makofi)*

Miradi hiyo ikiwemo, Marimbani, Kitongoji, Kitomondo, ambapo patajengwa kisima kirefu. Pia Kirongwe kutagenjgwa kisima. Kiegeni pia kutakarabatiwa kisima, Kanga *shallow well,* kutakarabatiwa pia, Kinondoni, Chunguruma, Miburani na Juani kwenye Shule na Zahanati ambapo utawekwa mradi wa kuvuna maji ya mvua. Hiyo ndiyo mipango ya Serikali kwa kipindi hiki cha mwaka wa fedha, ambacho Mheshimiwa alichokiongelea kuhusu hilo Bwawa, tunamwomba ashirikiane na Halmashauri yake ya Wilaya ya Mafia ili kutafakari hilo jambo na kulileta kwetu kwa ajili ya miaka ijayo ya fedha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani mtakubali kwamba Naibu Waziri amebobea, wala siyo swali la msingi, lakini amelijibu vizuri. *(Makofi)*

Na. 131

**Uhaba wa Maji – Nanyumbu**

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya mpya ya Nanyumbu imeathirika sana na ukame na hivyo kusababisha uhaba mkubwa wa maji hasa katika Kata za Maratani, Nanyumbu, Likokona, Chipuputa na Sengerenya; na kwa kuwa kutokana na hali hiyo wananchi wa maeneo hayo hutumia maji yasiyo salama hali inayosababisha magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu na kuhara damu hatimaye vifo kutokea:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuchimba visima virefu kwenye maeneo hayo ili kuwasaidia wananchi kupata maji?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaharakishia wananchi wa wilaya hiyo waweze kupata huduma ya maji safi ili waondokane na adha ya kutafuta maji kwa mwendo mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dustan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Wilaya mpya ya Nanyumbu imeathirika na ukame uliosababisha uahaba mkubwa wa maji kwenye Kata za Maratani, Nanyumbu, Likokona, Chipuputa na Sengenya.Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwasaidia wanachi kupata maji, Serikali imepanga kuchimba visima virefu vinane kwenye maeneo ya Michiga, Likokona, Napacho, Nangomba, Chitowe, Chipuputa, Sengenya na Mkonona katika mwaka huu wa 2006/2007. Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan imechimba visima virefu vitano kwenye vijiji vya Nanyumbu (ambako vilichimbwa vitatu); Kilosa (kimoja) na Namasogo kumechimbwa kisima (kimoja). Taratibu za kufunga pampu zinaendelea sasa. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji nchini na hasa vijijini, Wizara yangu imeandaa Programu ya Kitaifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, ambayo itaanza kutekelezwa katika wilaya zote nchini kuanzia mwaka wa 2006/2007. Programu hiyo itatekelezwa na Halmashauri za Wilaya zikisaidiwa na Wizara yangu. Vijiji vitakavyohusika kufanyiwa usanifu wa miradi katika mwaka huu 2006/2007 kwenye Wilaya ya Nanyumbu ni Chipuputa, Sengenya. Mangaka, (Makao makuu wilaya), Ndechela, Nandembo, Kamundi na Ulanga. Aidha, chini ya Programu hii Serikali inatarajia kukarabati miradi ya maji katika vijiji vya Wandebo, Mikangaula, Lukula, Nandete na Mangaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nia ya Serikali kuharakisha upatikanaji wa huduma ya maji chini ya Program hii ya kitaifa *(Makofi)*

**MHE. DUSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika sana na majibu mazuri na Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kuna baadhi ya pampu za maji zilizokuwa zimejengwa miaka kadhaa ya nyuma zimeharibika, kama pale Namagurubi, Ngarakate, Nakole, na sehemu nyingine kwa mfano Ngalinje, ambazo pampu zake zimeharibika muda mrefu sana. Je, Wizara inaweza kusaidia kukarabati pampu hizi ili wananchi wake waweze kupata maji safi. Swali la pili, kwa kuwa Ofisi ya pale Mangaka, haina maji kabisa na ninategemea kwamba Mkuu wa Wilaya hivi karibu atahamia pale. Je, Wizara inasemaje kuhusu hili, ili Mkuu wangu wa wilaya asipate adha ya kukosa maji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pampu za maji zilizoharibika, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge, kwa kupitia programu yetu ya maji, ambapo tuna programu maalum, ambayo tunaiita *quick wins,* ambayo ni kwa ajili ya Miradi ya ukarabati. Ninamwomba awasiliane na Halmashauri yake, ili kuhakikisha kwamba katika orodha ya Miradi ya *quick wins* watakayotuletea, awamu itakayofuatia na huu mradi uwe umo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, kukosa maji, ni jambo ambalo kwamba, mimi pamoja na Wizara yangu tutajaribu kuangalia chanzo chenyewe ni nini na pia tuweze kujua kitu gani kinachoweza kikatendeka. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya mpya ya Nanyumbu, ilikuwa katika Wilaya ya Masasi, na matatizo yake yanafanana sana na yaliyoko katika Wilaya ya Masasi hasa upande wa Masasi Magharibi, katika vijiji vya Lukuledi, Mpanyani, Namajani, Namatutwe, Nambawala, Chiwale na kadhalika.

Je, Serikali, au Wizara ya Maji, ina mpango gani kupunguza matatizo katika maeneo haya na hasa hasa kwa sababu *rig* lililopo katika Wilaya ya Masasi hivi ni kukuu sana na haliwezi kusaidia katika kuchimba visima virefu na vifupi katika sehemu hizo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vijiji alivyovitaja, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge, ya kwamba kwa awamu na vyenyewe viingizwe katika programu ya maji na usafi wa mazingira. Hata hivyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Mtwara, kwamba kwa hivi sasa Serikali ikishirikiana na Serikali ya Japan, tunafadhili Miradi mingi sana ya maji. *(Makofi)*

Kwa mfano kwa Mtwara tunafadhili Miradi katika vijiji 37 na hiyo kwa sasa hivi imetuchukulia sehemu kubwa ya shughuli za kufanya katika Wilaya husika za Mtwara. Kwa hali hiyo ninamwomba avute subira na hizo aziingize katika programu ziende kila moja kwa zamu ili tuweze kuhakikisha kwamba vijiji vyote vya huko na vyenyewe vimefadhiliwa na kupata maji. *(Makofi)*

Na. 132

**Ulipaji wa Mafao ya Wastaafu wa East Afrika**

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Tatu ilianza kulipa mafao ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwaka 1977; na kwa kuwa mafao hayo hulipwa kwa awamu na Serikali ya Awamu ya Nne imeahidi kuendelea kutoa malipo hayo:-

Je, ni kiasi gani cha fedha ambayo kinalipwa kwa awamu ya kwanza na kiasi gani cha fedha kinamalizia malipo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB**) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Masharika iliyovunjia hayakuwa na awamu mbili isipokuwa yaliwahi kulipwa mwaka

1999 ambapo wastaafu hawakuridhika na malipo hayo ndipo Serikali baada ya majadiliano na Kamati ya Muafaka ikaamua kupitia upya madai yao.

Serikali ilizingatia haki zilizoainishiwa kisheria na kuongeza riba ya malipo toka asilimia 7 iliyopitishwa na Dr. Umbricht hadi kufikia asilimia 17.53% ambayo ni wastani wa riba kwa dhamana za Serikali kwa miaka 25 kuanzia 1977 hadi 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi kilichokwishalipwa hadi kufikia Agosti, 2006 ni shilingi bilioni 117 kwa wastaafu 35,417. Hata hivyo, yafuatayo yanaendelea kufanyika:-

(i) Mirathi inaendelea kushughulikiwa kadri warithi wanavyojitokeza ambapo jumla ya mirathi 6,815 yenye kiasi cha shs.25,000,000,000 imekwishalipwa;

(ii) Wastaafu wa Mikoani ambao nyaraka zao zilikuwa haijakamilika bado wanaendelea kuziwasilisha Hazina kupitia kwenye Mashirika husika;

(iii) Wastaafu ambao majalada yao hayakuletwa katika kipindi cha ukokotoaji wanaendelea kuyawasilisha kutoka kwenye Mashirika husika; na

(iv) Wastaafu ambao hawakustahili kulipwa katika kipindi cha ukokotoaji kwa sababu ya kukosa kumbukumbu wanaendelea kujitokeza na Mashirika husika yanaendelea kuwatafutia kumbukumbu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastaafu 7,544 ambao malipo yao yako tayari bado hawajajitokeza kuchukua mafao yao hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasimamizi wa mirathi wanaombwa wajitahidi kumaliza taratibu za mirathi ili malipo yao yafanyike na wale walio hai wajitokeze kupitia kwenye Mashirika yao ili waweze kutambuliwa huko na hatimaye kulipwa mafao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba malipo haya hulipwa kwa kuzingatia taratibu za kulipa mafao. Ili kufanikisha hili, kumbukumbu za mhusika ni muhimu ili kuepuka kulipa wasiohusika. Serikali kwa kushirikiana na Mashirika husika na wahusika wenyewe inaendelea na zoezi hili ili kulifanikisha.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba fedha zimetengwa na bado kuna wastaafu hawajakamilisha kumbukumbu zao; na kwa kuwa wastaafu wengi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao tumeshuhudia katika magazeti na tumeshuhudia katika sehemu za

Serikali zinazohusika kuwashughulikia, wengi wao wakati huo walipostaafu walikwenda Vijijini na walipoteza kumbukumbu zao.

Lakini wanakumbuka namba zao za kazi. Watu hao wamekwenda katika Masharika husika na wanambiwa mafaili yao hayaonekani na wanaambiwa kwamba Wizara ya Fedha ndiyo itakuwa na kumbukumbu zao. Wakifika Wizara ya Fedha vilevile wanakatishwa tamaa kwa kuambiwa hawawezi kulipwa kwa kukumbuka namba tu.

Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutueleza kwamba Serikali ina mpango gani kuwathibitisha hao ambao ni kweli walifanya kazi katika iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao wana namba na majina yao kwa kweli yapo Serikalini. Ni mikakati gani watafanya ili wapate haki zao na wamekata tamaa na wanatia huruma na Serikali inazidi kupata aibu kwa malalamiko ya wananchi wake?

Mkataba wa Dr. Umbricht ulikuwa ni wa kulipa mgawanyo wa Afrika Mashariki kwa nchi zote tatu. Tanzania, Uganda na Kenya. Kenya na Uganda tayari walishalipa wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki miaka 29 iliyopita. Je, ni kigezo gani ambacho Tanzania hadi leo imekuwa kama kitendawili kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki wasilipwe fedha zao likaondoka tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB)**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza utaratibu wa malipo yoyote kutoka Serikalini lazima ufuate ushahidi wa vitambulisho vilivyopo. Bila ya kuwa na kitambulisho chochote ni kinyume cha sheria ya Uhasibu na siyo lazima kulipa na ukahakikisha kwamba yule anayelipwa ndiye mtu mwenyewe hasa.

Katika zoezi hilo, vilevile wamejitokeza watu ambao si waaminifu na wamekuja na vinavyoitwa vitambulisho kutoka katika Mashirika yao na wamelipwa. Hayo tunakiri yametokea, lakini lazima tuhakikishe kwamba anayekuja na kitambulisho na vitambulisho kama nilivyosema katika jibu langu la msingi. Vitambulisho vipo katika Masharika waliyokuwa wanafanyia kazi. Yale Mashirika ndiyo yatakayotuthibitisha sisi. Sisi bila ya vitambulisho vinavyomhusika yeye Wizara ya Fedha haiwezi kulipa. Hilo la kwanza.

La pili, kwa nini Serikali imekaa miaka yote hiyo haijalipa hao wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya Afrika Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifungua kesi na kwa sababu kesi ilikuwa Mahakamani, Serikali haikuweza kutoa uamuzi mpaka kesi ile imalizike. Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliyepita alipoulizwa na *Radio BB C* kwamba vipi hao watu watalipwa lini? Alisema kabisa kwamba wakiondoa kesi yao Mahakamani hilo watalizungumza. Ni kweli ulikuja ujumbe hapo niliupokea mimi, nikawambia masharti ni hayo, kitu kilichokuwa Mahakamani hatuwezi tukakijadili na tulifikia hatua tukakubaliana na hayo makubaliano ya fedha hizo

kulikuwa na *need of settlement* baina ya Serikali na wao iliyofanyika Mahakamani kwamba tutalipana kwa mpango huo na kwa kufuata taratibu hizo. Kwa hiyo, tuliyoyafanya tuliyafanya kisheria. *(Makofi)*

Na. 133

**Wahamiaji Haramu wa Mifugo**

**MHE. GOSBERT B. BALANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Karagwe ni wafugaji wa Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo; na kwa kuwa majosho yote yaliyokuwepo hayatumiki kwa sababu ya ubovu na uhaba wa madawa; na kwa kuwa eneo la malisho limevamiwa na wahamiaji haramu wa mifugo kutoka nchi jirani:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuwaondoa wahamiaji haramu na mifugo yao katika eneo la Karagwe?

(b) Je, ni nani aliyewaruhusu wahamiaji hao kuleta mifugo yao katika ardhi ya Tanzania?

(c) Je, ni lini Serikali itakarabati majosho yote na kutoa madawa ya kutosha kwa mifugo Jimboni Karagwe?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshmiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba eneo la malisho katika Wilaya ya Karagwe limevamiwa na wahamiaji haramu kutoka nchi za Rwanda, Burundi na Uganda. Wilaya ya Karagwe ina jumla ya ng'ombe 145,318, mbuzi 79,053 na kondoo 4,619. Pia kulikuwa na ng'ombe 42,550, mbuzi 8,920 na kondoo 2,100 wa wahamiaji haramu.

Serikali kupitia uongozi wa Mkoa wa Wilaya inachukua hatua za kuwarudisha wahamiaji hao pamoja na mifugo yao kwenda walikotoka, ambapo hadi kufikia mwezi Oktoba, 2006 ng'ombe 3,295 na mbuzi 70 walirudishwa kwenda Rwanda na zoezi linaendelea.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna taasisi ama mtu yeyote aliyewaruhusu wahamiaji hao kuleta mifugo yao katika ardhi ya Tanzania.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Karagwe ina majosho 30 kati ya hayo majosho 11 hayafanyi kazi kutokana na uchakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianzisha utaratibu wa Halmashauri kuibua miradi yao ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ile ya kuendeleza Sekta ya mifugo kuanzia mwaka 2003/2004 kupitia Mipango ya Kuendeleza Kilimo Wilayani *(DADPs).* Katika mipango hiyo ya Serikali iliziagiza Halmashauri zote nchini kuibua miradi itakayotatua matatizo yanayowakabili wafugaji kwa njia shirikishi ikiwa ni pamoja na miradi ya kujenga na kukarabati majosho. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe haikuibua miradi ya kukarabati majosho kwa mwaka 2003/2004 na 2004/2005 bali ilipanga kutekeleza miradi mingine ikiwamo kuchimba malambo, kuendeleza mashine za kukoboa kahawa, kuimarisha *SACCOS* na kuzalisha mbegu za mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mipango hiyo ya *DADPs* Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe katika mwaka 2005/2006 ilitengewa jumla ya shilingi milioni 1.2 kwa ajili ya ukarabati wa josho moja. Katika mwaka 2006/2007 jumla ya shilingi milioni 12 zimetengwa kwa ajili ya kukarabati majosho manne katika vijiji ya Nkwenda, Kahundwe, Kashanda na Nyaishozi.

Serikali itaendelea kujenga na kukarabati majosho katika Halmashauri zote zenye mahitaji kupitia Mpango *DADPs* sambamba na kutoa ruzuku ya madawa ya kuogeshea mifugo.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Zoezi la kuondoa wafugaji haramu katika Wilaya ya Karagwe lilipokelewa kwa furaha kubwa sana na wananchi wa Karagwe. Lakini kwa bahati mbaya zoezi hili liliingiliwa na watendaji wenye nia mbaya, na watendaji hao ni kwamba badala ya kuwaondoa mifugo ya wahamiaji haramu kutoka nchi jirani, wao walianza kukamata mifugo ya raia wa Tanzania yaani wananchi wa Karagwe na kuwatoza fedha nyingi sana. Kwa mfano, kuna ndugu Salvatory Karabamu yeye alitozwa shilingi milioni 3 na akapewa risiti na hizo fedha zimekusanywa kiasi cha shilingi milioni 170. Hatimaye fedha hizo zimeishia mifukoni mwa wajanja wachache. Je, Serikali inalijua hilo na kama inalijua imechukua hatua gani?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya Serikali kuwahamisha wafugaji wahamiaji kutoka nchi za nje ni kwa ajili ya kutoa nafasi kwa wananchi kuwa na malisho ya kutosha kwa mifugo yao. Zoezi hili kama alivyojibu vizuri Naibu Waziri limefanywa kwa uangalifu na kwa umakini mkubwa kuhakikisha kwamba hakutakuwepo na athari yoyote kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu katika Mkoa wa Kagera wananchi ambao wapo pale Mkoa wa Kagera ni wananchi ambao kila kabila wanafanana sana na wananchi wa nchi hizo za jirani kama Rwanda, Burundi na Uganda pia. Kwa hiyo, katika zoezi la kuwahamisha watendaji imewawia kazi ngumu sana kupambanua kati ya Mtanzania na asiyekuwa Mtanzania. Tumetegemea sana ujuzi na umahiri wao katika kufanya hivyo kwa sababu baadhi ya wananchi wanaotoka nchi za jirani wana

ndugu zao katika Mkoa wa Kagera, kama vile mashangazi, wajomba na watu wengine. Kwa hiyo, katika hali ya kusaidiana imekuwa kazi kubwa kwa watendaji kuhakikisha kwamba wanamudu kuwaondosha wale wageni na kuwazuia wananchi wengine kuwaficha hao wafugaji wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nimjibu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kama makosa yametokea Serikali itajitahidi kuhakikisha kwamba suala hilo linafuatiliwa kwa karibu. Lakini kwa ujumla ni kwamba kuna wananchi ambao hawakukubali kuwatoa moja kwa moja watu wengine ambao si wananchi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 134

**Barabara inayopita katikati ya Mbuga za Wanyama za Serengeti na Ngorongoro**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na malalamiko mengi toka kwa wana mazingira na wafanyabiashara kuhusiana na barabara inayokatisha katikati ya mbuga za wanyama za Serengeti na Ngorongoro:-

Je, Serikali imefanya juhudi gani kuangalia uwezekano wa kutengeneza barabara mpya itakayopita kwa sehemu kubwa nje ya hifadhi hizo na kuwaondolea watalii adha ya kupita njia hiyo wakati wa kwenda na kurudi kwenye mbuga hizo na kuboresha utalii, uhifadhi wa barabara kati ya Mikoa ya Arusha na Mara?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi, Mbunge wa Jimbo la Ludewa kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuepusha barabara kupita ndani ya Mbuga za Wanyama na kwa kutumia mkopo kutoka Benki ya Dunia, kati ya mwaka 1999 na 2000 ulifanyika upembuzi yakinifu kati ya Mji wa Karatu kupitia Oldeani hadi Lalago, upembuzi yakinifu huo ulionyesha kuwa itakuwa ni gharama kubwa kupitisha barabara ya lami maeneo hayo. Baada ya kuona kuwa barabara mbadala ya kupita Magharibi mwa Mbuga itakuwa ghali, Serikali imeamua kufanya upembuzi yakinifu mwingine wa kupitisha barabara Mashariki mwa Mbuga husika.

Hivyo, Serikali kwa kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* imesaini mikataba miwili tarehe 11/8/2006 na makampuni ya *Inter Consult* Tanzania *Limited* na *Crown Tech. Consult Limited*, zote za Tanzania kwa ajili ya upembuzi yakinifu kwa barabara kati ya Natta – Mugumu -Tabora B – *Kleins Camp- Loliondo* hadi Mto wa Mbu yenye urefu wa kilometa 452. Kazi ya upembuzi yakinifu inatarajiwa kukamilika tarehe 9/5/2007 na katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 jumla ya shilingi milioni 400 zimetengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya upembuzi yakinifu ndiyo yatachambua masuala yote ya kiuchumi, mazingira na kutoa mapendekezo kwa Wizara kuhusu athari au faida za kupita kwa barabara hii ndani ya hifadhi, uharibifu wa mazingira na kutoa mapendekezo ya barabara mbadala itakayopita nje ya mbuga kama italazimu kufanya hivyo.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa vile barabara hasa mpya zinazopita kwenye maeneo ya Hifadhi na hasa Hifadhi zinazokuwa zina wanyama wanaohama hama kama ilivyo Serengeti na hasa wanyama hao wanapohama kutoka nchi moja hadi kwenda nchi nyingine. Je, katika upembuzi yakinifu ambao umezungumzwa na Naibu Waziri ni juhudi gani zinafanywa kuhakikisha kwamba wadau wote na hasa wadau wa muhimu kama vile TANAPA, Ngorongoro *Wildlife Division* wanahusishwa kikamilifu katika upembuzi huo kuhakikisha kwamba hakuwi na athari kubwa kwa wanyama hao wanaohamahama?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Mbuga kama Serengeti kuna wanyama wanaohamahama na wanapita hata mipaka ya nchi yetu kwenda nchi nyingine. Lakini vilevile ni kweli na ni muhimu basi katika mazingira hayo wadau wote wanaohusika waweze kuwa *involve*d katika suala nzima la upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama nilivyosema makampuni hayo mawili, Inter *Consult* pamoja *Crown Tech. Consult* wameagizwa katika Mkataba kwamba wanapofanya upembuzi yakinifu wawahusishe wadau wote wakiwemo pamoja na *TANAPA* na Hifadhi ya Serengeti ili kuweza kupata mawazo kutoka kwa wadau hao na baadaye upembuzi yakinifu utakapokuwa umekamilika basi na mawazo na mapendekezo ya wadau kuhusu namna ya *control immigration* ya hao wanyama iwe namna gani. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi kwamba suala hilo litazingatiwa na wadau wote watahusishwa.

Na. 135

**Matatizo katika Ajira ya Walimu**

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika historia ya ajira ya walimu imebainika kuwa walimu wamekuwa na matatizo mengi katika ajira na ulipwaji wa maslahi yao; na kwa kuwa, katika nyakati tofauti malalamiko ya walimu yamekuwa katika ukosefu wa chombo kimoja cha kuwahudumia kikamilifu. Urasimu uliopo katika ajira unatokana na kuajiriwa na Serikali, watu binafsi na Taasisi mbalimbali:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani madhubuti sasa wa kutatua matatizo hayo ikizingatiwa kuwa ripoti ya Tume ya Rais ya mfumo wa Elimu Nchini ya 1982 na ripoti ya Tume ya Waziri Mkuu ya 2004 zimekuwa zikiendelea kubainisha matatizo hayo?

(b)Kwa kuwa, idadi ya shule za sekondari na walimu imeongezeka sana; je, Serikali ina mpango gani wa kusogeza huduma za utawala na vifaa kwa shule na walimu kwenye ngazi ya Wilaya na Mkoa badala ya utaratibu wa sasa wa kuwa chini ya Katibu Mkuu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Shaaban Kwaangw' Mbunge wa Babati Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Tume zilizoundwa kufuatilia kero za walimu ikiwa ni pamoja na Tume iliyoongozwa na Mheshimiwa Omar Shabaan Kwaangw' mwaka 2004 zilibaini kuwa kukosekana kwa chombo kimoja cha kuwahudumia walimu; ni moja ya chanzo cha kero za walimu. Serikali inayafanyia kazi mapendekezo ya Tume hizo. Hivi sasa zimenundwa Kamati Maalum ndani ya Wizara kushughulikia suala hili ikiwa ni pamoja na kwenda nchi jirani kujifunza jinsi walimu wanavyohumiwa.Kamati ikimaliza kazi yake tutawashirikisha wadau ili tuweze kupata utaratibu mzuri zaidi ikiwa ni pamoja na kuwa na chombo kimoja cha kuwahudumia walimu iwapo itaonekana inafaa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeliona tatizo la Makao Makuu ya Wizara kuwahudumia walimu wa shule za sekondari ambao kwa sasa ni wengi. Uamuzi wa Serikali wa kuwa na Waratibu wa shule za sekondari katika kila Wilaya ni hatua ya awali ya kushusha huduma za utawala karibu na walengwa wakiwemo walimu na wanafunzi.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu yenye matumaini kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini naomba kuuliza swali ndogo tu la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya uendeshaji wa shule za sekondari na hasa vilevile Mpango wa MMES ambao sasa unaendelea kuna matatizo mengi sana kwenye Mpango huo. Je, ni lini sasa Serikali itaharakisha kuteua hao waratibu ili matatizo mengine ya walimu pamoja na ya MMES yaweze kushughulikiwa mapema iwezekanavyo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niongezee katika yale aliyoyazungumza vizuri tu Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutokana na swali la msingi la Mheshimiwa Omar Kwaangw'.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe taarifa kwenye Bunge lako Tukufu kwamba waratibu wameishateuliwa kilichobakia sasa ni kwenda kuanza kazi. Tunategemea kwamba ifikapo tarehe 1 Januari, 2007 watakuwa wameishaanza kazi chini ya ofisi za Ma-*DC*. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira kidogo mwezi Januari, mwakani watakuwa ofisini tayari kwa kuanza kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mafupi. Tunaendelea muda unanipa shida.

Na. 136

**Kuanzishwa Kambi ya Kijeshi Kongwa**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Kongwa una historia ndefu ya mafunzo ya Kijeshi kwa wapigania uhuru wa Kusini mwa Afrika na mafunzo ya kijeshi kwa Askari wetu wa JWTZ kwa miaka zaidi ya 30; na kwa kuwa wananchi wa Kongwa wanapenda sana kuwepo Kambi ya JWTZ/JKT Kongwa na wako tayari kutoa ardhi kwa madhumuni hayo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Kambi ya Kijeshi ya JWTZ au JKT Wilayani Kongwa?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Jimbo la Kongwa, naomba kwanza kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mji wa Kongwa una historia ndefu inayohusiana na mafunzo kwa ajili ya wapigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika pamoja na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Sehemu ya historia hiyo ya Mji wa Kongwa ni pamoja na kuanzisha kambi ya wapigania uhuru ambayo ilikuwa ni miongoni mwa kambi za awali zilizoanzishwa hapa nchini. Kambi hii ilitoa mafunzo kwa wapigania uhuru wa Msumbiji, Zimbabwe, Angola, Namibia na Afrika Kusini.

Aidha, kabla ya wapigania uhuru kuwasili katika kambi hii mnamo mwaka 1964, kwa ajili ya kuanza shughuli zao, Marehemu baba wa Taifa, Mwalimu Julius

Kambarage Nyerere alifanya ziara katika eneo la kambi, wakati huo akifuatana na Rais wa kwanza wa Algeria, Marehemu Ahmed Bembela.

Vilevile, katika mwaka 1967, Kambi ya Kongwa pia ilipata bahati ya kutembelewa na Rais wa mwaka 1967, Kambi ya Kongwa pia ilipata bahati ya kutembelewa na Rais wa Misri, Marehemu Gamar Abdi Nassar wa Misri.

Kadhalika, kuna viongozi mashuhuri waliopata fursa ya kulala katika kambi ya Kongwa. Viongozi hao ni pamoja na Rais wa kwanza wa Msumbiji, Marehemu Samora Machael na Rais wa kwanza wa Namibia, Mheshimiwa Sum Nujoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya wapigania uhuru kuondoka kwenye kambi ya Kongwa, historia inatuambia kuwa, Jeshi la Wananchi wa Tanzania liliendelea kuitumia kambi hiyo kwa kuendesha mafunzo mbalimbali ya kijeshi hadi mwaka 1994. Kwa sababu wananchi wa Kongwa walikuwa mstari wa mbele katika kutoa eneo hilo pamoja na kuwasaidia wapiganaji, nachukua fursa hii, kuwashukuru sana wananchi wa Kongwa kwa juhudi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Jimbo la Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wakati huu, Serikali haina mpango wa kuanzisha Kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika eneo hilo. Kwani uanzishwaji wa Kambi unazingatia zaidi mikakati na vigezo vya kiulinzi na kiusalama. Hata hivyo, katika mipango yetu ambayo inalenga katika kuongeza Kambi za JKT eneo hilo la Kongwa tutaliangalia na kulifanyia tathmini, kama litaonekana kutosha na kufaa kwa shughuli mbalimbali za uzalishaji mali za JKT, tutaliingiza katika mpango huo.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, na namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana yanayotia moyo kwa wananchi wa Kongwa. Kama alivyosema kwa vile Rais wa sasa wa Namibia aliishi Kongwa kwa muda mrefu na Rais wa kwanza wa Msumbiji aliishi Kongwa kwa muda mrefu.

Lakini vilevile wapigania uhuru wa Zimbabwe, Afrika Kusini na Angola. Lakini toka nchi hizo zimepata uhuru haijawahi kutokea katika ziara rasmi za viongozi wakawepo hata watu wawili, watatu wa Kongwa au hata Mbunge wao kufuatana na ziara za viongozi kwenda katika nchi hizo za Kusini mwa Afrika. Je, Serikali itakubali ikitokezea nafasi angalau basi na sisi wa Kongwa tukaenda kuona wenzetu hao? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, maombi hayo tumeyasikia na tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Na. 137

**Wanajeshi WanaostaafuU**

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBON** aliuliza:-

Kwa kuwa wanajeshi wengi wanastaafu wakati bado ni vijana wenye nguvu na uwezo mzuri wa kutumikia Jeshi:-

(a) Je, ni utaratibu gani unaotumika wa kuwastaafisha wakati bado ni vijana?

(b) Kwa kuwa hali ya Wanajeshi mara baada ya kustaafu zinakuwa mbaya. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wastaafu hao?

(c) Je, Serikali haioni kuwa kuwastaafisha wanajeshi hao wakati wakiwa vijana ni kuongeza majambazi katika nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Amour Chombon, Mbunge wa Jimbo la Magomeni lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu unaotumika wa kuwastaafisha wanajeshi upo kwa mujibu wa sheria ya Jeshi. Sheria na kanuni za Jeshi zinaelekeza kwamba mwanajeshi atastaafu kwa mujibu wa cheo alichonacho na umri wake. Umri na cheo ambacho kimepangwa ni kama ifuatavyo:-

(1) Brigedia Jenerali kwenda juu -Atastaafu akiwa na umri wa miaka 57;

(2) Kanali – Atastaafu akiwa na umri wa miaka 55;

(3) Luteni Kanali - Atastaafu akiwa na umri wa miaka 53;

(4) Meja – Atastaafu akiwa na umri wa miaka 51;

(5) Kapteni – Atastaafu akiwa na umri wa miaka 49;

(6) Luteni – Atastaafu akiwa na umri wa miaka 47;

(7) Afisa mteule daraja la kwanza – Atastaafu akiwa na mika 57;

(8) Afisa Mteule daraja la pili – Atastaafu akiwa na umri wa miaka 53; na

(9) Askari wa kawaida hadi Sajini– Atastaafu akiwa na miaka 51.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, wanajeshi wastaafu hulipwa haki zao kama wastaafu wengine ili ziweze kuwasaidia katika maisha baada ya kustaafu. Aidha, katika mipango ya kila mwaka ya Serikali, kuna fursa nyingi ambazo pia huwasaidia wastaafu. Baadhi ya fursa hizo ni pamoja na mikopo midogo midogo inayotolewa pamoja na mafunzo kwa wajasiriamali.

Vile vile, Serikali mara kwa mara huongeza viwango vya pensheni kwa lengo la kuwasaidia wastaafu. Licha ya juhudi hizo, mstaafu wa Jeshi anaweza pia kuajiriwa katika sekta nyingine kama ana sifa zinazohitajika. Hata hivyo napenda kuwashauri wanajeshi wote kujiwekea msingi mzuri wa maisha kabla ya kustaafu, hasa katika kujiendeleza kielimu katika fani walizonazo ili ziweze kuwasaidia baada ya kustaafu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa hakuna sababu ya msingi za kuamini kwamba mwanajeshi mstaafu huongeza idadi ya majambazi nchini. Aidha, kwa kuzingatia asili ya kazi ya jeshi, mwanajeshi anapostaafu hupewa waraka ambao unamkumbusha na kumtaka awe mwananchi mwema, tabia nzuri pamoja na kufuata sheria za nchi. Pia katika waraka huo, mwanajeshi anakumbushwa kwamba, iwapo atavunja sheria za nchi atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Kwa kuzingatia waraka huo, wanajeshi wengi waliostaafu wamekuwa ni wananchi wazuri na wenye kufuata sheria na taratibu za nchi. Vile vile, napenda ieleweke kwamba Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ni chombo chenye nidhamu ya hali ya juu. Tangu jeshi hili lilipoanzishwa mwaka 1964, maelfu ya wanajeshi wameishastaafu na bado wanaendelea kuwa ni wazalendo na wanaoheshimika katika nchi hii. Baadhi ya wastaafu hao ni viongozi wa nchi hii na wengine ni Wabunge ambao wanawakilisha jamii zetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umekwisha. Tulichojifunza leo, Mawaziri wanajitahidi kujibu maswali yao kwa kifupi. *Problem* iko kwenye maswali ya nyongeza, zinakuwa hotuba. Kwa hiyo, tukifanya hivyo unakuta basi tunafanya kwa kukimbizana badala ya kuuliza maswali. Kwa hiyo, nawaombeni Wabunge muwe mnauliza maswali ya nyongeza siyo hotuba za nyongeza. Kwa hiyo, nadhani tumeelewana. *(Mkofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mengi. Kwanza naanza na yale ya mikutano. Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Gideon A. Cheyo aonamba wajumbe wake wakutane saa 5.30 leo katika ukumbi 231. Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, anaomba kuwatangazia wajumbe wa Kamati yake kuwa leo baada ya kikao hiki saa 4.30, wakutane katika ukumbi namba 133. Tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Wabunge wa CCM, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed. Anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wa CCM Wanawake kuhudhuria pia kikao cha uchaguzi mara baada ya kusitisha kikao saa 7.00 mchana, katika ukumbi wa Pius Msekwa (Ukumbi wa Zamani wa Bunge). Mheshimiwa Ameir ni mjumbe wa Kamati ya Wabunge Wanawake, kwa hiyo msi......... ndio. Mheshimiwa *Privileged* huyo! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, anaomba wajumbe wake wakutane saa 5.00 Asubuhi hii katika Ukumbi Namba 227 ghorofa ya pili.

Mheshimiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, anawaomba wajumbe wake wakutane leo saa 6.00 mchana katika ukumbi namba 219 ghorofa ya pili. Haya ndiyo matangazo ya mikutano. Nina matangazo kibao ya wageni! *(Makofi)*

Kwanza kabisa, kuna Wanafunzi wa Sekondari ya Handali – Mvumi, Mkoa wa Dodoma, wasimame kama wapo na walimu wao! Mheshimiwa Dr.Harrison Mwakyembe ana wageni wake, Wanachama wa Chama cha Ushirika wadogowadogo (VIKOBA). Nao naomba wasimame wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi ana wageni wake wafanyabishara ndogo ndogo, wasimame! Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu ana wageni wake, wasimame! Hapa kuna Mary Mashala, Michael Mashala na msaidizoi wake.

Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, ana wageni wake akianzia na *partner* wake-mke wake, halafu na wasaidizi wake. Kama nina wageni wengine nimewasahau, naomba niwakaribisheni katika Bunge letu, ni Bunge la watu wote, mnaruhusiwa kuja kuona kwa wakati wote, si lazima kwa kukaribishwa.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *Speaker's Guidance!* Nataka msaada wako kidogo unifahamishe, bado sijaelewa. Wakati linaulizwa swali katika Bunge na kwa bahati aliyeuliza swali alikuwa ana swali la nyongeza, ina maana kauliza swali lakini kwa bahati alikuwa na swali la nyongeza.

Sasa hatuoni kwamba yule kutompa fursa wakati swali lake la msingi tumemyima haki kwa sababu ina maana hakupata ufafanuzi katika swali lake. Hatuoni kwamba ni vizuri kuweza yule kumpa nafasi akauliza. Labda yule mwingine anayetaka kuuliza la nyongeza ndiye akanyimwa nafasi ile. Ninahitaji kupata maeleo tu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana. Huo ndio utaratibu. Kinachotokea, kama mtu aliuliza swali la msingi, yeye ndiye atakuwa wa kwanza kupewa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, tena si moja, mawili, halafu wengine ni moja tu.

Lakini, yule atakayekuwa ameuliza swali la msingi kama huyu aliyeuliza wa mwisho na muda umekwisha, ndiye aliyenyimwa fursa kwa kuwa muda ulikuwa umeisha. Nadhani ndiye huyo tu, kama tumekosea tutakuwa tumekosea kwa bahati mbaya, lakini utaratibu ndio huo uliousema wewe. *(Makofi)*

## MISWADA WA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu wa Mwaka 2006
### *(The Anti-Money Laundering Bill, 2006)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu yaani *(The Anti – Money Laundering Act, 2006)* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote waliotoa michango yao wakati wakichangia katika Semina iliyoandaliwa na Wizara ya Fedha siku ya Jumamosi tarehe 11 Novemba 2006. Naishukuru pia Kamati ya Muda ya Kitaifa ya Udhibiti wa Fedha Haramu yenye wajumbe kutoka Wizara za Fedha, Sheria na Katiba, Usalama wa Raia, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu – Zanzibar, Benki Kuu ya Tanzania na Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana kwa kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya Muswada huu.

Vilevile nawashukuru Wadau na washauri mbali mbali katika sekta ya fedha ambao kwa nyakati tofauti, wametoa ushauri na mapendekezo yao kwa lengo la kuuboresha Muswada huu. Aidha, namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalamu wake kwa ushirikiano wao mkubwa walioonyesha wakati wa maandalizi na kuwasilisha Muswada huu mbele ya Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba, tumezingatia kwa dhati michango ya Kamati ya Fedha na Uchumi na ile iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wengine wakati wa Semina ambayo imesaidia sana kuuboresha Muswada huu. Vile vile nawashukuru sana wadau mbalimbali ambao wametoa ushauri wao ambao kwa kiwango kikubwa tumeuzingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu una lengo la kuharamisha *(criminalize)* mapato ya fedha na mali itokanayo na biashara na vitendo vya kihalifu na kubainisha adhabu zake. Biashara ya Fedha haramu ni utaratibu unaotumiwa na wahalifu kuficha chanzo halisi cha mali au mapato yatokanayo na vitendo vya kihalifu kwa kufanya mali au mapato hayo yaonekane kama yalipatikana kwa njia halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chimbuko la Muswada huu ni kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu pamoja na uhalifu wa kimataifa ulimwenguni ikiwemo Tanzania. Biashara ya Fedha Haramu ni tishio kwa uchumi na usalama duniani, kwani hudhoofisha mfumo wa uchumi, huyumbisha Serikali zilizoko madarakani kwa kununua viongozi walioko madarakani na kijamii, huathiri maisha ya wananchi. Kufuatia hali hii, Umoja wa Mataifa ulipitisha mkataba dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa yaani *The United Nations Convention Against Transnational Organized Crime and the Protocols Thereto* wa mwaka 2000.

Mkataba huu umeainisha makosa mbalimbali ya uhalifu wa Kimataifa ikiwemo biashara ya fedha haramu na kuzielekeza nchi Wanachama kuchukua hatua madhubuti za Kisheria na nyinginezo kukabiliana na vitendo hivyo. Tanzania ni mojawapo ya nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa zilizotia saini mkataba huu na kuuridhia kupitia Azimio la Bunge Na. 14/2005.

Aidha nchi nyingi duniani zimeungana kikanda kudhibiti vitendo vya uhalifu vinavyozalisha fedha haramu. Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika mnamo mwaka 1999 zilianzisha Umoja ujulikanao kama Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika za Udhibiti wa Fedha Haramu *(The Eastern and Southern Africa Anti-Money Laundering Group)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Umoja huu una jumla ya nchi 14 wanachama za Afrika Kusini, Botswana, Kenya, Lesotho, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Shelisheli, Swaziland, Tanzania, Uganda, Zambia na Zimbabwe, ambapo makao Makuu ya Sekretariati yapo mjini Dar es Salaam, Tanzania. Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa Makao makuu ya Sekretariati ya Umoja huu nchini kwetu ni kielelezo thabiti cha azma ya Serikali ya Tanzania kupambana na uhalifu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madhumuni ya Muswada huu ni kupendekeza kutunga sheria madhubuti yenye kuzingatia viwango vya kimataifa vya udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu kwa kuharamisha mapato na mali yote itokanayo na biashara na vitendo vya kihalifu na kubainisha adhabu zake. Aidha, Muswada unaanzisha chombo cha Kiserikali cha uchunguzi *(Financial Intelligence Unit (FIU)* kitakachopokea taarifa mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi zenye mwelekeo wa mashaka *(suspicious transaction reports)* kuhusiana na fedha haramu, kuzichambua na kuziwasilisha katika vyombo husika kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaeleza maudhui ya Muswada, naomba kutoa maelezo kwamba suala la udhibiti wa biashara ya fedha haramu si geni hapa nchini. Itakumbukwa kwamba Bunge lako tukufu lilipitisha Sheria ijulikanayo kama *The Proceeds of Crime Act,* Sura Namba 256 (Toleo la 2002). Chini ya sehemu ya saba, kifungu cha 71 cha Sheria hii, mali na mapato yote yatokanayo na biashara na vitendo vya kihalifu vinavyozalisha fedha haramu hususan biashara ya madawa ya kulevya vimeharamishwa, na kwamba mtu yoyote anayejihusisha na biashara ya fedha haramu anatenda kosa la jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, hata hivyo, mtakubaliana nami kwamba tangu Sheria hii itungwe mwaka 1991 wigo wa biashara na vitendo vya kihalifu vinavyozalisha fedha haramu umepanuka sana, kama mlivyoshuhudia katika Semina iliyotolewa Jumamosi hususan katika mada ya *typologies on money laundering*, yaani, mbinu mbalimbali zinazotumika na wahalifu katika kusafisha fedha haramu.

Hivi sasa, fedha haramu hazitokani tu na biashara haramu ya uuzaji wa madawa ya kulevya bali ni pamoja na vitendo vya rushwa, biashara ya silaha haramu *(illicit arms trafficking)*, biashara haramu ya kuuza binadamu na viungo vyake, ujambazi wa kutumia

silaha, vitendo vya kughushi, uchapishaji na utawanyaji wa fedha bandia, biashara ya magendo, usafirishaji wa wahamiaji haramu, rushwa na ufadhili wa ugaidi. Kutokana na hali hii, ni dhahiri kwamba kuna haja ya kuwa na Sheria madhubuti itakayokidhi mahitaji ya wakati huu katika kukabiliana na biashara na vitendo vya uhalifu vinavyozalisha fedha haramu ambazo matokeo yake yana athari kubwa kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa pia hivi karibuni katika mkutano uliofanyika mjini Arusha wa Umoja wa Wabunge Duniani dhidi ya Rushwa *(GOPAC)* wenye makao yake makuu nchini Canada ambapo Tanzania ni mwanachama, Umoja huu uliazimia kuziomba nchi wanachama kutunga Sheria madhubuti za udhibiti wa biashara ya fedha haramu ili kukabiliana na madhara yatokanayo na biashara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu yafuatayo yamezingatiwa katika Muswada huu:-

(i) Sheria itatumika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

(ii) Kuweka tafsiri ya biashara ya fedha haramu pamoja na kuainisha makosa yatakayohusishwa na biashara ya fedha haramu.

(iii) Kuweka tafsiri ya asasi za kifedha na zinginezo *(reporting persons)* ambazo zitapaswa kuwasilisha kwa *FIU* kwa uchambuzi taarifa za kifedha zenye mwelekeo wa mashaka *(suspicious transactions reports)* wa biashara ya fedha haramu.

(iv) Kuanzisha chombo cha kiserikali cha uchunguzi *(Financial Intelligence Unit)* kitakachopokea taarifa mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi zenye mwelekeo wa mashaka *(suspicious transaction reports)* kuhusiana na fedha haramu, kuzichambua na kuziwasilisha katika vyombo husika kwa hatua zaidi. Aidha, chombo hiki kitakuwa kinajitegemea chini ya Wizara ya Fedha.

(v) Kuweka Kamati ya Wataalam ya Ushauri ya Kitaifa ya Udhibiti wa biashara ya fedha haramu.

(vi) Kuharamisha mapato na mali yote itokanayo na vitendo vya kihalifu vinavyohusika na biashara ya fedha haramu na kubainisha adhabu zake.

(vii) Kuweka taratibu tambuzi za wateja *(know your customer principle)* kwa benki na asasi nyingine za kibiashara ili kubaini wateja wanaojihusisha na biashara ya fedha haramu pamoja na kuwajibisha benki na asasi hizo ziweke kumbukumbu na taratibu za ndani za udhibiti wa fedha haramu.

(viii) Kuweka taratibu za kuwalinda watakaotoa taarifa kuhusu vitendo vya uhalifu na biashara ya fedha haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu sita:

Sehemu ya Kwanza, yenye ibara ya 1 hadi 3 inahusu masuala ya utangulizi ikiwemo jina la Sheria, tafsiri za maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada na matumizi ya Sheria ambapo Sheria hii itatumika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika sehemu hii pia imetolewa tafsiri ya *money laundering* na pia makosa yote ya kihalifu yatakayohusishwa na makosa ya *money laundering*. Aidha, Waziri wa Fedha amepewa mamlaka ya kuongeza orodha ya makosa hayo kwa kutumia kanuni atakapoona inafaa kufanya hivyo.

Sehemu ya Pili, inajumuisha ibara ya 4 hadi ibara ya 11 zinazohusu kuanzisha chombo cha kiserikali cha uchunguzi *(Financial Intelligence Unit - (FIU)*. Chombo hiki kitakuwa kinajitegemea chini ya Wizara ya Fedha, kitapokea taarifa mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi zenye mwelekeo wa mashaka kuhusiana na fedha haramu, kuzichambua na kuziwasilisha katika vyombo husika kwa hatua zaidi, uteuzi wa Mtendaji Mkuu, Wafanyakazi, majukumu ya *FIU* na masharti ya kuwataka wafanyakazi wa *FIU* kutoa tamko la mali zao *(Financial disclosure)* mara kwa mara pia yameainishwa katika sehemu hii. Aidha kuweka Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Watalaam wa masuala ya Udhibiti wa Fedha Haramu, majukumu yake, uteuzi wa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu na Wajumbe wa Kamati ni baadhi ya mambo yaliyoainishwa katika Sehemu hii.

Vilevile katika jedwali la marekebisho ambalo naamini Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mmelipata yamefanyika marekebisho ili kuwezesha wafanyakazi wa *FIU* walioonyesha utendaji mzuri kuweza kuteuliwa kwa kipindi kingine cha miaka mitano, na pia yamefanyika marekebisho katika wajumbe wa Kamati ya Kitaifa kwa kuongeza mjumbe mmoja kutoka Ofisi ya Usalama wa Raia Zanzibar.

Sehemu ya Tatu, Mheshimiwa Naibu Spika, yenye ibara za 12 hadi 14, inaainisha tafsiri ya vitendo vya kihalifu ambavyo mapato au mali zitokanazo na vitendo hivyo vitahusishwa na fedha haramu na kubainisha adhabu zake. Aidha, kwa kuzingatia athari ya vitendo vya kihalifu vinavyozalisha fedha haramu na mapato makubwa yatokanayo na uhalifu huo, kama Waheshimiwa Wabunge mlivyoshuhudia katika Semina ya Jumamosi, Sheria katika Jedwali la Marekebisho Kifungu cha 13 kimefanyiwa marekebisho ili kuweka adhabu kali kwa mtu au taasisi yoyote itakayotiwa hatiani chini ya Sheria hii ili kukomesha vitendo hivi vya kihalifu. Chini ya marekebisho haya mtu atakayepatikana na hatia adhabu itakayotolewa ni faini ya kiasi kisichozidi shilingi milioni mia tano na kisichopungua shilingi milioni mia moja au kifungo kisichozidi miaka kumi na kisichopungua miaka mitano badala ya faini ya kiasi kisichozidi shilingi milioni mia tatu na kisichopungua shilingi milioni hamsini au kifungo kisichozidi miaka saba na kisichopungua miaka mitatu. Kwa taasisi, adhabu itakuwa ni faini ya kiasi kisichozidi shilingi bilioni moja na kisichopungua shilingi milioni mia tano badala ya faini ya kiasi kisichozidi shilingi milioni mia sita na kisichopungua shilingi milioni mia mbili.

Sehemu ya Nne, ya Muswada inahusu ibara ya 15 mpaka 23 zinazobainisha taratibu mbalimbali za Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu ikiwa ni pamoja na utaratibu wa Asasi za kifedha na nyinginezo kuwasilisha taarifa zenye mwelekeo wa mashaka wa biashara ya fedha haramu kwa chombo cha *FIU*. Sehemu hii pia inatoa

masharti kwa Asasi za kifedha na nyingine za kibiashara kuweka taratibu tambuzi za wateja ili kubaini wateja wanaojihusisha na biashara ya fedha haramu pamoja na kuwajibisha benki na Asasi hizo kuweka kumbukumbu na taratibu za ndani za udhibiti wa biashara ya Fedha Haramu.

Kwa kuzingatia kwamba baadhi ya vitendo vya kihalifu vinavyohusisha fedha haramu vinafanywa na vikundi vya wahalifu wenye mtandao *(organized crimes)* au watu wenye uwezo mkubwa wa kifedha wa kuweza kuhatarisha maisha ya watoa taarifa, sheria imeweka masharti ya kuwalinda watakaotoa taarifa za mashaka kuhusu vitendo vya uhalifu na biashara ya fedha haramu ikiwa ni pamoja na mashahidi kutoa ushahidi kwa njia ya vifaa vya elektroniki.

Aidha masharti ya uchunguzi yahusuyo wateja wa kibiashara kutoka nje ya nchi wenye kinga ya kisiasa *(politically exposed persons)* yamebainishwa, ambapo asasi zitakazofanya mahusiano ya kibiashara na kundi hili zinapaswa kujihakikishia zinapata utambulisho wa ziada *(enhanced due diligence)* wa wateja wao na kwamba kinga waliyokuwa nayo isitumike kama kificho cha kuendesha biashara ya fedha haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia athari za vitendo vya uhalifu vinavyohusiana na usafishaji wa fedha haramu, Sheria imeweka sharti kwamba masharti yote yahusuyo siri baina ya taasisi/au mtu na mteja wake hayatatumika chini ya Sheria hii, ambapo taasisi ambayo ni *reporting person* itapaswa kutoa taarifa za mashaka kwa *FIU* bila kujali matakwa ya usiri *(secrecy)*. Madhumuni ya sharti hili ni kuhakikisha kwamba wahalifu wa makosa ya usafishaji wa fedha haramu hawatumii washauri wao kwa mfano wanasheria na wahasibu kama vyombo vya kufanya uhalifu kwa kuwa jamii imejenga imani kwa taaluma kama za wanasheria kwamba huzingatia sheria siku zote. Hivyo taasisi hizi zinapaswa kufahamu utambulisho wa wateja wao na endapo wanajihusisha na vitendo vya mashaka ya uhalifu watoe taarifa kwa *FIU*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 20 kimefanyiwa marekebisho chini ya Jedwali la Marekebisho kwa kuongeza adhabu ya faini kwa mtu na taasisi kutoka faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miaka mitatu kwa mtu na badala yake kuwa kiasi kisichozidi shilingi milioni mia tano na kisichopungua shilingi milioni mia moja au kifungo kisichozidi miaka kumi na kisichopungua miaka mitano, na kwa taasisi kutoka faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni tano na badala yake kuwa faini ya kiasi kisichozidi shilingi bilioni moja na kisichopungua shilingi milioni mia tano, kwa kosa la kutoa taarifa kwa mhusika wa biashara ya fedha haramu au kwa mtu yeyote asiyepaswa kufahamu kwamba kuna taarifa kuhusu biashara ya fedha haramu iliyowasilishwa kwa *FIU* kuhusu mtu/taasisi fulani kwa ajili ya uchunguzi.

Sehemu ya tano ya Muswada inahusu ibara ya 24 mpaka Ibara ya 26 zinazoelezea masuala ya kifedha hususan bajeti, mwaka wa fedha wa *FIU* masharti ya kutunza mahesabu na ukaguzi wa mahesabu wa *FIU* ambao utafanywa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Sehemu ya Sita na ya mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, inahusu ibara ya 27 mpaka ibara ya 29 zinazobainisha masuala ya kijumla hususan kinga kwa wafanyakazi wa *FIU*, wajumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Wataalam ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu wakati wa kutekeleza majukumu yao. Vile vile taratibu za uchunguzi, upelelezi, ukusanyaji wa ushahidi, uendeshaji wa mashauri yahusuyo biashara ya fedha haramu ikiwa ni pamoja na utaifishaji wa mali zitokanazo na makosa haya pia zimeainishwa. Aidha mamlaka ya Waziri wa Fedha ya kuandaa taratibu na kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria hii pia yamewekwa bayana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ADAM K. A. MALIMA (k.n.y. MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA FEDHA NA UCHUMI):**Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu 70(2) Toleo la Mwaka 2004, baada ya kukamilisha kazi ya kuchambua na kujadili Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu *(The Anti-Money Laundering Act, 2006)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kabla ya kuwasilisha maoni ya Kamati, ninaomba nitumie fursa hii kulifahamisha Bunge lako kwamba Kamati imetumia muda mwingi kulielewa tatizo hili kwa kina na hivyo kuridhia kwamba suala zima la fedha chafu inayotokana na mapato ya biashara haramu (*proceeds from illegal activities*) ni tatizo kubwa sana sasa hivi katika jamii ya dunia yetu hii, na kuanzia huko nje ilikoanzia biashara hii miaka ya nyuma ya themanini sasa matumizi ya pesa hizi zinaelekezwa katika nchi maskini kama zetu na madhara yake kwa jamii, mmomonyoko wa maadili lakini pia katika kuathiri nguvu kazi na uzalishaji wa kiuchumi, ni tatizo kubwa na ambalo linazidi kukuwa siku hadi siku.

Aidha Kamati inatambua kwamba Tanzania inaishi katika mfumo wa jamii ya kimataifa na tunalazimika kutambua kwamba majanga yanayotokana na kukuwa kwa biashara haramu za madawa ya kulevya, uuzaji haramu wa silaha, matumizi ya fedha hizi katika kufanikisha ugaidi, biashara haramu ya viungo vya wanadamu, ujambazi wa kimataifa *(Organized Crimes)*, umalaya wa kimataifa na utumwa wa watoto katika biashara hiyo unahitaji kukemewa kwa kauli na vitendo na watu wa jamii zote kwani kinachomuathiri mwenzako leo, kesho kitagonga mlangoni mwako. *(Makofi)*

Hivyo Kamati yangu imekubaliana na Serikali kwamba huu ni wakati muafaka wa kuungana na jamii ya Kimataifa na kushirikiana nayo kwa nguvu zote kukabiliana na namna zote za uhalifu wa namna hii na matumizi au uhalilishaji wa mapato yanayopatikana kwa njia hizi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, naomba kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Kamati imepitia na kuchambua Muswada huu na inaunga mkono mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu *(The Anti-Money Laundering Act, 2006.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unalenga kuharamisha mapato ya fedha na mali itokanayo na biashara na vitendo vya kihalifu na kubainisha adhabu zake. Madhumuni yake ni kupendekeza sheria madhubuti inayozingatia viwango vya Kimataifa vya udhibiti wa uhamishaji na matumizi ya baadae ya fedha hiyo itokananyo na biashara haramu na kupendekeza adhabu stahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unazingatia mambo muhimu yafuatayo:-

§ Kuweka tafsiri ya vitendo vya uhalifu ambapo mapato au mali zitokananzo na vitendo hivyo zitahusishwa na fedha zitokanazo na biashara haramu.

§ Kuweka tafsiri za asasi za kifedha na zinginezo *(reporting entities)* ambazo zitapewa jukumu la kuwasilisha taarifa za kifedha zenye mwelekeo wa mashaka *(reports of suspicious transactions)* wa fedha zitokanazo na biashara haramu kwa chombo cha Kiserikali cha kuchunguza taarifa za kihalifu.

§ Kuanzisha chombo cha Kiserikali cha uchunguzi kitakachoitwa *The Financial Intelligence Unit,* kitakachokuwa chini ya Wizara ya Fedha. Chombo hiki kitakuwa na mamlaka ya kupokea taarifa mbalimbali kutoka nje na ndani ya nchi zenye mwelekeo wa mashaka.

§ Kuanzisha Kamati ya Kitaifa ya Wataalam ya Ushauri wa Udhibiti wa fedha zitokanazo na Biashara haramu.

§ Kuharamisha mapato na mali yote itokanayo na vitendo vya kihalifu na kubainisha adhabu zake.

§ Kuweka taratibu tambuzi za wateja *(know your customer principle)* kwa benki na asasi nyingine za kibiashara. Lengo la taratibu hizi ni kubaini wateja wanaojihusisha na fedha zitokanazo na biashara haramu.

§ Kuweka adhabu kwa watu au asasi zitakazohusika na uhalifu wa fedha zitokanazo na biashara haramu.

§ Kuweka adhabu kwa watu au asasi zitakazoshindwa kutoa taarifa za uhalifu wa fedha zitokanazo na biashara haramu unaofanyika au unaotaka kufanyika kwa kipindi kisichozidi masaa 24 baada ya kutia shaka ya uwezekano wa uhalifu huo kutokea.

- § Kuweka adhabu kwa mtu au taasisi yoyote ambayo imebainika kumtaarifu mhalifu *(tipping off)* ili aweze kukimbia au kuharibu ushahidi.

- § Kuweka taratibu za kuwalinda watoa taarifa kuhusu vitendo vya uhalifu na fedha itokanayo na biashara haramu.

- § Kuoainisha Muswada huu na sheria zingine husika ili kupata ufanisi uliokamilka katika utekelezaji wa kisheria wa malengo yanayokusudiwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao cha pamoja Waziri wa Fedha, Manaibu Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na timu yao kilichofanyika tarehe *27 October, 2006* na 8 Novemba, 2006 Kamati ilipitia vifungu vya Muswada wote, ambapo baada ya majadiliano Kamati ilipitisha Muswada huo pamoja na Mapendekezo mbalimbali yaliyolenga kuboresha Muswada huo ambayo kimsingi Mheshimiwa Waziri aliyakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo pamoja na Kamati yangu kuafiki Muswada huu wa Serikali, Kamati ina maoni ya jumla na ya kuboresha baadhi ya mafungu ya Muswada huu. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu 70(2) Toleo la Mwaka 2004, sasa naomba niwasilishe Maoni ya Kamati yangu kuhusu Muswada uliyotajwa hapo juu kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha (4) cha fungu la 17 kinachopendekeza adhabu ya faini isiyozidi Shilingi milioni tano au kufungwa jela miaka isiyozidi mitano kwa mtu na Shilingi milioni kumi au mara tatu ya thamani ya kitu ambacho kilihusishwa na uhalifu huo kwa taasisi itakayoshindwa kutoa taarifa za uhalifu wa fedha zitokanazo na biashara haramu unaofanyika au unaotaka kufanyika kwa kipindi kisichozidi masaa 24 baada ya kutia shaka ya uwezekano wa uhalifu huo kutokea. Kamati inashauri kuwa Serikali iangalie upya kipengele hiki kwani mazingira kwa maeneo yetu mbalimbali hayafanani.

Kuna baadhi ya sehemu mawasiliano ni rahisi na mengine ni magumu. Ikitokea mtu au taasisi haikutoa taarifa katika muda unaotakiwa kutokana na ugumu wa mawasiliano au mpokea taarifa kutokupatikana basi vyombo husika vitambue hivyo na mtu huyo au taasisi hiyo isiadhibiwe. Mtu au taasisi yoyote iadhibiwe kama haikuweza kutoa taarifa hali ikijua uhalifu unatokea au utatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri pia Serikali itoe motisha (zawadi) kwa mtu au taasisi itakayotoa taarifa na jamii itangaziwe kuwa kuna motisha kwa atakaewezesha kuzuia uhalifu wa namna hii au kukamatwa kwa wahalifu wanaojihusisha na vitendo vya fedha chafu itokanayo na mapato ya biashara haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, fungu la 22 linapendekeza kuwalinda watakaotoa taarifa za mashaka kuhusu vitendo vya uhalifu. Kamati imepitia kwa kina na kubaini kwamba fungu hili linalinda taasisi *reporting person* na siyo mtu (*individually)* mtu

binafsi, atakayetoa taarifa za mashaka kuhusu vitendo vya uhalifu ambao baadae ndiyo watakuwa mashahidi kwenye kesi. Na imeonekana kwamba hakuna sheria ya kuwalinda watoa taarifa hizo. Kuna hatari watoa taarifa hizo wakadhurika na watuhumiwa wa uhalifu huo. Aidha, wanaweza kuwa wanazo taarifa za mashaka za uhalifu lakini wakaogopa kuzitoa kwenye vyombo husika kwa kuwa hakuna sheria inayowalinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa Serikali, iangalie uwezekano wa kutunga sheria inayojitegemea kuhusu kuwalinda watoa taarifa za mashaka kuhusu vitendo vya uhalifu, mashahidi wa kesi hizi na pia kuwapatia ulinzi zaidi maafisa wanaofanya kazi katika vitengo hivi. (*i.e. whistleblowers, witnesses and related officials)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuhalalisha fedha *(Money Laundering)* ni suala gumu sana ambalo ni tishio kwa uchumi na usalama wa nchi duniani. Kwani washiriki wa mchezo huu mchafu ni watu hatari sana na fedha zinazohusishwa na uhalifu huu ni mabilioni ya fedha, za kigeni na sasa hata za shilingi pale ambapo biashara hizi zinawahusu raia wa Tanzania.

Watu hawa katika kutimiza malengo yao wanaweza kuhujumu hata Serikali, zilizopo madarakani na vyombo vya dola na haswa usalama wa raia kama ambavyo imeshuhudiwa katika nchi zingine. Kwa kuwa watu hawa wana uwezo mkubwa kifedha zitokanazo na biashara hizi zisizo halali hubuni mbinu nyingi za kisasa za kukwepa mkono wa dola na mara nyingi huhusishwa na ukwepaji mkubwa wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kuwa Muswada huu unapendekeza mikakati mbalimbali ya kisheria ya kukabiliana na tatizo hili, hivyo basi ni maoni pia ya Kamati kwamba maandalizi na mikakati madhubuti inahitajika ili sheria hii iweze kutekelezeka.

Aidha, utekelezaji wa Sheria hii unategemea ushirikiano wa vyombo mbalimbali vya dola kama vile Polisi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mahakama, Mamlaka ya Mapato, Benki Kuu, Magereza, Usalama wa Taifa, TAKURU, Wizara ya Fedha na kadhalika. Kama inavyoanishwa kwenye Muswada huu. Hivyo Kamati inashauri yaandaliwe mazingira ya ushirikiano wa hali ya juu kabisa ya kiutendaji baina ya vyombo hivi kama walivyoainishwa hapa juu ili kufanikisha azma na makusudio ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye maandalizi makubwa hususan ya kiutendaji ikijumuisha kujenga na kuimarisha miundombinu ya upashanaji habari, kuwasomesha watekelezaji wa sheria hii, ili kuwa na mbinu za kisasa za kukabiliana na tatizo hili, kuielimisha jamii kuhusu ubaya wa tatizo hili na kuomba ushirikiano katika mapambano haya. Aidha, Serikali iweke utaratibu ambao utawapa motisha wale ambao wamejitolea kutoa taarifa. Pia Serikali iboreshe mazingira ya utendaji kazi kwa vyombo vitakavyohusika na utekelezaji wa sheria hii ikiwa ni pamoja na kutenga Bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Sheria hii, utakuwa mgumu sana hususan katika jamii. Wahalifu hao hao wanaweza kujaribu kusafisha pesa hizi kwa

kuzitumbukiza katika uwekezaji wa shughuli za kiuchumi ambazo zinaweza zikawa na maslahi ya moja kwa moja katika maisha ya wana jamii na hivyo ubaya wa uwekezaji huo usipokelewe ipasavyo na watu ambao wangenufaika na uwekezaji huo.

Kuna uwezekano pia kwamba sheria hii, ikatumika vibaya kwa sababu binafsi iwapo Serikali haitakuwa makini. Wasimamizi na hata watu wa kawaida waweza kutumia sheria hii kama kukomoana na kulipa visasi. Kuna uwezekano mtu akawa hampendi mtu mwingine kwasababu ama wana ugomvi au anachuki nae kutumia sheria hii kwa kutoa taarifa kwa vyombo vya usimamizi kuwa mtu fulani anajihusisha kwenye uhalifu wa kuhalalisha fedha chafu.

Hali hii isipopatiwa udhibiti makini wa kisheria yaweza kuleta madhara makubwa sana katika mahusiano na maisha ya watu. Kamati inashauri kuwa serikali iandae utaratibu mzuri utakaowezesha kutambua kuwa taarifa zilizotolewa ni za kweli au ni za kukomoana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kukamilisha kuwasilisha maoni haya ya Kamati yangu kuhusu Muswada huu, ninaomba nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, kwa michango yao makini iliyokuwa na uchambuzi wa kujenga (*constructive criticism*) ambayo kwa kiwango kikubwa imesaidia sana kuboresha Miswada huu. Naomba kuwatambulisha Wajumbe hao wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda Mbunge - Mwenyekiti, Mheshimiwa Adam K. Malima - Makamu Mwenyekiti wakati Wajumbe ni Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Parmoukh S. Hoogan, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Ledioana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Omar S. Mussa, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman Saddiq, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Mzee Zubeir, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mheshimiwa Hamad R. Mohamed. Naomba pia nitambue mchango wa Ndugu Anselm Mrema, Katibu na Ndugu Emmanuel Mpanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji, Mbunge, Manaibu wake Mheshimiwa Abdisalaam I. Khatibu, Mbunge, na Mheshimiwa Mustafa Mkulo, (Mbunge) Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Johnson Mwanyika, (Mbunge), Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Ndugu Grey Mgonja, pamoja na timu ya wataalamu mbali mbali kutoka idara husika kwa kushirikiana na Kamati na kuisaidia kufanikisha kujadili na kupitisha Muswada huu. Napenda kukuhakishieni kwamba sisi kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, tumefarijika sana na ushirikiano huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tena kuipongeza Serikali yetu kwa kuleta hapa mbele yetu Muswada huu muhimu kwa jamii ya Watanzania na uchumi wa nchi hii na kwa wakati muafaka kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI – WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kupata nafasi hii kuwasilisha maoni Muswada wa Sheria tajwa hapo Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu 43(5) (c) na 70(2) toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kuangalia maudhui ya Muswada wenyewe ni mazuri lakini swali la msingi la kujiuliza ni kama tuna nia ya dhati na utashi wa kisiasa *(Political Will)* wa kuhakikisha kwamba sheria husika inafanya kazi na sio kama sheria nyingine ambazo tunazipitisha kutokana na kutakiwa na Jumuiya za Kimataifa, kufanya hivyo kisha kuziacha zikiozea makabatini pasipo wananchi au vyombo vinavyohusika na ufanikishwaji wa utekelezaji wa sheria husika kuwekewa mazingira bora ya kuziwezesha kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyazungumza haya kwa kufahamu kwamba sheria hii ni chimbuko la Mkataba, dhidi ya uhalifu wa kimataifa uliopitishwa na Umoja wa Mataifa yaani *The United Nations Conventions against Transitional Organised crime and the Protocol Thereto* wa mwaka 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni bora ikafahamika kwamba kama ambavyo muswada huu ni muhimu sana kwa kuboresha mfumo wa uchumi wa nchi yetu ndivyo pia ni mmoja kati ya Miswada ambayo itakuwa migumu sana kuitekelezeka hasa kutokana ustadi wa hali ya juu unaotumiwa na wahalifu wa fedha haramu na ugumu unazidi pale ambapo muswada unaainisha mazingira mbalimbali ambayo yanaashiria fedha haramu rejea kifungu cha tatu cha Muswada kinachoelezea maana ya *Predicate Offence.* Ukiyaangalia kwa umakini mazingira husika yanatugusa baadhi yetu kama sio wote katika maisha yetu ya kila siku. Ndio maana narudia kwa kusema kwamba kwa Muswada huu kutekelezeka kunahitaji nia ya dhati na utashi wa kisiasa kuutekeleza

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia katika Muswada wenyewe kama unavyoeleza kuhusu udhibiti wa fedha haramu, fedha haramu zinakwenda sambamba na matukio ya rushwa Ni wazi kabisa licha ya vyombo mbalimbali kuundwa na sheria mbali mbali kali kutungwa tatizo la rushwa linazidi kuota mizizi .

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha haramu kwa njia nyingine ambayo imekuwa ikitumiwa na baadhi ya makampuni makubwa ya kigeni katika kupata kandarasi mbali mbali ndani ya nchi ni jambo ambalo lipo wazi na hata Mtanzania wa kawaida analiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimedokeza hapo awali kuwa fedha haramu na rushwa ni vitu mapacha ambavyo kwa njia yeyote haviwezi kutenganishwa.

Hivyo basi ni bora sheria hii ikaeleza wazi pale bei ya kuuzia au kununulia bidhaa inapokuwa hailingani na thamani halisi ya bidhaa yenyewe. Ifahamike kwamba waathirika wa ongezeko la bei hiyo ni walalahoi na nchi wachache ndio wanaonufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha sheria imekaa kimya pale inapoonyesha wazi kuwa mali anazomiliki mtu hazina uwiano wowote na kipato halisi cha mhusika. Kambi ya Upinzani, inaona huu ni muda muafaka kwa washukiwa ambao wanafanya biashara ambayo inaingiza fedha haramu ambapo hakuna- *justifacation* ya faida kutoka katika biashara zao na baadaye fedha hizo zinawekezwa katika biashara halali, watu hao watoe uhakikisho wa fedha hizo vinginevyo sheria hii itakuwa ina wanasa dagaa na kuwaacha mapapa yakiogelea huru katika mwambao wa bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni pale mfanyabiashara anapochangia katika harambee za kisiasa mamilioni ya shillingi kwa mkupuo . Kwa biashara halali na ambayo inalipa kodi ni jambo lisilokuwa la kawaida na linalosababisha walakini katika uhalali wa shughuli za biashara zake. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali itoe maelezo katika hali kama hiyo niliyoieleza, wahusika wanasimamia wapi katika sheria hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa mbalimbali za Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) zinaonyesha kuwa fedha haramu na rushwa vimesababisha kupanda kwa gharama za manunuzi ya Serikali *(Government Procurements)* kitu kinachosababisha kushuka kwa uwezo wa Serikali katika kutoa huduma muhimu kwa wananchi wake na kushindwa kujenga miundombinu mbalimbali kwa maendeleo.

Aidha pale fedha haramu zinapoingizwa katika medani za siasa kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia, ununuaji wa kura au shahada za kupigia kura umekuwa ukiongeza gharama za chaguzi. Mathalan pale mgombea anapotumia takriban dola za Kimarekani milioni 400 katika kampeni kwa nafasi ya uwakilishi katika vyombo vya kutunga sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha fedha hizo mara nyingi huwa ni haramu na pindi mgombea akishakuwa kiongozi ni dhahiri hawezi kupigana na fedha haramu au rushwa katika kuiongoza nchi katika nafasi ya utunzi na usimamizi wa sheria dhidi ya vitendo hivyo haramu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, kwa kuona matatizo ya rushwa katika kandarasi za manunuzi ya Serikali, mara kwa mara tumekuwa tukiitaka Serikali iachane na mtindo wake wa sasa na ianzishe mtindo wa *electronic procurement* au *e-procurement* ambapo kwa juhudi zetu tulifikia hatua ya kupata wafadhili wa kuwafundisha maafisa waandamizi kutoka Wizara ya Fedha jinsi ya kutoa kandarasi kwa njia hii ya *e-procurement.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, tunaamini kabisa fedha haramu na rushwa vitapungua ama kumalizika kabisa pale tutakapobadili mazoea tuliyonayo katika

utendaji wetu wa kazi na kuweka mbele maslahi ya Watanzania badala ya maslahi ya mtu mmoja mmoja au kundi fulani katika jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 4(1) cha muswada huu kinaanzisha wa chombo cha uchunguzi wa mambo ya fedha yaani *Financial Intelligence Unit (FIU)* ambacho kwa mujibu wa Muswada huu chombo hicho kitakuwa chini ya Wizara ya Fedha kama idara.

Kambi ya Upinzani inaona kwamba chombo hiki kinaweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kama kikiwa chombo huru na chenye bajeti yake na badala ya kuwa chini ya Wizara ya Fedha kingekuwa chini ya Wizara ya Usalama wa Raia kwani kwa mtazamo wetu shughuli za kiuchunguzi zinaweza kufanywa vizuri na kiuhakika na chombo chenye mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoweza kufanyika ni kuwahusisha watu wenye utaalam wa mambo ya fedha au kuwa na mahusiano ya karibu na Wizara ya Fedha na sio kitengo husika kuwa kama sehemu ya Wizara ya Fedha kama idara.

Mheshimiwa Naibu Spika Kambi pia inashauri juu ya umuhimu wa Serikali kuwa na utaratibu maalum ambao utakiwezesha chombo hiki kuwa na uhusiano wa kazi na vyombo vingine vinavyofanya kazi zinazoendana na chombo hiki. Mfano *PCB* na vyombo vingine vya aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 5 kinazungumzia uteuzi wa Kamishna. Kambi inakubaliana na uteuzi wa Kamishna husika kufanywa na Rais, ila kwa kuzingatia unyeti wa kazi husika na ili kuwezesha utekelezaji wa sheria Kambi ya Upinzani, inashauri Kamishna awe na kinga ya ajira *(Security of Tenure*) kama ilivyo kwa Majaji kama ilivyoainishwa na ibara ya 120A ya Katiba ya Jamuhuri ya Mungano wa Tanzania, toleo la 2005. Mbali na kutokuwa na hofu ya kufukuzwa kazi kutokana na maamuzi au hatua atakazokuwa anazichukua, hali hii itasaidia vile vile ufanisi katika utekelezaji wa sheria husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ibara 6 (a) kipengele kinachohusu kupokelewa na kuzifanyia kazi taarifa zenye mashaka katika muhamala wa kifedha *(Financial Transactions)* zinazowasilishwa na watoa taarifa. Kambi ya Upinzani, inashauri hapa kuwepo na uangalifu wa hali ya juu kwani ni rahisi kwa watu kuwasilisha taarifa za chuki binafsi na fitina. Kitu ambacho kitapelekea Serikali kufikishwa Mahakamani na fidia kulipwa.

Aidha, katika muswada hatujaona kipengele cha kuheshimu haki ya usiri wa taarifa za mtu *( Right of Privacy)* kitu ambacho ni haki ya Kikatiba kwa kila Mtanzania. Ni haki ya usiri kwa taarifa za mteja ni muhimu na lazima kipengele hicho kiwepo ndani kwani huo ndio msingi mkuu wa biashara ya kibenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia inashauri sheria kuvitaja wazi vyombo vitakavyokuwa na jukumu la kutekeleza sheria hii ili kuepusha kurushiana

mipira. Ni muhimu kwenye *definition section* ikaelezwa wazi *Law Enforcement Agencies* ni zipi na majukumu yake ni yapi na katika mazingira gani.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7 kinaeleza waajiriwa wa *Financial Intelligence Unit*. Kambi inapenda kufahamishwa tumejiandaaje kabla sheria haijaanza kufanya kazi, kwa kuwatambua na kuwapa mafunzo watu watakaokuwa waajiriwa wa kitengo husika .

Vile vile tungependa Serikali ituambie ni vigezo gani vilivyotumika hadi kuweka kwenye sheria kipindi cha ajira kuwa cha miaka mitano tu? Kwa kuzingatia kwamba ufanisi wa kazi husika unahitaji mafunzo ya mara kwa mara na mbinu mbali mbali.

Je, Serikali haioni kwamba kwa sharti hili mbali na kutopata watu makini kwa hofu ya kumalizika kwa ajira baada ya muda mfupi, utaigharimu sana Serikali kwani itakuwa ina jukumu la kusomesha watu wapya mara kwa mara? Kambi ya Upinzani, inashauri ajira iwe kwa mkataba na kwamba kuendelea ama kutokuendelea kwa mkataba wa mtu kutegemeane na ufanisi wake katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu 7 (4) kinaeleza jukumu la waajiriwa wa *FIU* kutangaza mali zao katika vipindi mbalimbali. Ni muhimu kutathmini kwanza mafunzo tuliyoyapata kwa sheria iliyowataka viongozi kutaja mali zao, ni mchakato gani utakaotumika kuthibitisha kwamba kinachotajwa ni halisi na hasa kwa kuzingatia kwamba ili kukwepa kukamatwa kumekuwa na mtindo ulioshamiri ambapo wahalifu hufanya kuhamishia mali zao zilizopatikana kwa njia zisizo halali kwa watoto au ndugu na jamaa wa karibu. Mifano ni mingi tu watoto wadogo au wanafunzi kumiliki akaunti za benki zenye mamilioni ya fedha ndani na nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 17 kinaelezea majukumu ya mtoa taarifa haramu *(Reporting person).* Kambi ya Upinzani, pamoja na kukubaliana na dhana nzima ya majukumu ya mtoa taarifa inapata wasiwasi juu ya kipengele cha 17(4) ambacho kinatoa adhabu kwa mtoa taarifa ambaye atashindwa kutoa taarifa ndani ya masaa 24 kama sheria inavyompasa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu wakati tunatunga sheria tuangalie aina ya miundo mbinu ambayo nchi yetu inayo kiasi cha kuwezesha taarifa kuweza kusambazwa katika kipindi kifupi kiasi hicho. Tunatoa angalizo hili ili kuepusha watoa taarifa *(Reporting Persons*) kujikuta wakiishia kwenda jela kutokana na kujikuta wanashindwa kukidhi matakwa ya kifungu 17(1) . (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 27, inayohusu kinga kwa Kamishna, wanachama wa Kamati ya Taifa ya *FIU* na wafanyakazi kuhusiana na kosa lolote/tendo lolote watakalolifanya kwa nia njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inataka kuwepo na angalizo la kifungu hiki kwani sheria inatakiwa kulinda haki za raia na haitakiwi kutoa mwanya kwa mtu yeyote au kundi fulani kuingilia au kudhalilisha haki hiyo kwa kisingizio kuwa haki hiyo ya Kikatiba ibara ya 16 imevunjwa wakati akifanyakazi yake kwa nia njema.

Tunashauri kuweka angalizo hilo kwa ukweli kuwa, kuna matukio ambayo yalitokea katika zoezi la kupambana na ujambazi hapa nchini ambapo baadhi ya watu walituhumiwa kuwa ni majambazi na kuvunjiwa heshima katika jamii japokuwa watoa tuhuma hawakuwa na ushahidi dhidi ya tuhuma hizo. Jambo ambalo linaweza sababisha Serikali kupoteza kiasi kikubwa cha fedha za walipa kodi kama fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia hayo naomba niwasilishe hoja kwa niaba ya Kambi ya Upinzania. (*Makofi*)

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kuniruhusu kuwa mtu wa kwanza kuchangia kwenye Muswada huu muhimu. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa maelezo ya kina ambayo ametufanya wengi sasa tupate picha kamilifu zaidi ya Muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utandawazi, uhuria wa uchumi tulionao na vile vile mapinduzi ya mawasiliano, nchi yetu imeiingizwa kwenye uchumi wa dunia kwa kasi sana pamoja na mizengwe yake yote ikiwemo biashara ya fedha haramu. Juzi tulikuwa na semina na kwenye semina hiyo, nilisema kuna fedha haramu na fedha haramu.

Kuna fedha haramu upande mmoja, inayotokana na vitendo haramu vinavyofanyika nje ya nchi yetu. Kwa mfano biashara haramu ya ngono, biashara haramu ya silaha, biashara haramu ya madawa ya kulevya. Na fedha inayotokana na vitendo hivyo haramu inapelekwa nchi zingine ili iingizwe kwenye mikondo ya kawaida ya fedha ili kuweza kupoteza uasilia wa hiyo fedha kwamba ni haramu.

Kwa hiyo, tunatakiwa na Mikataba ya Kimataifa kwamba tubaini uasilia wa hiyo fedha lakini vile vile tudhibiti uingizwaji wa hiyo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakiri kabisa kwamba Muswada huu azma yake hiyo na inakamilishwa hapa na sisi kama sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa ambayo tumedhamiria kabisa kupiga vita biashara hii hatuna budi kuupitisha Muswada huu. Lakini nilitaka tu kutoa angalizo kwa watendaji wetu katika kutekeleza Sheria hii ambayo tutaipitisha leo, nina uhakika tutaipitisha leo, wawe waangalifu waweka mbele uzalendo na maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiingia kutekeleza hii Sheria kichwa kichwa, Sheria hii itakuwa kwa faida ya Wazungu tu na huku sisi tunaachwa hoi na mambo yetu yakiharibika. Utekelezaji mbovu utakuwa na madhara mimi naona manne. Mengine yamegusiwa na wasemaji waliotangulia hasa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha. Kwanza inaweza ikawakatisha tamaa wawekezaji wenye nia nzuri ya kuwekeza fedha zao hapa Tanzania. Kwa sababu mtu anakuja anataka kuwekeza wewe kazi yako kusema hii hela uliipata wapi? Sasa mimi mwekezaji lazima niwe na fedha. Kwa hiyo, tuwe na utaalam

mzuri wa kuweza kuangalia unamhoji nani. Sawa, mtu ana kibanda cha *chips* kesho anajenga ghorofa hao ndiyo watu wa kuweza ku-*suspect. (Makofi)*

Pili, inaweza hii Sheria ikatumika kuvikaba koo vyombo vyetu vya uwekezaji na vyombo vyetu vya biashara. Kwa mfano, *TIC* imepunguza urasimu kweli kweli. Leo tukiitekeleza vibaya sheria hii tutailundikia makaratasi chungu mbovu kuanza kuwahoji watu wamepata wapi hiyo hela. Mbona umebeba *briefcase* nzuri, hapana. Tuwe waangalifu, uzalendo mbele na vile vile maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Tatu, limeelezwa na wenzangu hapa kwamba kwa kweli isije ikatumika kuwakomoa wenzetu bila sababu na mwisho kabisa hata kuwavunja moyo Watanzania wenye ari ya kutajirika kwa njia halali kabisa. Kwa sababu kutajirika siyo kwa mzungu tu, hata sisi tunaweza kutajirika, siyo bwana. Kwa hiyo, nilikuwa nasema tu kwamba lazima tuwe waangalifu katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa pili kuna fedha haramu inayotokana na vitendo haramu humu humu ndani ya nchi yetu. Rushwa, ukwepaji kodi, mikataba feki inayoingia nchi yetu hasara kubwa sana na pesa hiyo inaenda kuwekwa nje, yote hiyo ni fedha haramu. Lakini utafiti wa hivi karibuni unasema kwamba nchi maskini ikiwemo Tanzania zinapoteza zaidi ya dola bilioni 20 kwa mwaka kutokana na vitendo hivyo haramu, rushwa, mikataba feki, ujangili na kadhalika. Lakini ukilinganisha na fedha ambayo tunaingiza kama misaada kutoka nchi za nje kutoka nchi tajiri tutapata kama dola bilioni 50 tu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ukiangalia hela inayotoka ni nyingi kuliko inayoingia. Nimefarijika sana kwa marekebisho yaliyofanywa katika Muswada huu hasa Ibara ya 3 yaani kifungu cha tafsiri ukurasa wa 48 ambapo kwa kweli nimefurahi kwamba *predicate offence* zimeongezwa. Zimekuwa nyingi mpaka rushwa imeingia, vimeingia vitu vingi, *tax evassion.* Nimefurahi sana na nawapongeza sana Wizara kwa kufanya hilo. *(Makofi)*

Napenda hata kosa ambalo wenzetu Jumuiya ya Ulaya wanalo ambalo linawabana watu wanaoingiza jamii kwenye mikataba mibovu na hasara nyingi, wao wanaita *fraud to the detriment of the financial interest of the EU.* Ningependa ingekuwa *to the financial interest of Tanzania,* lakini hata hivyo mimi nimefarijika kwamba kifungu cha 3 kinamruhusu Waziri *from time to time* kuweza kuongeza makosa mengine. Hilo usitubane sana hapa, mimi nadhani marekebisho yaliyofanywa ni mazuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kifungu cha 13 na kifungu cha 20 nimefurahi sana tena sana kwamba adhabu sasa hivi kwa kweli mimi zimeniridhisha, ni nzito kuweza kumwonya mtu ambaye anataka kujiingiza kwenye mambo haya. Ibara ya 21 imetuletea ubishi kidogo wanasheria juzi hapa. Tulikuwa tunasema aah, mbona hii ibara inakuwa kama inaondoa *requirement* ya *secrecy,* usiri kati ya mteja na wakili, kwa mfano. Lakini baada ya kuusoma vizuri huu Muswada hasa ukisoma ile ibara ya 21 pamoja na ibara ya 3 unaweza kugundua kwamba hapana. Usiri kati ya mteja na Wakili, kwa mfano sisi Mawakili bado uko pale pale. Umeondolewa katika maeneo mawili tu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikiliza Kiongozi wa Upinzani akisema kwamba kwa kweli hata suala la ufaragha ambalo ni haki ya Kikatiba, pengine lingezingatiwa. Lakini mimi nasema hapana, ukiangalia Katiba yetu kweli Ibara ya 16 inaeleza haki ya ufaragha ya mtu mmoja mmoja. Lakini ukiangalia pia Ibara ya 30 haki ile ya ufaragha ya mtu mmoja mmoja inamezwa na haki ya maslahi ya umma. Kwa hiyo, mimi nadhani ni sahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa maombi mawili tu kwa Serikali, la kwanza, kama dhamira yetu kweli ni kuifanya Sheria hii ifanye kazi kweli kweli, basi mimi naona hatuna budi kuboresha mazingira ya kazi ya Maafisa wa hiyo *Finance Intelligence Unit (FIU).* Kwa kweli ni kazi yenye vishawishi vikubwa. Wakianza kazi yao na mazingira ya kazi magumu, basi kwa kweli tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu.

Vile vile mbali na hawa *reporting persons* wanaotajwa kwenye huu Muswada, mimi naona makundi mengine mawili muhimu ya watu wanaweza kutusaidia sana kuifanya hii Sheria ifanye kazi vizuri zaidi. Kundi la kwanza ni vyombo vya habari, ili viwe msaada katika *operationalization* au katika kuitekeleza hii Sheria hatuna budi kuwekeza zaidi kwenye *training* ya vyombo vyetu vya habari ndani na nje ya nchi. Hatuna budi vile vile kusikiliza sasa kilio cha vyombo vya habari cha muda mrefu cha kufuta Sheria ambazo zinazuia zuia ukusanyaji na *distribution* ya habari, *distribution* ya *news*.

Lakini vile vile nilikuwa nadhani kwamba umefika muda wa kulifanya suala la utoaji habari lisiwe la hiari, lisiwe la hisani. Lakini uwe ni wajibu kwa watu ambao wako kwenye kazi ya umma na vile vile kwamba muda umefika kwa suala la mazingira ya kazi na kipato cha waandishi wa habari kuweza kutupiwa jicho sasa.

Nimalizie kuhusu suala la *whistle blowers. Whistle blowers* amewagusia kidogo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, lakini hawa ni watu ambao wako ndani ya Taasisi hiyo hiyo na kwa moyo wao tu wa uzalendo wanataka ku-*report* kwa chombo kinachohusika ambacho ni *FIU* kwamba kule kunatendeka mambo haya na haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba kwamba *FIU* ikishaundwa, kuna umuhimu wa kuweka utaratibu wa kuwalinda *Whistle Blowers Tanzania* kwa sababu tuna historia mbaya Watanzania katika ku-*handle* watu wanaojitolea kutoa taarifa kwenye vyombo vya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasikia mara kwa mara watu wanaogopa hata kwenda polisi kwa sababu kesho asubuhi anajikuta kwamba hiyo shutuma inamrudia yeye mwenyewe. Mimi ni mfano ulio hai wa *whistle blower* niliyejaribu kusimama kidetete kwa maslahi ya Taifa, nikaishia kuji-*blow up* mimi mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilielezee ili liingie kwenye *Hansard.* Mimi nilikuwa Mkurugenzi wa *NBC Limited,* nikakuta ufisadi ndani ya hilo Shirika ambalo Serikali yetu ina hisa. Nikavitaarifu vyombo vyote vya umma na Wizara husika. Wizara ikanigeukia kuniomba mimi nijiuzulu ili wazungu waendelee kutesa na kuiba. *(Makofi)*

Nikajiuzulu, lakini haikuishia hapo ndiyo madhara ya *whistle blowing Tanzania* ambayo lazima yarekebishwe, *otherwise* hizi sheria zitaishia tu kuokota uchafu kwenye *shelves.* Haikuishia hapo Wizarani au niseme Serikali ikahakikisha kwamba huyu *whistle blower* anaondolewa kwenye kila Bodi ya Wakurugenzi ili asiendelee ku-*whistle blow* kule. Lakini mimi hiyo haikunisikitisha kwa sababu nchi hii ni yetu na lazima tufanye kazi kuweza kuisaidia mpaka leo ninapoongea nilijiuzulu tarehe 18 Septemba, 2003. Hakuna Afisa yeyote wa Serikali amekuja kuniuliza bwana eeh, hebu tupe ushahidi, nina ma-*volume* yamejaa vumbi hakuna hata *messanger* wala kiongozi wa Serikali kuja kuniuliza, nilikuwa na ushauri upi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasema kwa kweli historia yetu kama Serikali katika ku-*protect whistle blowers* ni mbaya kupita kiasi, kwa hiyo, kuna umuhimu. *FIU* ikishaanza kazi basi iweke utaratibu wa kujenga *confidence* kwa wananchi kuweza kujitolea. Tena ukishajitolea kuna tatizo kubwa linakufuatilia. Unakuwa *stigmatized,* yule mtu mbaya yule. Ubaya wako ni kutetea maslahi ya umma. Kitendo kilichofanyika mwaka 2003, kimenirudia juzi tulipokuwa na uchaguzi hapa unasikia tena baadhi ya viongozi aah, yule mbaya sana yule Mwakyembe, atatusumbua kule mbele. Kuwasumbua kwa maslahi ya umma? Kwa kweli hii ni aibu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja hii bila kigugumizi na nadhani tunawajibu Wabunge wote tuliopo hapa kuupitisha huu Muswada, ni muhimu sana. Ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu ulio mbele yetu. Awali ya yote napenda kuungana na mchangiaji aliyetangulia kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta mbele yetu Muswada huu wakati huu ambapo fedha haramu zinatesa sana dunia na zinatishia tu siyo uchumi wa dunia, pia na amani ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ambazo zimeanza kutekeleza kama Sheria Muswada huu nchi nyingi za Ulaya, Marekani zimetunga Sheria mahususi ambazo zinawalinda watoa habari. Nina mifano, hapa nchini kwetu miaka ya 1990 tumewahi kuona mtu mmoja amekamatwa au Taasisi wamekamatwa na dawa za kulevya, wamekatwa wamepelekwa Mahakamani, wamepelekwa jela, tena jela yenyewe ya *maximum protection* ya Ukonga. Lakini baada ya miezi miwili mtu huyo tumeambiwa ametoroka jela. Hiyo ni nguvu ya pesa aliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi hapa mtu mmoja mtumishi amekamatwa kwa sababu ameiba pesa za Serikali karibu milioni 800. Amewekwa jela, amewekwa sijui Segerea sijui Ukonga. Huyo mtu anasema yeye mgonjwa, anakaa miezi mitano, ni mgonjwa lakini hiyo ni *collusion* tu kawakatia maafisa wanaohusika na ndugu zake. Huyo mtu baada miezi hiyo mitatu, minne, mitano amekaa hospitali ya Muhimbili, anatoroka akiwa Muhimbili, kwa sababu ya nguvu ya pesa hii. Pesa haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali baada ya kuuleta Muswada huu ukapita kuwa Sheria, Serikali ilete Muswada mwingine ili itungwe Sheria mahususi ya kuwalinda watoa habari. Kwa sababu watu hawa wana pesa sana na wana nguvu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi kama India au Uingereza huwezi ukaingia tu pale ukafika ukasema mimi nataka kuwa na simu ya mkononi ukanunua, ukaweka *line* ukaanza kuongea. Hizo simu lazima zisajiliwe. Tukiwa kwenye semina yetu siku ya Jumamosi, wataalam waliokuwa wanatuelimisha kuhusu Muswada huu kuna wataalam wa usalama ambao walisema kwamba wao hata wakipata ile kadi ya simu ambayo mtu ameitumia imetupwa, imeshatumika, akiipata namba zile inaweza ikamwongoza kwenda kumkamata mhalifu. Sawa tunakubali kwamba wana utaalam huo na taalum hiyo ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ingekuwa rahisi zaidi, ingekuwa bora zaidi, ingekuwa simu za mkononi zimesajiliwa. Tuko Watanzania milioni 36 au milioni 37, nchi kama India ambao wana watu bilioni moja wanasajili simu za mkononi, tutashindwaje Watanzania milioni 35? Nadhani kungekuwa na kanuni au sheria ambayo inalazimisha Watanzania wote kusajili simu zao ingerahisisha sana katika zoezi hilo la kukabiliana na wahalifu wa fedha haramu. *(Makofi)*

Mwisho, naiomba sana Serikali iweke kampeni kabambe ya kuwafahamisha wananchi kuhusu Muswada. Wananchi wengi hawaelewi, wao wakiona maisha ya Mheshimiwa Mwambalaswa leo alikuwa ana *Voksi wagen* kesho ana *VX* wao wanashangilia wanaona kama ni umaarufu. Kile kitendo cha kuhoji kwamba imekuwaje, maisha yake yamebadilika wanaona kuwa na mapesa ni umaarufu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ifanye kampeni kabambe ya kuwaelimisha wananchi ili wajue fedha haramu ni nini na matokeo yake ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo tu. Kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri na kuipongeza Serikali kwa ujumla kuleta Muswada huu ambao kwetu ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kwanza ambacho tutatakiwa tujiulize ni kwamba hivyo hawa watu ambao wana uwezo wa kuwa na fedha haramu ni akina nani? Tusije tukaanza kuzungumzia kama vile ni watu wanatoka nje huko tu wa aina yake. Watu hawa ni watu matajiri sana na watu matajiri hutengeneza watu matajiri wenzao ili washirikiane, hawakai tu matajiri peke yao wakawa matajiri. Akiwa tajiri anataka tajiri mwenzake, wazungumze naye, wajadiliane naye, wafanye naye mambo wanayofanana fanana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika hawa ni watu hatari sana. Duniani kuna nchi zingine watu hawa hawataki kuingia hata kwenye siasa. Hawataki hata kujulikana, kwa sababu wao ndiyo wanaoendesha Serikali. Wana Serikali yao chini, pembeni ya kuendesha Serikali iliyochaguliwa. Kwa mantiki hiyo, watu hawa wana uwezo wa kununua viongozi ndani ya Serikali, wana uwezo wa kutoa rushwa wa kufanyiwa kitu chochote, wana uwezo wa kuua wakati wanataka mtu afe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika hii si sheria tu ya kawaida, Sheria ya kawaida ipo hapa Mheshimiwa Waziri ameitaja. Sheria inayoitwa *The Proceed of Crime Act No. 256* toleo la mwaka 2002. Imeingiza kila kitu lakini bado ilikuwa haitoshi kudhibiti watu hawa ambao wanatumia fedha haramu kuhalalisha na lingine vile vile ni vizuri tukaelewa hivyo ni nani huyo na anazitumiaje hizo fedha haramu. Kwa sababu wananchi wa kawaida inawezekana wakawa saa hizo sisi tunazungumza wao wanaanza kujiuliza kitu gani fedha haramu. Kuna watu wengine wanasema fedha ni fedha tu, haramu, halali mimi naendelea. *(Makofi)*

Lakini si kweli, mtu anakuja na fedha zake nyingi sana anakuja anataka kuwekeza, lakini atamwona nani kwanza. Kuna watu ndani ya nchi humu humu ambao watamsaidia, anaanza kuwanunua hao, anawekeza kwa hali ya juu sana. Huwezi kuwajua hao, matokeo yake ya kuwekeza ndiyo sasa yanazalisha fedha halali. Ameitengeneza fedha haramu ama kwa kuiba ama kwa kuuza dawa za kulevya, ama kwa kuuza binadamu, ama kupewa kwa rushwa na sasa anatengeneza matokeo yake kuwa fedha hiyo sasa inakuwa fedha halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa wana uwezo na wanaweza wakawa Wabunge. Maana yake tusianze kuzungumzia nje, wako ndani ya Bunge wana uwezo huo, ndani ya Serikali wana uwezo huo. Tuanze kuangalia kwanza nyumba yetu kabla hatujaangalia nyumba ya mwenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ndani ya Serikali na ndani ya Bunge hili na ndani ya wafanyabiashara na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali wapo wenye uwezo wa kufanya hayo? Tunawadhibiti vipi? Wako watu wanapewa rushwa mpaka hawajui wafanye nazo nini hizo pesa. Kwa nini wasizigeuze hizo fedha sasa zikawa fedha halali. Wako watu wanafanya vituko kabisa hapa na wanaachiwa, katika misingi ipi?

Naomba ombi langu la kwanza kabisa juu ya Muswada huu ni hao wahusika ndani ya *Financial Intelligence Unit* wapewe maslahi makubwa kabisa ambayo yataepusha watu hawa kushawishika kwa namna yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiwe na wivu kuwafanyia mambo haya, tumejaribu hii kwa *TRA* na imefanya kazi. Watu hawa ukiwapa mshahara kama unampa Mbunge umefanya kazi ya bure. Kama wewe unaweza kumtoza faini mtu binafsi aliyehusika na kosa hili kufuatana na kifungu cha 13, shilingi milioni 500 sasa yule anayemshughulikia unampa shilingi laki mbili mshahara, hufanyi kitu. Lazima wawe na maslahi makubwa sana ya kufanya kazi kwa utulivu.

Mimi nashukuru sana Ibara ya 3 ya Sheria hii imeingiza mambo mengi sana, mpaka rushwa kitu ambacho kilikuwa ni muhimu sana kiingie mahali pale. *(Makofi)*

Kuhusu dawa za kulevya mpaka bangi, mimi nashukuru najua kule kwangu tunalima sana bangi. Nilikuwa sijui hata mimi Mbunge wao. Lakini juzi Polisi wamenithibitishia kabisa kwamba Mheshimiwa Mbunge watu wako wanalima bangi. Lakini kufikia ile sehemu wanayolima bangi ni ngumu kweli kweli lazima uende kwa miguu milimani juu. Nashukuru sana Polisi wamechukua hatua hiyo wamegundua. Lakini hao watu wanauza wapi? Ndiyo nilikuwa najiuliza. Lazima kuna watu wamewatuma, wana uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengine wanatakiwa kulindwa katika sheria hii ni Waandishi wa Habari. Mimi naomba niwatahadharishe sana. Mimi mwenyewe ni Mwandishi naandika vitabu, siandiki habari. Lakini kitu kikubwa sana kwa waandishi wetu wa habari sasa ni wakati kwa sheria hii ukimwandika mtu kwamba yeye ni mmojawapo katika *money laundering* uwe na uhakika umefanya *research* utakaa siku mbili hapa tu, utapotea. Ukumbuke unaandika watu wenye uwezo sana. Ni *group* la *mafia.* Hawana mchezo, hawataki kutaniwa, hawataki kuchezewa kwa namna yoyote. Kwa hiyo, fanya utafiti kabla hujaandika ili uwe na uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine muhimu katika ibara hii, unaniona ninachukua hapa na pale kwa sababu mimi ni mmoja katika wana Kamati huko, kwa hiyo, kuna vitu vingine kwamba huyu mwingine ambaye anafikiriwa anafanya *money laundering* anasaidiwa na watu lazima wawepo hapa, kama anaifanya Tanzania anasaidiwa na Watanzania. Kwa hiyo, wao tayari wana msingi mkubwa wa kupewa rushwa kubwa na pesa nyingi. Je, wanahusika vipi kwa makosa katika sheria hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamzungumzia huyu tu ambaye yeye anahalalisha pesa haramu? Waliyemsaidia kuhalalisha pesa haramu tunawashughulikiaje kwa Muswada huu. Huu Muswada lazima wao wahusike, kwa bahati mbaya kabisa jana nilipokuwa nakisoma hiki ndiyo nimeona hawa watu ambao wanasaidia watu wanaokuja kufanya *money laundering,* biashara ya fedha haramu hawamo kwenye Muswada huu. Naomba Waziri aliguse hili, tujue wanahusika vipi hawa katika kupigwa faini na kufungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ambalo ni muhimu kabisa Sheria zote zilizotajwa kwenye *Crime Act No. 256* ziko nyingi mle lakini hakuna Sheria ya kumlinda shahidi. Sasa nani atajitolea kumtambulisha shahidi hata jambazi tu wa kawaida unaogopa. Sasa unakwenda kumtambulisha shahidi ambaye ana pesa nyingi au ukimwonyesha kidole watu wengine wamekwishakuona 10 na huyo ambaye atajitolea kwa vyovyote vile kushiriki na kuisaidia Serikali kutambua, Serikali inamlinda vipi, sheria gani inamlinda *witness* maana yake pengine itabidi ahamishwe kabisa, anatoka Dar es Salaam anakwenda Umasaini kule na anakuwa Mmasai katika kumlinda na Serikali inamgharamia, sheria gani inatumika kumlinda?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechunguza hilo, tumezungumzia hilo kwenye Kamati hakuna sheria inayomlinda shahidi, *whistle blower* hakuna hizo sheria, watu wanaogopa.

Kwa hiyo, mara moja sheria hii leo tunaipitisha naomba sana Serikali tunapokuja kikao cha Januari wajitahidi kweli kweli kuleta sheria ya kumlinda shahidi kabla watu wetu hawajaanza kugongwa gongwa. Ni muhimu kabisa sheria hiyo ikaja hapa. Kuchelewa kwa sheria ya kumlinda shahidi ni kumkosesha shahidi raha na kumwogopesha mtu yeyote mwenye ushahidi kuja kujitolea kutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana na Waziri wa Fedha anajua, *AG* anajua. Mwanasheria Mkuu tulikuwa tunazungumza habari hizi muhimu kabisa, walete sheria ya kumlinda shahidi ambaye atatoa ushahidi juu ya watu hawa. Hawa si watu wa kuchezea hawa na wala Mbunge usiinueinue shingo hapa ukafikiri unaweza kutania tania mambo haya. Hawa ni watu wakubwa wa aina yake na inawezekana wapo sijui. Hawapo sijui, lakini wanaweza kuendesha Serikali wanavyotaka wao. Ninyi mnapitisha Sheria wao wanaendesha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo ukubwa wenyewe huo, zamani tulikuwa tunasema fedha haiwezi kutawala siasa. Lakini sasa tunasema siasa inatawaliwa na fedha na ni hatari. Sio lazima nikupe wewe moja kwa moja. Mimi naweza nikatawala kiongozi wako na kiongozi wako akikuambia hili jambo ndilo linakuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa tu najaribu kuongezea ongezea vitu na kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati hiyo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Vuta kidogo halafu!

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge jina, linaloonekana hapa, linaonekana ni la Mheshimiwa William Ngeleja, na siyo la kwako.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kutumia *Microphone* yangu, naona imekataa, lakini ninatumia sehemu ya Mheshimiwa William Ngeleja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuwa mmoja kati ya wachangiaji wa kupitisha Sheria hii ya Udhibiti wa Fedha Haramu katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Mimi nadhani nitakuwa nina sehemu moja tu ambayo ndiyo nitaizungumzia zaidi na hii si sehemu nyingine bali ni sehemu ya dawa za kulevya ambayo binafsi yangu naona inawaathiri zaidi na sana vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa na ndiyo Taifa la kesho na ndiyo watu ambao tunawategemea. Lakini wanakuwa waathiriwa sana na dawa hizi za kulevya. Nimekuwa nikizungumza toka nyuma, juzi nimezungumza na leo naomba nizungumze tena msinichoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kuzungumzia kitu kimoja kwamba naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuliangalie suala hili kwa umakini zaidi na tuliangalie suala hili kwa upana zaidi. Kama inawezekana tubadilishe sheria za nyuma ambazo zimepitwa na wakati, ambazo haziendani na wakati wa sasa. Haziwasaidii watu ambao wanaathirika na utumiaji wa dawa za kulevya, bali zinakuwa kama vile zinawanufaisha watu wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa za kulevya ni kitu hatari sana katika jamii yetu ya Watanzania na kwa vijana ambao ndiyo waathirika wakubwa. Sheria zimekuwa zikizungumzwa hapa, tunaambiwa watu watakamatwa. Lakini kinachoniuma na kunisikitisha zaidi mimi ni kwa sababu watu bado wanaendelea kuuza dawa za kulevya, vijana bado wanaendelea kutumia madawa hayo na wananchi wanawafahamu wauzaji wa dawa za kulevya, lakini wanashindwa kutoa taarifa, inabidi tu wakae kimya, kwa sababu wanatoa taarifa polisi, mtu anakamatwa, jioni mtu anaachiwa.

Kwa hiyo, mwananchi anakuwa ameshajiweka katika mazingira ambayo ni ya hatari kabisa. Sasa hivi watu wanajua siyo kama hawajui. Wananchi wanajua na kufahamu, lakini wanashindwa kuongea, wanashindwa kusema, inabidi tu wakae kimya na kuvumilia na mambo yako huko huko mitaani. Lakini wanashindwa kusema kutokana na Sheria zetu ambazo zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa nikipitia huu Muswada ambao tunatarajia kuupitisha, Muswada huu wa Udhibiti wa Fedha Haramu, wanasema mtu kama akikamatwa na kosa la dawa za kulevya, anaweza akafungwa si chini ya miaka mitano ama kumi au anaweza akatozwa faini ya shilingi milioni mia moja na zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nikasema mwanzoni kwamba tuziangalie sheria zetu, inawezekana nyingi zimepitwa na wakati. Kwa sababu kama mtu anakamatwa na mzigo wa dawa za kulevya wa shilingi bilioni moja au mzigo wa shilingi milioni mia tano, milioni mianane. Mzigo labda wa shilingi milioni mia, milioni hamsini, unamtoza faini ya shilingi milioni moja, unamuacha na mzigo wake anaondoka nao, yeye ametoa shilingi milioni moja, bado anaendelea kuuza ile biashara na bado anaendelea kuwaharibu hawa vijana.

Naiomba Serikali, kama ambavyo imeonyesha umakini wake katika zoezi la bomoa bomoa mjini Dar es Salaam, wamelifanya zoezi hili kwa umakini sana. Wamebomoa hata sehemu ambazo ni sehemu za viongozi. Ni kweli tunasema sheria ni msumeno, inafanyakazi yake, imepita mpaka kwa viongozi. Hili suala la dawa za kulevya lichukuliwe hivyo hivyo kama ambavyo bomoabomoa na mazoezi mengine ambayo Serikali imekuwa ikiyasema yafanyike kwamba watu wanaouza dawa za kulevya wakamatwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni mimi Amina ninauza nikamatwe, hata kama ni Mbunge, kama ni mume wangu anauza hata kama ni mume wa Mbunge akamatwe, kama kuna Mbunge humu ndani anafanya biashara ya dawa za kulevya jamani akamatwe na kufikishwa katika vyombo vya sheria na sheria ziwe kali. Kama kuna kiongozi

mwingine yeyote wa nchi, sheria ni msumeno kama nilivyosema imkute kila mtu ikate kila mahali. Lakini siyo sheria ni msumeno kwenye bomoabomoa tu na mazoezi mengine, inapokuja kwenye *issue* ya dawa za kulevya sielewi kinachofanyika kwa kweli sielewi. Ingekuwa mimi ni polisi na nina majukumu, nasema leo ningetoka ningekwenda kuwakamata wanaouza dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi ni Mbunge, nitafika na kukamata, mimi siyo polisi, sina jukumu lolote, sina uwezo. Wananchi wanayajua haya, mbona hatufanyi upelelezi wa kutosha huko mitaani jamani? La kujiuliza hapa ni moja tu, kama vijana wanatumia dawa za kulevya wanapata wapi? Dar es Salaam pale kuna nyumba, siyo hospitali, hazina Daktari ndani, lakini zinapokea watu 500 mpaka 200 kwa siku wanaingia katika nyumba moja wanatoka. Wanaingia wanatoka, wanaenda kufanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, polisi mnasema hamna ushahidi. Ushahidi gani mnaousubiri zaidi ya huo kama mtu akiingia anatoka. Dawa kwani zinapatikana wapi jamani, si yapo? Yako mitaani, yapo. Lakini nikisema naambiwa Amina huyu mdogo, umri wake hajui mambo yanavyokwenda. Sidhani kama ni mdogo wa hivyo wa kushindwa kutambua jema na baya, wakushindwa kutambua mambo yanavyokwenda. Naweza nikawa ni mdogo kiumri, lakini kutokana na elimu yangu niliyopewa. Elimu ndogo ninayopata kutoka humu Bungeni, ninavyojichanganya na watu, ninao uwezo wa kutambua hili ni jema na hili ni baya. Hili lifanywe hivi na hili hivi. Jamani ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tutunge sheria ambazo ni kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sioni sheria ya kumwambia mtu unamfunga miaka mitano kwa sababu umemkamata na dawa. Tuchukulie mfano, mtoto mdogo leo, akibakwa na mtu mzima, sheria inavyosema ni kwamba anatakiwa afungwe jela maisha. Mtu mzima mmoja ambaye amembaka mtoto mdogo, iweje leo mtu mzima mmoja anayewaathiri vijana hamsini, vijana mia moja wanaoharibika kwa mara moja, wanafikia mpaka kufa, anatozwa faini ya shilingi milioni mia moja na kuachiwa? Anaingizwa Gerezani miaka mitano na kutoka. Hivi kweli jamani ndiko tunakoelekea, hivyo ndivyo nchi inakokwenda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuseme ukweli, tuzungumze ukweli, tusiwe wanafiki. Siyo kuogopa tu, mimi naogopa sizungumzii dawa za kulevya wataniuwa. Unaweza ukauliwa na dawa za kulevya bila hata kuthubutu kuyazungumza. Kwa hiyo, kama Mungu amekuandikia kufa kwa dawa za kulevya utakufa tu, hata usipozungumza Bungeni na kama Mungu amekuandikia usife, hautakufa. Mimi naongea hapa japo watu wanasema ni jambo la hatari, mimi ni mdogo. Lakini naamini na ninamuamini Mungu, yeye ndiye mwenye uwezo wa kunisaidia mimi, kama niliandikiwa kufa kwa dawa za kulevya, nitakufa hata nisipozungumza hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba tulichukulie hili kama ni jambo la dharura na tuliangalie kwa makini. Leo unaweza ukaliona jambo hili halikuhusu kwa sababu mtoto wako hajaathirika kutokana na dawa hizi au vijana wako, watu wako wa karibu unaokaa nao hawajaathirika. Lakini

kwa mtindo huu tunaokwenda nao, kwa *speed* hii vijana wengi wanavyozidi kuathirika kesho litakuwa ni tatizo lako Mheshimiwa Chikawe, kesho tatizo lako Mheshimiwa Ngeleja, kesho ni tatizo lako Mheshimiwa Makinda, Mheshimiwa Mama Anna Komu na Waheshimiwa wote waliopo humu ndani. Tuliangalie kiundani jamani. Mimi linaniuma yaani linaniuma sana, ndiyo maana nalizungumza, tusilione kama ni jambo la mchezo, hili ni jambo zito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, japo ni jambo la dunia nzima, nchi zote liko, lakini mbona wenzetu wana utaratibu, wanaheshima, ukifika nchi za watu huwezi ukaambiwa pale dawa za kulevya zinauzwa, huwa ni siri kwanza, ni siri ya kupita kiasi, iweje hapa Tanzania ni rahisi kutamka tu kwamba pale kuna dawa za kulevya, ni kwa nini? Kwa nini hatuko makini na hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia kitu kimoja, mimi ninamshukuru Mwenyezi Mungu, nilikuwa sijawahi kufika Uingereza. Lakini kutokana na safari hizi za Bunge, wiki mbili zilizopita nilikuwa nchini Uingereza na Wabunge wenzangu nane ambao tulitumwa kwenda kule kwa ajili ya mafunzo nchini Uingereza. Tukatembelea *House of Commons, House of Lords,* pamoja na maeneo mengine mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho mimi nilikipenda japo kinakera, kinaudhi, lakini nakipenda na ninawasifu Waingereza, baada tu ya kupewa tishio la ugaidi kwamba watalipuliwa wakati wowote, wamekuwa makini sana, sana kupita kiasi. Ukifika *Airport* unakaguliwa hawajali wewe ni Mbunge, umetoka Tanzania umetoka sijui nchi gani. Wewe ni mgeni wa Uingereza uko pale, hata kama ni nani, unakaguliwa kila kitu. Hauruhusiwi kwenye *hand bag* yako kwa sisi wanawake tubebe sijui *lip stick,* vitu vya *liquid,* siyo sheria. Lakini ni utaratibu wao ambao wao wamejiwekea wa kuhakikisha kwamba hawafikiwi na madhara makubwa. Mimi ninapenda niwapongeze kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeenda Dubai, hatukuwa *searched,* tumepita, kila mtu ana utaratibu wake. Hata sisi Tanzania pia tujenge taratibu kama walivyo wenzetu, wakiamua jambo wanalifanya hata kama ndiyo tunakuwa *searched* na mambo mengine ambayo unayaona ni maudhi. Lakini sawa si mmetishia kwamba ugaidi utakuja hapa watu watalipua majumba na watu watakufa. Lazima wajihadhari na sisi kama Tanzania, kama wananchi, kama Wabunge, kama wazalendo wa nchi hii, tunawasaidia vipi wale vijana wanaothirika na dawa za kulevya. Leo tunapitisha hapa sheria ya udhibiti wa fedha haramu, bado mimi naona miaka mitano, miaka kumi ni kidogo sana. Bado naona miaka mitano, miaka kumi ni miaka michache na haitoshi kwa hawa watu ambao wanafanya hizi biashara ya dawa za kulevya. Kwa hiyo, chonde chonde, naiomba Serikali yetu, wananchi wana imani kubwa na Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Naomba wapelelezi mfanye wajibu wao, polisi fanyeni wajibu wenu yaani hata sijui hata nisemeje. Lakini inasikitisha kuona kwamba maeneo ya watu wanaouza dawa za kulevya yanajulikana, watu hawakamatwi, wanajua kabisa huyu mtu anauza dawa za kulevya, tena wanasema kabisa, yule fulani anauza, wanazungumza tu chini chini, lakini

kwa nini waongee chini chini, wewe polisi kwa nini hutimizi wajibu wako? Huo ushahidi unasubiri upate ushahidi mpaka lini? Tukisema hivi basi hautapatikani maisha, vijana wataendelea kutumia dawa za kulevya, tutakuwa na Taifa ambalo lina watoto wajinga, watoto mataahira, wameharibiwa, Taifa la kesho, hata sijui litakuwaje. Sasa hivi tunashukuru viongozi wapo, lakini nina wasi wasi kama tukiendelea hivi, miaka ishirini, thelathini ijayo, hawa vijana ambao tunawategemea ndiyo waje kuwa marais wetu, mawaziri wetu, viongozi wetu wa baadaye, tutakuwa katika hali gani, Taifa gani? Watu wanasema vianzishwe vituo vya kuwatengeneza wale watu ambao wamekwishathirika kutokana na dawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa mimi hili siliungi mkono. *Okay,* sawa sasa hivi kuna watu ambao wameathirika wanatakiwa watibiwe. Lakini tutakapoanza kujenga vituo kama hivi ni kwamba tumehalalisha hiki kitu kifanyike. Naomba Serikali ichukulie suala la dawa za kulevya kama ni jambo la dharura ambalo linatakiwa lifanyiwe kazi. Asiogopwe mtu kwa sababu ni kiongozi, asiogopwe mtu kwa sababu ni tajiri ana fedha, asiogopwe mtu kwa sababu tu ana vitu ambavyo havieleweki sisi wote ni Watanzania tuna imani na Serikali ya awamu ya nne, hii ni changamoto. Ninaumia, naniumi sana, tena sana, kuona hatua zozote hazichukuliwi na watu wanaendelea kuuza madawa, halafu unanieleza sijapata ushahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru Mbunge wa Vijana, unayo sababu. Sasa anafuata Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, atafuatiwa Mheshimiwa Esther Nyawazwa na Mheshimiwa Peter Serukamba pia ajiandae.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie katika Muswada huu muhimu uliopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimshukuru Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, kwa jinsi alivyoufikisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu. Kabla sijaendelea napenda nitamke rasmi kwamba ninauunga mkono Muswada huu, lakini ninayo maoni yafuatayo ambayo nigependa yazingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo sheria nyingi ambazo zinashughulikia kwa namna moja au nyingine tatizo lililo mbele yetu, miongoni mwa Sheria hizo ni pamoja na *The Drug Trafficking Act, Bank of Tanzania Act, Banking and Financial Insitutions Act, Proceeds of Crime Act, 2002,* TAKURU na sheria nyingine ambazo zinafahamika. Sasa tatizo ni kwamba kwa nini bado leo hii tunalazimika kupitisha sheria nyingine?*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nionavyo mimi, tatizo si sheria, tatizo ni utekelezaji. Utekelezaji hafifu, utekelezaji usio makini wa sheria zilizopo. Mfano hai ni pamoja na maoni aliyoyatoa mzungumzaji aliyenitangulia kuhusu dawa au madawa ya kulevya. Maoni yake ni sahihi, malalamiko yake ni sahihi, lakini ukweli sheria zipo, tatizo ni utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye sheria, mathalini ya *Banking and Financial Institutions Act of 1992* kama ilivyofanyiwa marekebisho katika nyakati mbalimbali. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine, inaipa jukumu la uangalizi wa shughuli za Mabenki Benki Kuu ya Tanzania kwa maana ya *Banking Supervision.* Jukumu hili ni kubwa na liko chini ya Benki Kuu ya Tanzania na kutokana na kutekeleza wajibu wake huo Benki Kuu ya Tanzania ilitoa *Circular No. 8* kwa Mabenki yote. Waraka huu unajihusisha na suala zima lililopo mbele yetu, la *Money Laundering* kwamba kwa kutumia nguvu za kisheria, Benki Kuu itapitia na itapata taarifa zote zinazohusiana na *Money Laundering* katika Mabenki yetu na kwa maana hiyo kuchukua hatua zinazostahili. Sheria ipo leo hii bado tunalazimika kupitisha sheria nyingine juu ya suala hilo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina uhakika kama sheria ya *Banking and Financial Institutions* inaipa nguvu za sheria Benki Kuu, kuzijua *Bureau De Change.* Kama inaipa nguvu za Kisheria Benki Kuu ya Tanzania kuzikagua *Bureau De Change,* basi nazidi kusisitiza kwamba tatizo letu siyo sheria tatizo letu ni utekelezaji. Kwa mtazamo wangu mimi, tatizo hili la *Money Lanudering,* pamoja na yote tutakayoyafanya ipo haja ya kuongeza nguvu ya usimamizi wa shughuli za *Bureau De Change,* ama sivyo tutakuwa tunatwanga maji katika kinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Section IV(2)* ya Muswada tunaoujadili unazungumzia juu ya mambo mengine kwa kifupi *suspicious transanctions.* Tatizo langu mimi hasa hapa ni kuhusu kiwango cha *suspicious transanction* au *transanctions.* Ni vizuri tukawa tunafanya kazi inayoleta tija kuliko kuanza kufukuzia *transanction* ndogo ndogo. Kwa maneno mengine tutahadhari na kufukuza dagaa tukaacha samaki wakubwa. Sehemu hii ningeshauri iainishe kiwango cha *suspicious transanctions. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuchukue mfano wa Marekani, kule Marekani, unapoingia tu kama msafiri, miongoni mwa vitu vingine unavyotakiwa kufanya ni ku-*declare,* unaletewa *form* ya *Customs Declaration* ambayo pamoja na mambo mengine unatakiwa ueleze unaingia na fedha kiasi gani. Lakini wanakupa tahadhari kwamba ikiwa unaingia na fedha za kiasi cha Dola 10,000 au zaidi elezea kwenye ile fomu. Sasa sisi hapa hatuna utaratibu huo na kwa maana hiyo wanaoingia hapa nchini wanaweza kuingia na kiasi chochote cha fedha. Ningeshauri sheria hii iazime uzoefu wa Marekani kwamba wanaoingia Tanzania, iwe ni lazima ku-*declare* kiasi cha fedha wanachoingia nazo na hapa tufikirie tu hao wenzetu ambao tunawapa jukumu la kushughulikia sheria hiii, washughulikie kiwango ambacho ndicho tunaweza kusema ukiwa unaingia na kiwango hicho tueleze *at the entry point.*

Mheshimwia Naibu Spika, kwa nini ninasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu sheria hii ya *Anti-Money Laundering,* kwa mtazamo wangu imejikita sana kwenye pesa zinazopitia kwenye mikondo ya Mabenki. Lakini hebu tujiulize katika nchi yetu hii ya Tanzania ni asilimia ngapi ya uchumi wetu unaopitia kwenye Mabenki na kwa maana hiyo, ni kiasi gani cha fedha walizo nazo Watanzania ziko ndani ya mabenki? Ukweli ni kwamba wanaoutumia Mabenki kama Watanzania kiasilimia nadhani pengine hawazidi asilimia 25 na pengine hiyo asilimia 25 ni kubwa, ninalo jaribu kulisema hapa ni nini? Hoja yangu ya msingi ni kwamba uchumi wetu bado ni uchumi wa pesa za mfukoni.

Tunanunua kwa pesa taslimu, tunalipia mambo mengi kwa pesa taslimu, hatupiti kwenye Mabenki tulio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika kwa maana hiyo kama hatutapanua uwanja wa kushughulikiwa jambo hili la *Money Laundering,* tukaishia tu kwamba ni pesa zinazopitia Mabenki, sina uhakika kama tutakidhi haja tunayokusudia. Sehemu kubwa ya pesa za Watanzania ziko nje ya mkondo wa Mabenki kiasi kwamba zipo au wapo wafanyabiashara ambao wanakopesha pesa. Unakwenda unaingia unakopa, pale pale mnazungumza tu *terms* zenu, mkimaliza masharti yenu unapata mkopo wa shilingi milioni 10 mpaka 20 bila kupitia Benki. Sasa kuna haja kupitia maeneo hayo ili tuweze kuwa na uhakika kwamba tume-*cover* sehemu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa niliowazungumza kwa lugha ya kigeni wanaitwa *Money Changers,* wako wengi tu, ni nani anayewa-*supervise.* Kitengo cha *FIU* ambacho kinatarajiwa kuundwa chini ya sheria hii, mimi ningeshauri kiwe kitengo peke yake kabisa nje ya Wizara. Kinaweza kuwa chini ya Wizara lakini kiwe peke yake kabisa, nje ya Wizara kinafanya mambo yake kama kitengo chenye uongozi wake. Siyo chini ya uongozi wa Wizara, mambo hayaendi mpaka ifike kwa *Principal Secretary,* hapana, kiwe ni kitengo peke yake nje ya Wizara. Lakini tumeambiwa kwamba kitengo hiki ili kifanye kazi yake kitahitaji pesa za kukiendesha. Moja ya *sources* za *fund* ni kutoka kwenye *Budget* ambayo sisi kama Wabunge tutahijtajika kuziruhusu. Lakini nyingine ni *donations* na *grants.* Hivi kweli tunaunda chombo muhimu kama hiki halafu unatarajia kukiendesha kwake tupate *donations* na *grants,* zisipokuja? Kwa hiyo, mimi ningesema tuwe na uhakika na *sources* za *financing. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kilivyo chombo hiki, si chombo zalishi, hakitakuwa kinazalisha chochote, kitakachokuwa kinazalisha ni kuiondoloea Tanzania tatizo la kuwa pitio la *Money Laundery.* Kwa hiyo, ni vizuri tukawa na uhakika tutaki-*finance* namna gani. *(Makofi)*

Mheshmiwa Naibu Spika, kabla sijasema hilo lingine nisema kwamba Mashirika yetu ya dini. Mashirika yetu ya kidini, yanafaidika sana na misaada kutoka nje. Naomba nitoe kama angalizo kwamba katika kusimamia utekelezaji wa sheria hii, Mashirika ya kidini yasije yakaingizwa kwenye mlolongo ya kwamba hii misaada ina walakini, mnataka kufanya nini ninyi? Pengine wanataka kujenga makanisa, pengine wanataka kujenga misikiti, basi ni vizuri itazamwe kwa mtazamo huo isije ikadidimiza ile azma ya kuzisaidia au kuyasaidia haya mashirika ya dini, eti kwa sababu ya mashaka na hizi pesa wanazoletewa kujenga makanisa au misikiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya pesa ambazo baadaye huingizwa kwenye mkondo wa fedha haramu, kama sisi Watanzania, inabidi tuangalie maeneo mawili pamoja na mengine. Maeneo ya *over invoicing* za *imports* zetu na *under invoicing* ya *exports* zetu. Wanao-*over invoice import,* wanaifanya nchi inaingia gharama kubwa kwa *imports* zetu kuliko vile ilivyo sahihi. Kinachofanyika ni kwamba sehemu iliyokuwa-*over invoiced* inabaki nje na baadaye inaoshwa katika utaratibu wa kupitia haya ambayo leo tunayawekea sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *under invoicing* ya *exports* zetu ni kwamba muuzaji au *exporter* ana-*declare* kiasi kidogo cha thamani ya *exports* anazopeleka nje. *Difference* kati ya bei halisi na bei ailyo-*invoice* inabaki nje na baadaye inapitishwa katika mkondo wa kusafishwa. Hayo ni maeneo yanataka uangalizi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapitisha sheria ambayo ina mambo mengi muhimu na ni mazuri kwa Taifa letu, lakini ni lazima tujenge uwezo wa kusimamia na kuhakikisha kwamba yale maudhui yote tunayohitaji yafanyike, kweli yanafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii na mimi kuungana na wenzangu katika kupitisha Muswada huu muhimu kwa Watanzania. Kabla sijasahau naomba niuunguke mkono kwa asilimia mia moja huu Muswada upite. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umefika wakati muafaka. Lakini tunapitisha hii sheria, niiombe tu Serikali tutakapopitisha, elimu tupeleke kwa jamii, kwa sababu wananchi wengi hawatofautishi fedha haramu na mapato yanayotokana na biashara haramu. Nitaomba sana Serikali itusaidie kwa wananchi huko vijijini kuwafafanulia kutoa tofauti ya fedha haramu na mapato yanayotokana na fedha haramu. Nitaiomba sana Serikali ijaribu kutoa mafunzo kwa wingi ili kuwaelimisha wananchi kuhusu haya mapato yanayotokana na biashara haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama jamii haitahusishwa katika Muswada huu ni kazi bure. Nimechambua tu kidogo kuhusu biashara haramu kwa aina tatu, nyingine nimeziacha. Kuna biashara haramu ya umalaya, kuna biashara haramu ya utumwa wa watoto na kuna biashara haramu ya viungo vya wanadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria tunayoipitisha hapa Bungeni, lakini sisi kama jamii, tusipoisimamia sisi wenyewe haitafanya kazi. Ukilingalia suala la umalaya, kama sisi walezi, wazazi ndani ya familia zetu hatutalisimamia suala hili la kutoa elimu ya kutosha kwa vijana wetu, biashara kama hii sheria tutaisimamia biashara ya umalaya haitakuwepo kwa sababu jamii, tutasimamia kuhakikisha vijana wetu na sasa hivi Serikali yetu ya awamu ya nne imeleta fungu la uwezeshaji wa wananchi. Kama hatutawaelimisha hawa vijana wetu wakaachana na biashara mbaya kama hii ya umalaya, wakajiunga na *SACCOS* ambamo Rais wetu ameshawekeza mfuko katika kila Mkoa, hili suala la umalaya, biashara hii itafutika mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama jamii italiona hili, hii biashara ni halali na kama sisi wazazi ndani ya familia hizo utaona kijana wako anatoka ndani ya nyumba yako anaenda kufanya biashara hii tunaangalia tu, sheria hii haitawasaidia Watanzania na hasa vijana wetu na hasa vijana wa kike kwa sababu umalaya ya mtoto wa kike ni mkubwa zaidi kuliko umalaya ya mtoto wa kiume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utumwa wa watoto, sisi kama jamii hatutausimamia, ni mara kumi sisi kama jamii tukajihusisha na kukusanya, kama kweli tuna huruma na hawa watoto kwa nini basi tusiwakushanye hawa vijana, hawa watoto tukawapa elimu ndiyo itakuwa urithi wao kuliko unawakusanya hawa watoto unafanya biashara nao mbaya, upate mapato wewe ambayo yatakuwa yameathiri nchi yetu. Tuwasaidie watoto kama hawa, badala ya kufanya huu utumwa wa kuwakusanya, kuwafanyisha biashara yako, wewe ujinufaishe mwenyewe, tuwasaidie hawa watoto kwa kuwakusanya na kuwapa elimu ya kutosha ambapo katika miaka ijayo watakuwa wanajisaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la biashara haramu ya viungo vya bindamu ni biashara chafu na ni ya kusikitisha sana, lilitokea katika mkoa wa Mbeya na lilikuwa linaandikwa kwenye magazeti ya kwamba wanachuna ngozi wa binadamu. Kama jamii haitahusishwa kwa kulikemea hili kwa kuhakikisha kwamba hii biashara ni mbaya, tutakuwa na sheria ambayo haitasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba ili tuwape motisha wale wananchi watakaojitolea kutoa habari kwa chombo hiki ambacho kitaundwa cha *FIU* cha watalaam cha kuhakikisha kwamba kinawachukua hawa watu wanaofanya biashara hiyo walindwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamezungumzia usalama wa hao watu watalindwaje. Utamthibitishaje huyo mtu anayekuja kutoa habari usalama wake utakuwaje. Lazima tuangalie katika Muswada wetu huu unamlindaje mtu kama huyo, Mtanzania mwenye uchungu na nchi yake, anaona kabisa biashara hii inafanyika katika nyumba fulani, lakini anaogopa.

Naomba tuweke motisha kabisa ya kuhakikisha kwamba tunawaelimisha wananchi wajue kwamba watakapotoa habari kama hizo zitawasaidia watanzania na yeye atakuwa katika usalama mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wataalam ambao tayari sheria imewaainisha kwamba watakuwepo wataalam wa *FIU.* Kuhusu suala la rushwa, mtawawekaje wataalam wale katika kuwatoa katika vishawishi na kuhakikisha kwamba suala la rushwa halitawawekea vishawishi vya kuwaweka katika mtego ambapo wataletewa habari ya kwamba kuna watu fulani wana mamilioni ya fedha haramu wakaweza kumudu ili wawe na uzalendo wa kuhakikisha kwamba Taifa letu wanalisimamia vizuri. Lakini nitaomba zaidi wataalam hao wawekewe bima ya maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii kazi ni ngumu sana na inatakiwa moyo, kama hatutawawekea bima ya maisha, hao watumishi walioainishwa hapo kwenye Muswada. Tunaomba wawekewe bima ya maisha ili wajikinge kwa sababu watajulikana kwamba hao wako kwenye *FIU.* Watatekeleza jambo moja ambalo litakuwa ni kuwathibitisha kwamba ni kweli huyo ni mfanyabiashara haramu amethibitika kwamba hiyo fedha si halali, atarudi nyumbani, lolote linaweza likamtokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, familia yake ambayo atakuwa ameiacha, atakuwa ameicha katika hali gani. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kusisitiza kwamba wataalam hao walindwe na wakingwe baadaye kama litatokea baya fedha hizo ziwasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu wametuambia kwamba wananchi ambao wataweza kutoa taarifa wapewe saa 24. Nikikumbusha tu katika Bunge lako Tukufu hapa kwamba mawasiliano vijijini ni kidogo sana, mtu atoe habari kwenye vijiji vilivyoko huko tunakotoka barabara hakuna, huduma ya simu hakuna. Sasa wanaposema ataadhibiwa atakapochelewa katika saa 24 kufikisha hiyo taarifa, hizo saa 24 hazitoshi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Muswada huu unalenga kuhakikisha kwamba fedha haramu au mapato yanayotokana na fedha haramu tuyazuie kabisa katika nchi yetu ambayo yatakuwa yanadidimiza uchumi wetu na kuathiri usalama wa nchi kidunia. Naomba nipendekeze suala moja tu, pamoja na faini ipo imeandikwa kwenye Muswada huu na kifungo kimeandikwa kwenye Muswada huu. Kwa nini visiendane sambamba na kutaifisha mali zake zote ambazo zitagundulika zimetokana na biashara hiyo pamoja na kwamba ana kifungo. Lakini atakapopatikana na kesi hiyo na mali zake zote zilizotokana na fedha hizo kama nyumba, kama amewekeza kwenye vyombo vya usafiri vyote vichukuliwe na Serikali tuhakikishe kwamba tummaliza kabisa huyo mtu anayejihusisha na shughuli ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niendelee kuungana mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja na upitishwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umekuja kwa wakati na mimi naanza kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu na Sheria hii tuweze kuipitisha. Lakini mimi nasema sheria hii ni muhimu sana kwa sababu inashirikiana na sheria zingine katika kupambana na jambo hili ambalo kwa kweli ni baya sana kwa maendeleo ya nchi na kwa uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi la kwanza nataka tukubaliane hapa nadhani hii sheria ambayo tutaipitisha leo iwe na maana. Jambo la kwanza lazima kuwe na dhamira kweli ya kuitekeleza. Kwa sababu tunataka kwenda kupambana na watu ambao kwa hakika wana fedha, maana mtu akiwa na uwezo wa kifedha ana uwezo na watu wanaoweza kufanya huu uhalifu namna hii wana fedha nyingi sana ndiyo tunakwenda kupambana nao leo ili tuweze kufanikiwa la kwanza lazima iwe dhamira ya kweli. Sijui kama upande wa Serikali kweli dhamira ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana huko nyuma tulipitisha sheria mwaka 2002 ya *Proceeds of Crime Act* ambapo ukiisoma ile sheria ndani yake kuna *Anti Money Laundering*, tumefikia wapi mpaka tukaona sasa leo tulete sheria nyingine? Kwa hiyo,

mimi cha kwanza nilitaka nisisitize upande wa Serikali kwa kweli tuwe na dhamira ya kweli. Sheria yenyewe ni nzuri, lakini je, dhamira tunayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna namna ya kusafirisha pesa, watu hao kwa sababu wana uwezo mkubwa ambao wana fedha hizi, njia ya kwanza wanayotumia kusafirisha pesa ni kwenye *real estate* huko ndiko wanakokwenda kusafirisha fedha hizo. Mimi sina tatizo, lakini wakishafanya hivyo hiki chombo ambacho tunakiunda sasa kile kiwaambie *Okay,* tuambieni sasa wewe fedha hizi ulizipata wapi? Lakini pia lazima kwenye sheria hii tuihusishe *TRA,* kwa sababu tuna *deal* na *income,* hizo *income* lazima watu wazilipie kodi. Haiwezekani tunataka ku-*deal* na mambo halafu tunaiweka *TRA* pembeni, lazima *TRA* wawe *hand and hand* na hii *Finincial Intelligence Unit* tunayoiunda ili kuweza kuwashughulikia hao watu. Pamoja na kulipa faini lazima na kodi ilipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine ambayo mimi najiuliza tuwe na usimamizi thabiti. Wenzangu wameongea kuhusu *Bureau De Change*. Mimi nasema moja ya sehemu katika nchi hii ambako fedha haramu zinapita ni kwenye *Bureau De Change*. Leo unakwenda kwenye *Bureau De Change* unalipa fedha Dar es Salaam hata dola milioni moja, wanakwambia nenda Dubai, utamkuta mtu sehemu fulani atakupa ile fedha. Serikali inayajua haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nasema lazima tutafute pa kuanzia. Kama *Bureau De Change* zinaachwa zinaendelea kama zinavyoendelea leo tutatunga sheria baada ya miaka mitano watabadilisha lugha, tutatunga sheria nyingine. Lakini hizi *crimes* zitaendelea. Kwa hiyo, ndiyo maana narudia kusema pale dhamira ya kweli ni muhimu sana kwenye hili jambo. *In this country* leo kuna watu kabisa na Serikali inawafahamu na watu wanawafahamu kama alivyokuwa anasema Mheshimiwa Amina Mpakanjia, pale kwamba kuna watu wanajulikana wanafanya biashara ya dawa za kulevya hakuna anayewagusa na Sheria zipo. Sasa jamani *are we serious?* Sasa tutakuwa tunakutana kila siku hapa tunatumia mamilioni ya Watanzania hawa tunakaa hapa ndani tunatunga sheria ambazo kesho *enforcement* yake hakuna ya nini sasa tunatunga hizi sheria. *Context* ya Sheria ni nzuri sana. Kwa hiyo, mimi nataka kuomba kweli wenzetu wa Serikali watusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake mwisho wa haya mambo tutaua nchi yetu na tutaua uchumi wetu. Hao watu tusipofanya kazi hii vizuri ndiyo watakaoamua hata nani aingie ndani ya Bunge hili na nani awe kiongozi wa nchi hii kwa sababu wana uwezo wa kifedha na fedha ni chafu. Sasa ni aidha, tuamue kwamba tumewaacha wao sasa ndiyo waendesha hii nchi kwa fedha chafu. Kuna watu kabisa ukim-*trace* ukamwambia niambie hizi fedha zako umezitoa wapi, hana hata ofisi. Lakini hao ndiyo wanaopendwa kwa sababu wana fedha na ndiyo wana-*decide.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachosema wameleta sheria nzuri sana, lakini wasipoisimamia wanapoteza muda kabisa. Tunaongea habari ya *corruption* hapa kwenye huu Muswada nao tunaambiwa moja ya njia ya kupata fedha chafu ni kwenye rushwa. Lakini mimi habari ya rushwa sielewi, tuna *PCB* wanafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kuamini kwamba *PCB* wetu hawajui kazi, *PCB* ya nchi hii inajua kazi kweli kweli, ukiwafuata wakupe *information* wanazo, lakini siyo *decision maker, at the end of the day* watafanya uchunguzi, watampelekea mtu, atawambia weka hapo mezani biashara imekwisha. Matokeo yake tutawafanya watu wawachukie. Ukiwa mtu wa *PCB* ukipita mitaani watu wanakuangalia wanakutemea hata meta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata hii *Fininc**ial Intelligence Unit* tunayounda leo tusipowapa uwezo, wakifanya mambo wakaleta tusipo-*decide* nayo itakuwa *another PCB. It will be non starter.* Kwa hiyo, lazima tuamua kwamba leo tunaanzisha *Unit* ya kuja kusimamia matajiri maana hatuongelei watu wenye fedha ndogo hao, mtu anayeweza ku-*organize crime* kubwa kubwa ni bilionea. Sasa tunawateua hao Watanzania waje kuwasimamia, watafanya kazi nzuri sana ninao uhakika, wakiileta kwenye meza tutoe maamuzi, tusipotoa maamuzi maana yake hao watu tunawaweka kwenye hali mbaya. Matokeo yake nao watakachofanya ni kuungana na hao watu ambao wana-*organize crimes*. Sasa kama unafanya kazi hakuna anayeamua, unafanya nini kesho, tutaandaa Taifa la watu ambao siyo *responsible. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nasema kama walivyozungumza wenzangu hili jambo ni kubwa. Leo Tanzania ndiyo nchi pekee hata nchi zilizoendelea hawafanyi hivyo. Kaka yangu hapa amesema watu wananunua vitu kwa *cash this is indicator* kwamba hapa kuna *corruption ,* ndiyo *indicator* ya kwanza. Mtu unafahamu kabisa kwamba huyu mshahara wake ni milioni moja, lakini kesho anakwenda ananunua kitu cha shilingi milioni 50 analipa *cash.* Hivi hata kodi zenyewe tutazipataje? Maana hata wigo wa kodi lazima tuupanue, tufanye mazingira ya uchumi wetu uingizwe ili watu wa kodi waweze kukusanya kodi. Lakini *at the moment* kama tunatumia *cash cash everywhere,* watu wa kodi watapata fedha wapi? Ng'ombe huyo tutamkamua! Watu wa *TRA* tutawawekea vigezo, tutawambia wakusanye shilingi bilioni 300 kwa mwezi, watafanya kazi watawarudia kuwatoza kodi watu wale wale. Wakati wenye fedha nyingi kodi hawalipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nasema naunga mkono hii sheria, lakini kwa kweli kabisa ili sheria hii iwe na maana sasa tuamue kidogo kuwa *serious,* dhamira ije tuifanyie kazi. Tusipokuwa na dhamira basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na mimi naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**MHE. ANNA M. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafuraha kweli kwa kupata nafasi hii na mimi nichangie kwenye Muswada huu muhimu sana. Kwanza nawashukuru wale wote walioleta Muswada huu hapa Bungeni ili tuujadili na kupitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Muswada huu umekuja wakati muafaka kweli kweli kama walivyosema wenzangu hasa ikizingatiwa kwamba Tanzania sasa hivi inaimarika kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara au fedha haramu katika nchi hii zimeota mizizi na siyo kwa watu maskini Watanzania wenye nchi hii ni watu wachache ambao wana fedha. Mtu ambaye hata muhogo hamiliki mchana, hawezi kufanya biashara ya fedha haramu ambao ndiyo wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi hii sasa hivi biashara zinajaa na zinazidi kila kukicha, kuna *supermarkets* zinafunguliwa kwenye nchi hii na watu kutoka nje hawana idadi, tuna mahoteli Tanzania Zanzibar na huku Tanzania Bara yanaanza kila siku kujengwa makubwa makubwa yapo yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huku kwetu sasa hivi tuna mambo mengi ya haya madini hayajaanza leo. Nchi hii ina madini, dhahabu, vito na vitu vya thamani na hata wanyama, vinaondoka kwenye nchi hii kwenda kuuzwa nchi za nje Watanzania tupo tumetoa macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna biashara ya ajabu ya watoto wetu wa kike wanasafirishwa kupelekwa nchi za nje kwenda kufanyishwa biashara ambazo hata kuzitaja naogopa. Wachache wanajilimbikizia fedha, wao wanapewa visenti viwili, vitatu na hata *passport* wakati mwingine wananyang'anywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wataalam tunawaita *expatriate,* wanakuja katika nchi yetu kufanya kazi na hili tumelipigia kelele sana katika Bunge hili na ni wengi wanaletwa na wengine wanakuja kuuza mtama, njegere na korosho wako hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ma-*expatriate* hawa wanakuja wanajaa hapa nchini kwa kazi ambazo Watanzania wangeweza kuzifanya. Wale matajiri wanaowaajiri wanapata mwanya wa kuweza kusafirisha fedha zetu kupeleka nchi za nje kwa sababu mishahara yao nusu wanalipwa kwa fedha za Tanzania na nusu nyingine wanalipwa kwa fedha za kigeni. Kwa hiyo, hapo hapo na sisi ndiyo tunapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zetu hao ambao wanaleta watalii hapa nchini, siku hizi mtalii analipa fedha huko huko anakotoka, akija hapa yeye anakuja tu kupanda mlima na kuona wanyama, lakini malipo ameshayafanya huko alikotoka. Hizo zote ni biashara za ajabu ajabu, fedha zinaondoka katika nchi hii bila ya kuwa na thamani au bila ya kumsaidia Mtanzania tunaendelea kulia asubuhi na jioni umaskini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Muswada huu umeletwa wakati muafaka kweli kweli na unafaa. Lakini je, tuko tayari kufanya kazi, tuko tayari kukomesha haya mambo, tuko tayari kweli hii sheria ambayo tutaipitisha hapa itakwenda iwe muafaka kwa mwananchi Mtanzania apate anachokitaka kutokana na hii sheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wenzangu walivyozungumza hizi sheria zimetungwa nyingi na zipo, zinafanya kazi. Mtanzania hapati chochote kutokana na sheria hizi, kwa sababu anayefanya haya siyo mimi Anna Komu wala siyo maskini, wanaofanya haya ni wale wenye fedha. Nilizungumza kwenye Bunge hili hili mtu ana biashara ya kuuza kandambili, kesho unamwona anajenga nyumba ya ghorofa sita Kariakoo, unabaki unatoa macho kama mjusi aliyebanwa na mlango. Tunaona

maghorofa hayo yanajengwa, yanapanda kwa biashara ya mtu ya kuuza mikate kweli, kwa biashara ya kuuza kandambili na maplastiki, tunasema tunaleta biashara ya fedha zinatoka nje au fedha haramu tunaleta hizo sheria Bungeni tuzizungumze, tunazipitisha wapi, wakati wao wenyewe au sisi wenyewe hapa ndani tunayaona hayo mambo tunanyamaza kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Amina Mpakanjia, amezungumza hapa sasa hivi nani hajui, mimi nilizungumza hapa kuhusu dawa za kulevya. Leo tunazungumza kweli tukiweka udhati kama Mheshimiwa Rais alivyosema tuseme sasa kwamba tunasimama kidete kupambana kabisa kuzuia dawa za kulevya tutashindwa kupata *hint* ya nani analeta hizo dawa au ni basi tu kama ninavyosema kwamba tutaleta hizi sheria zitakuwa sheria tujaza vitabu vya sheria katika nchi hii mpaka hivyo vitabu tutashindwa kuvibeba. Lakini utekelezaji ni finyu mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli tumeamua kuleta hizi sheria basi tuzitekeleze hizi sheria na wale ambao wanaleta habari kwamba fulani anasafirisha dhahabu tumlinde kwa sheria maalum siyo mimi ninakuja kumwambia hapa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba bwana mimi nimegundua fulani anasafirisha dhahabu hapa, anabeba *briefcase* lakini kwa sababu yeye ni mtu mkubwa, watu hawa-*search briefcase* yake lakini anabeba dhahabu kwenye *briefcase,* Mheshimiwa Anna Komu analeta mdomo. Kesho, anaenda kuwaambia, unajua mama Anna Komu anasema wewe unasafirisha dhahabu, nimeshakuwa adui kwa yule mtu. Kwa hiyo, tulete sheria ya kusema kwamba sheria hii kweli kweli ina meno na itafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha, Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna ndugu zetu wako nchi za nje wanaleta fedha Tanzania kwa wazazi wao au kwa ndugu zao, kuna watu wamekaa hapa wanazisubiri hizo fedha za kigeni kama ni dola au kama ni *pound* wanazipokea hapa kwa sababu hawapaswi kulipa ushuru wa kutuma zile fedha huku. Kwa hiyo, mimi naona hii ndiyo nzuri maana nikituma *pound* 100 silipi chochote, mama yangu ataipokea ile *pound* 100 Tanzania atapewa kamili. Lakini tuone hizi fedha kweli zinaweza zikasafirishwa namna hiyo kweli? Tuwape elimu hao ndugu zetu na tuwape elimu hao watoto waone kwamba fedha ya kigeni ni kitu kizuri na ni kikubwa na kina faida kubwa katika mchepuo wa utajiri katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ndugu zetu mimi nilishaliona katika miaka iliyopita ana mali nje ya nchi, wazee wake walikuwa nje wamekufa, wameacha mali, ile mali anatoka na tajiri hapa nchini anakwenda huko nje kwenda kuiona ile mali, tajiri fedha yake imebaki kule, anakuja Tanzania anamlipa fedha ya Kitanzania na ile mali anachukua kule. Ile fedha ya kigeni hatuipati sisi ambako angemuuzia hapa akampa kwa fedha ya kigeni Tanzania ingepata hiyo fedha. Hayo yote lazima tuyatupia macho na tuyaangalie ndiyo tuseme tunataka kuleta sheria. Kama hatuwezi kufanya hivyo bora tuache tu watu waendelea kutajirika, watu waendelee kula migongoni kwetu, wananchi wa Tanzania waendelea kuumia, wanaendelee kufa maskini na wale wachache walioko juu waendelea kutajirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama tunasema tunataka kuondoa upumbavu wa kusafirisha fedha za kigeni, upumbavu wa kusafirisha madini mpaka wanyama, Tanzania hii walishachukuliwa Twiga, Tembo wakatiwa ndani ya ndege wakapelekwa nje. Yule anaenda kuchuma kule, anaenda kuweka kwenye bustani yake kila siku watu wanaingia anawatoza fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tuko tayari kusafirisha hivi vitu basi tuangalie alicho kipata kule awe anatuletea na sisi *percent* huku siyo kila kitu kiwe kinaishi kwake tu, mpaka tausi wanasafirishwa tuko hapa tunaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema tunataka kuleta sheria. Mimi naiunga mkono hii sheria wala siipingi kwa sababu kwa kweli itasaidia. Lakini natahadharisha kitu kimoja kama tunasema tunaleta sheria maana yake sheria hizi zote zinakuja kuwa msaada kwa wale maskini wananchi wa Tanzania ambao tunakaa kwenye hivi viti tunawapigania. Lakini tusilete sheria ambazo kuna vitu chungu mzima tunaviona kwenye macho yetu na sisi ndiyo wafanyaji wakubwa kama alivyosema Mheshimiwa Amina Mpakanjia. Tulisikia hapa kwamba Mheshimiwa Rais alipelekewa *list* ya watu wauza unga tunasubiri tuone watafanywa nini hao watu. Kwa sababu haya mambo yanasemwa kila siku, utapeleka jina la mtu anayehusika kwenye jambo fulani, utasikia fulani ametolewa jina kwamba anahusika kwenye jambo fulani, unasikia tu *radio* kifua, zinasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa nani anachukuliwa hatua, haonekani anayechukuliwa hatua, yanazimika taratibu yanakwisha. Tujitahidi kuondoa ma-*expatriate* katika nchi yetu. Tujitahidi kuzuia biashara za ajabu ajabu katika nchi yetu, *TPDC* imekufa kabisa, tuna *petrol station* siku hizi za watu zinafunguliwa kila siku kwa majina mapya.

Tuna hakika kwamba hizo fedha ziko hapa au basi, maana yake tunapanua biashara kwa hiyo, nchi yetu inakwenda vizuri. Inakwenda vizuri hii nchi au tunapeleka mifuko ya wengine vizuri sisi tunakwenda kuzimu. Tufanye kazi, tusikubali upumbavu wa kusema kwamba sisi tunapitisha tu sheria hapa halafu basi tukikaa tukiangalia tunasema ahaa, fulani ndiyo mbaya, tunaondoa kiboriti kilichoko kwenye jicho lake wakati humu ndani kuna maboriti yametujaa kwenye macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema tuna hili jambo, tufanye jambo la kweli kweli, tusikubali kutumiwa na nchi nyingine kupewa fedha kuja kufanya kampeni hapa, kuleta matajiri Bungeni, maskini wanabakia wanalia kwa kutumia hizo hizo fedha haramu. Ndugu zetu wa Marekani na Waingereza wanapiga kelele na *Al-Qaeda* kwa sababu inawamaliza na ma-*Al-Qaeda* tunao humu humu. Fedha wanasafirisha nje ya nchi na wengine wanaletewa, nyingine wanapeleka, sisi tumekaa tu, tunasema haya unamwona fulani, basi nitakwenda kumwambia, nikimfuata Mwanasheria Mkuu wa Seriakli sasa hivi nikimwambia, kesho asubuhi ameshampigia simu mama Komu, kaja kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Sheria zitungwe na sheria zifanye kazi na sheria ziwe na meno ili tuone wananchi wanatokana na umaskini. Tusitunge sheria kwa sababu tu tunatunga sheria kufurahisha wengine. Tutunge sheria ambazo kweli zina muafaka na mustakabali wa wananchi wetu katika nchi na watafaidika na sheria ambazo tunazitunga humu ndani. Tusijitie hatuoni tukavaa miwani kumi kumi au hatusikii, tukachakua pamba tukatia masikio halafu tunatunga sheria kesho au kesho kutwa utasikia dawa za kulevya zimeingia, sijui polisi kakutwa kayaiba, sijui nani kachukua yanakwisha hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea jioni, wako wasemaji wachache tu labda niwataje kusudi wawahi kufika nao ni Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Godrefy Zambi, Mheshimiwa Vita Kawawa na wengine ambao wanataka kuongea nafasi bado ipo. *(Makofi)*

Sasa katika dunia ya sasa tunayoendelea nayo hivi sasa kuna kitu kinaitwa *Government Accountability* halafu *Role of Parliament* yaani uwajibikaji wa Serikali lakini wajibu wa Bunge. Kwa hiyo, hayo mnayoyasema mnatunga sheria, lakini ni wajibu wa Wabunge kuwasimamia kama hiyo sheria inafanya kazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nadhani hiyo msilalamike ni kazi yetu kusimamia sheria kama inafanya kazi na wajibu wa Mahakama nao unajulikana. Kwa hiyo, tunafanya kazi kwa upande zote mbili. Kwa hiyo, mimi sipendi Wabunge mlalamike, mnao wajibu wa kufanya kazi ya kuisimamia Serikali kama sheria mlizotunga zinafanya kazi. *(Makofi)*

Lakini nina tangazo nadhani mliambiwa kwamba tulikuwa na shughuli ya kumpongeza Mheshimiwa Dr.William Shija, kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa chombo muhimu sana cha *Commonwealth Parliamentary Association (CPA)* kwamba tungemfanyia shughuli ya kumpongeza kesho tarehe 14 Novemba, 2006. Sasa tumearifiwa kwamba Dr. William Shija ametoa udhuru. Kwa hiyo, hatutakuwa na shughuli kama hiyo labda mpaka Bunge lingine. Kwa hiyo, kama mliambiwa basi hiyo shughuli imeahirishwa. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 12.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge kipindi cha mchana, tulibakiwa na wasemaji watatu. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa William Ngeleja, atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi, halafu Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii kufungua mjadala wa majadiliano ya jioni ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wenzangu awali ya yote kuwapongeza sana watumishi wa Wizara ya Fedha, Kamati zinazohusika pamoja na Serikali kwa ujumla kwa kuleta Muswada huu wakati huu, ni kipindi muafaka na nadhani tunahitaji sheria ya namna hii ili kuimarisha juhudi za Serikali kupambana na matumizi ya fedha haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache ya kusema, lakini pia naomba niseme kabla sijaendelea sana kusema kwamba naunga mkono hoja hii. Pamoja na hayo machache, nitakayaoongelea ni pamoja na yafuatayo:-

Kwanza, ni sehemu ya Katibu wa hii *National Committee*. Ukisoma kifungu cha 8(5) kinampa mamlaka Waziri mhusika kumteua Katibu *(Secretary)* wa hii Kamati kutokana na watumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili mimi naona bado kuna kitu cha kuboresha hapa. Nasema hivyo kwa sababu sifa za watumishi wote kwa mfano wa *FIU* pamoja na *Commissioner* na hata *members* wa hii *National Committee* zimeainishwa bayana na zinaeleweka katika Muswada huu ambao baadae utakuwa sheria. Lakini nafasi nyeti ya Katibu, hatujaainisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nadhani hapa tuboreshe na kwa kuanzia ningependa kupendekeza kwamba kwanza, tuainishe sifa za huyu Katibu zitakuwa za namna gani, kwa sababu tumesema hiki ni kitengo nyeti, kinaanzishwa mahsusi kwa ajili ya shughuli maalum. Kwa hiyo, ni vyema tukafahamu sifa za huyu Katibu zinafana vipi, kwa sababu watumishi wengine zimeshaelezewa na nikadhani pamoja na kwamba sina mashaka na busara itakayotumika kwa Waziri mhusika, lakini kwa nini tusiainishe kwa sababu jukumu lake ni nyeti. Ukiangalia kazi zitakazofanywa na hii *National Committee* ni nzito sana na nadhani kwa sababu Katibu wao ndiye atakuwa mtendaji wa kuratibu shughuli zote ambazo Kamati hii inafanya, basi ni vyema sifa za Katibu ama Karani wa hii *Committee* zifahamike.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine, tufahamu majukumu yake yawe wazi, tusije tukamwachia tu Mheshimiwa Waziri kwa kutumia busara yake. Nadhani ni vyema ile mantiki iliyotumika kuainisha sifa za watumishi wa *FIU,* sifa za hawa *Members* wa *National Committee,* sifa za *Commissioner* zitumike pia kubainisha kwa sababu siyo nafasi ndogo katika utendaji. Tunafahamu kwamba hiki ni kitengo maalum, nadhani pia ingefahamika majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine tufahamu ule mkataba wake wa utumishi utakuwa unakwenda kwa miaka mingapi. Tumeona watumishi wote wa *FIU* watakuwa wanakwenda kwa miaka mitano halafu ajira yao ama utumishi wao unaweza kuhuishwa, unaweza kuongezewa muda. Lakini vipindi vimetengwa. Lakini tumeona wajumbe wa hii *National Committee* wamepewa miaka mitatu mitatu ambapo pia wanaweza kuwa *re-appointed.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikadhani kwamba ni vyema pia hili tuliangalie. Nafasi ya kipindi cha utumishi kwa Katibu ama Karani, iainishwe isije ikawa tu wazi. Kwa hiyo, hayo yakizingatiwa Muswada huu au sheria hii inaweza kuwa imeboreka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo nataka kusema, sina wasiwasi sana na utendaji, lakini sifa za *Commissioner* hapa zimebainishwa, utumishi wake uko wazi. Lakini kipindi cha utumishi wake hakijasemwa! Nilikuwa nadhani kwa sababu tumesema watumishi, yeye ndiye atakuwa Bosi wao, wamepewa miaka miatano na ile *National Committee* imepewa miaka mitatu, pengine tunahitaji maelezo ya ziada kidogo kujua ni kwa nini sasa *Commissioner* katika kitengo hiki nyeti na maalum asingetengewa muda, lakini pia ukawa wazi kwa kuhuishwa kwa kuongezewa muda kama ilivyo kwa watumishi lakini pia kwa wajumbe wa hii *Natioanal Committee*. Hayo nilikuwa nadhani ni mambo ya kuangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine wenzangu wamelichangia asubuhi na wamesisitiza kwamba ni vyema kitengo hiki kikafanya kazi kwa ukaribu sana na vyombo vya habari. Kwa hili, napendekeza kwamba tusisitize, pengine si jambo la kuingiza kwenye sheria kama ilivyo lakini jambo la kuzingatiwa wakati wa utekelezaji. Wakati ajira zitakapokuwa zinaanza kuwa *implemented,* tuone kwamba ni vyema kuwa na Afisa Habari kama ambavyo Sera ya Serikali na tumekuwa tukisisitiza kama Serikali kwa muda mwingi kwamba mambo ambayo yanafanywa na watumishi wa umma, lazima pia yajulikane kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisha kuwa na Afisa Habari katika kitengo hiki maalum, itakuwa ni jambo zuri kwa sababu wananchi watakuwa wanapewa taarifa za mambo ambayo yanafanywa na hiki kitengo. Lakini pia tutawapa nafasi wananchi kuweza kupima na kuona hii sheria mpya na utekelezaji wake imeboresha vipi ufanisi wa kupiga vita matumizi ya fedha haramu. Wananchi watapata nafasi ya kupima kwa sababu watakuwa wanajua tulikotoka na tulipo na tunakoelekea. Nilikuwa nadhani ni jambo pia la kuzingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine limesemwa na Waheshimiwa Wabunge wengine asubuhi waliokuwa wanachangia Muswada huu, ni kuhusu kuimarisha hii sheria na hili tulikuwa tunaongelea jinsi gani kitengo hiki kinaweza kusaidia kuwatambua wahalifu hasa kupitia simu za mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu simtaji kwa jina, lakini amesikika asubuhi alisema na mimi narudia kusema hayo aliyosema asubuhi kwamba juzi tulipokuwa kwenye semina, mojawapo ya maswali yaliyoulizwa au changamoto ambazo zilitolewa kwa watoa mada ilikuwa ni kwa jinsi gani Jeshi la Polisi ama vyombio vya usalama vimejidhatiti kuwatambua wahalifu kupitia simu za mkononi, kwa sababu tunafahamu, simu zetu za Tanzania nyingi hazijasajiliwa, kuwabaini wahalifu kwa simu ambazo zinakuwa hazijasajiliwa, mara nyingi inakuwa ni ngumu sana. Nafahamu mara kadhaa vyombo vyetu vya dola vimekuwa vikifanikiwa, navipongeza kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasema mazingira hayajawa bora sana kuwawezesha kufanikisha shughuli zao kwa ufanisi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. Kwa hiyo, yale ambayo yalisemwa na Waheshimiwa wengine asubuhi kwamba tumarishe tuweke utaratibu wa kusajili simu zetu, nadhani ni jambo jema sasa hivi kwamba tuweke utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishafanya hivyo, tutakuwa tunakisaidia sana kitengo hiki. Nasema hivyo kwa sababu pamoja na kwamba juzi kwenye semina tulijibiwa kwamba Jeshi la Polisi sasa hivi ama vyombo vya usalama vinaweza kubaini hata kama mtu amenunua *line,* akaweka *chip* kwenye simu, akaitupa! Mimi siamini katika hilo, bahati nzuri ama mbaya, nina uzoefu katika masuala ya makampuni ya simu. Kinachofanyika ni kwamba hata nchi nyingine ambacho zinafanya ni kwamba simu zinakuwa zimesajiliwa, kuna zile *element* zake, kumbukumbu sahihi ambazo zinakuwa zimeingia kwenye mtandao tayari na kwa sababu nchi zingine, nchi zilizoendelea zinakuwa zinatumia simu mpya, inakuwa rahisi zile *information* zikishaingia kwenye mtandao, huyu mtu aliyetumia ile simu, hata akitupa ile kadi *(chip)* ambayo ummenunua ile line, kwa sababu taarifa zitakuwepo kwenye ile simu yako, kwenye ile simu yenye, kwenye ile bodi ya simu, utapatikana tu, kwa sababu wataona kuna *information* ambazo wanaweza kuzi-*trace* kwenye mtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini simu zetu sisi nyingi tunazinunua madukani hizi siyo mpya, hazijasajiliwa, hatuna chombo au hatuna utaratibu maalum ambao unalazimisha watumiaji wa simu kuzisajili hizi simu. Sasa hii inaongezea ugumu kwa hawa watendaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana tunasisitiza kwamba ni vyema Serikali ilione hili, ishirikiane na makampuni ya simu. Tunajua hii ni *social responsibility* na makampuni ya simu yanaweza kusema kwamba hili ni jukumu la Serikali. Lakini ni vyema na naomba sana tusisitize kwamba tushirikiane nao, tufikie mahala ambapo tuweke utaratibu mzuri maalum wa kuhakikisha kwamba simu zetu zinasajiliwa. Simu zikishasajiliwa itakuwa ni rahisi kuwatambua, hata ukitupa *chip,* utajulikana tu wewe uko wapi, simu itaonekana unatumia kwa wakati huo ni mnara upi kwa sababu utakuwa nayo. Hilo litalazimisha kama mtu amefanya uhalifu, akinunua *chip,* atupe na simu. Kwa hiyo, itakuwa ni gharama kwao. Lakini kwa sasa hivi ilivyo, ni jambo gumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo ambayo nilikuwa nayo, nilikuwa nataka kuchangia katika huu Muswada, kuboresha kwa hali ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi ili niweze kuchangia mambo machache kuhusu sheria hii ya udhibiti wa biashara ya fedha haramu *(The Anti- Money Laundering Act, 2006).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia na mimi nianze kwa kweli kuipongeza Wizara hususan Waziri pamoja na Manaibu Waziri na wataalam wa Wizara kwa kuleta

Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu. Pengine mimi sitasema wameleta wakati muafaka kwa sababu mara Miswada inapoletwa mbele ya Bunge, tunasema imeletwa wakati muafaka, inawezekana wakati mwingine inaletwa kwa kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningesema kwamba sheria hii ilipaswa kwa kweli iwepo muda mrefu. Hata hivyo, tushukuru kwamba sasa imeletwa mbele ya Bunge na kwa sababu ya umuhimu wake na mimi naomba niseme kabisa mwanzoni kwamba naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nichangie mambo machache. Kuna hasara pia ya kuzungumza wakati wenzako wengi wameshazungumza. Kwa hiyo, mengi tunayozungumza inawezekana yakaonekana kama tunarudia, lakini pia wakati mwingine ni kusisitiza na kuionyesha Serikali kwamba haya mambo yana umuhimu. Wabunge wengi wanapoyazungumza maana yake yanakuwa na umuhimu. Kwa hiyo, ni muhimu au ni vizuri zaidi Serikali ikayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nizungumzie sehemu ya pili ya Muswada, *The Financial Intelligence Unit (FIU)* ambayo pia wenzangu wengi wameizungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba pia niishauri Serikali, kitengo hiki kiwe huru, kiwe kitengo ambacho kinajitegemea. Pamoja na kwamba kwenye Muswada wanasema kwamba itakuwa ni *Extra Ministerial Department,* lakini mimi nadhani bado inapaswa iwe mbali zaidi ili wafanyakazi watakaohusika wawe huru zaidi katika kufanya kazi. Tunasema sababu hizi za msingi kwamba kuna mambo ambayo yanawezekana yakawa *reported* wakati unaohusika, lakini kwa sababu pengine ya urasimu ikachukua muda mrefu hawa wahusika kuweza kufanyia kazi taarifa wanazozipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia alizungumza Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe hapa asubuhi kwamba kutoa taarifa katika nchi hii wakati mwingine viongozi waliopo Serikalini hawazipokei vizuri na wala hawazifanyii kazi sawa sawa na unaweza ukatoa taarifa lakini kwa sababu baadhi ya viongozi wanakuwa na maslahi, inakuwa ni vigumu sana kuzifanyia kazi taarifa hizo. Kwa hiyo, mimi nahofia hiki Kitengo kukiweka chini ya Wizara ya Fedha, bado viongozi wa Wizara wanaweza wenyewe wakati mwingine wakawa kikwazo cha utendaji kazi kwa viongozi watakaokuwa wanaongoza Kitengo hiki. Kwa hiyo, bado kuna umuhimu Kitengo hiki kikawa kinajitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya wakati mwingine ni ya kibinadamu tu. Mwanasayansi mmoja wa Sayansi ya Jamii aliwahi kusema kwamba katika nchi nyingi za Dunia ya tatu au nchi maskini, nyingi mapinduzi ya kijeshi yanatokea kwa sababu tu ya umaskini wa viongozi ambao wanakuja madarakani. Kwa hiyo, wanapokuja madarakani viongozi wengi wa nchi za dunia ya tatu au nchi zinazoendelea au nchi maskini, wengi masuala yao ya msingi yanakuwa ni kuimarisha uchumi wao binafsi. *Primary concern* yao ni uchumi binafsi.

Kwa hiyo, masuala ya uchumi wa Taifa yana-*assume secondary role*. Kwa hiyo, kuna sababu za msingi kwa kweli za kufanya hii *Unit* ikawa inajitegemea ili kuifanya iweze kuwajibika zaidi kuliko kama viongozi hawa watalazimika kuwajibika kwa viongozi wengine tena. Hili linaweza likachelewesha sana utendaji wa kazi wa kitengo chenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna vitengo ambavyo viko huru na vinafanya kazi vizuri na mimi nadhani kama vinaingiliwa, basi inawezekana vinaingiliwa kwa kiwango kidogo sana. Tuna *PCB,* tunaona inafanya kazi vizuri ingawa kuna kasoro za hapa na pale lakini bado wanafanya kazi vizuri. Kuna kitengo cha Usalama wa Taifa, kuna kitengo cha *Human Rights* kinafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, mimi sioni kwa nini kitengo hiki tuseme kwamba lazima kiwe chini ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali kwa kweli kwa sababu naamini Wabunge wengi wamelizungumzia, basi ione umuhimu wa kukifanya hiki kitengo kiwe kitengo kinachojitegemea ili kiweze kufanya kazi zake ambavyo Watanzania wengi wanategemea kifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nilikuwa nafikiri kama kinaweza kikajitegemea viongozi wapewe maelezo kwamba wawe mbali wala wasijihusishe na shughuli za kisiasa kama vile ilivyo kwa vyombo hivi vingine ambavyo nimevitaja hivi punde.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hili, naomba pia nizungumze juu ya makosa yale yalioyoongezwa kwenye *amendment* yanayohusu biashara haramu ya viungo vya binadamu pamoja na uchimbaji wa madini haramu *(Illegal Mining)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara haramu ya viungo vya binadamu imezungumzwa sana nadhani katika kipindi cha miaka miwili, mitatu, kwa *incidences* ambazo nyingine zimetokea Mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, zilivyozungumzwa hizi habari, mimi naomba Serikali ifahamu kwamba watu wengi wanaojihusisha na biashara hii haramu hasa kwa kule Mbeya, wengi wanafanya hivyo kwa sababu ya kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu mambo haya. Wengi wanafanya hivyo kwa sababu za kishirikina.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri ili watu hawa waache kujihusisha na biashara hizi, ni vizuri Serikali ikachukua hatua za kuwaelimisha. Kwa sababu tunaweza tukasema kwamba biashara za viungo vya binadamu, lakini wanaofanya hawajui au hawajawahi kusikia hata Muswada huu wenyewe. Kwa hiyo, inawezekana tusisaidie chochote, tutazungumza lakini itabaki hapa hapa, kwa sababu upeo wa elimu ni mdogo. Haya mambo hawapati nafasi ya kuyasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri Serikali ichukue hatua ili kupeleka elimu kwa hawa watu wanaohusika na biashara hizi ambao mimi naamini wao wanapozifanya hawazifanyi pengine kwa lengo la utajiri sana, lakini kwa

sababu za kishirikina ambazo zina malengo ambayo wakati mwingine huwezi kuzieleza sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumze suala la *Illegal Mining*. Mambo haya mara nyingi yanafanywa na watu ambao kwa kweli ni wakubwa, watu ambao kama wenzangu waliosema wana uwezo wa kifedha, ndio wanaoweza kufanya shughuli hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi hii kumekuwa na tabia kwa kweli ya kulindana sana. Watu wanafanya makosa, makosa yanaeleweka, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya madini ndio tumeona kuna mambo haya yanajitokeza sana, yanajitokeza sana, hatua zinazochukuliwa nyingi hata huwezi kuzieleza. Mikataba mingi ambayo imefanyika mingine siyo mizuri, bado hakuna hatua zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza hivi inawezekana Wabunge wakaonekana wanaichokonoa Serikali, lakini nataka niseme kwamba sisi kama Wabunge, ndio washauri wa Serikali. Tunaishauri Serikali juu ya masuala haya na siyo vinginevyo, tumekuwa tunasema tangu huko nyuma kwamba Serikali ilete Mikataba mbalimbali kwenye Bunge na kama siyo kwenye Bunge basi Kamati za Kisekta ambazo zimeundwa ndani ya Bunge, zipelekewe Mikataba kabla haijatiwa sahihi ili Wabunge waweze kuipitia na kuishauri Serikali. Mimi nadhani tunaweza tukaenda vizuri. *(Makofi)*

Sasa hapa tukisema, wakati mwingine Serikali inasema kwamba Wabunge wanataka kuingilia shughuli za Serikali. Kwa kweli nia ya Wabunge kama ilivyo nia nzuri ya Serikali ni kuitakia nchi hii mema. Mimi nadhani tukiona Mikataba tunaweza tukaishauri Serikali vizuri zaidi na tusipate matatizo ambayo sasa hivi Serikali inapata. Lakini ni baadhi ya viongozi wa Serikali ambao wanasababisha haya, lakini hata wakijulikana, hakuna hatua ambazo zinachukuliwa. Kwa hiyo, viongozi wakikosa, Serikali inachofanya ni kuwahamisha kutoka Wizara moja kwenda nyingine au kutoka Idara moja kwenda nyingine. Hatuwezi kusaidia namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala ambalo alizungumza Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, asubuhi, suala la fedha za mfuko. *Section* ya 24 inazungumza *the Fund of the FIU*, anasema *shall consist of:-* moja, sehemu ya (b) *Grants and Donations lawfully received by the FIU*.

Sasa mimi nikasema, unaposema *grants and donations lawfully received by the FIU,* sasa unaweza ukajiuliza *how lawfully?* Kwa sababu tusipoangalia tunaweza tukakuta huu mfuko ukapata pesa hizo hizo ambazo ni haramu zikaanza kuuendesha Mfuko. Mpaka tutakapokuja kugundua kwamba hizi pesa zilikuwa haramu, tayari hizo pesa zinaweza kuwa zimeshatumika kwenye Mfuko. Watakuja watu na pesa zao kupeleka kwenye Mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumesema *lawfully received.* Unajuaje, kwa sababu unapozipata huwezi ukajua kwamba hizi ni fedha haramu, unaweza ukajua baadae, tutakuja kujilaumu. Watu wengine wanaweza kuwa na uhusiano wa karibu na Mfuko huo kwa sababu tu wanachangia pesa haramu kwa ajili ya uendeshaji wa Mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nataka niishauri Serikali, kuna taasisi nyingine ambazo kwa kweli inapaswa Bunge hili ndilo liidhinishe pesa za kuendesha Mifuko hiyo na si vinginevyo. Kwa hiyo mimi pia ningeshauri kwenye Mfuko huu, hili suala la pesa au michango kutoka maeneo mengine, lisiwepo. Pesa zote zitoke kwenye Mfuko wa Serikali ndizo ziweze kuendesha Mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la mwisho ambalo nataka kuzungumza, ni sehemu ya Sita ya Muswada huu, *Miscellaneous Provisions*. Hili linazungumza *immunity* za viongozi ambao watakuwa kwenye Mfuko. Sehemu hiyo inasema kwamba, viongozi watakaokuwa kwenye Mfuko, hawatashitakiwa kwa makosa ambayo watakuwa wameyafanya bila kukusudia, inawezekana kwa kukusudia lakini wanapotimiza shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nilikuwa nafikiri ili tuwalinde vizuri zaidi na wafanye kazi zao vizuri zaidi, tungesema hata baada ya kumaliza muda wao, ili mradi walifanya kazi zile katika kutimiza matakwa ya sheria, basi hata wakiwa nje ya kazi hiyo, basi pia wasichukuliwe hatua kwa sababu walikuwa wanafanya hivyo kwa maslahi ya nchi, kwa maslahi ya taifa.

Kwa hiyo, isiwe *limited* kwamba tu wanapokuwa madarakani, hawatachukuliwa hatua, lakini pia wakiwa nje ya kazi yaani wakimaliza mikataba yao. Lakini hata kwa wale ambao watakuwa kwenye kazi za mikataba, basi watakapomaliza mikataba yao wawe huru, wala wasije wakashitakiwa kwa sababu watakuwa walifanya hivyo kama nilivyosema wakiwa wanatimiza shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilitaka niseme hayo na narudia tena kusema naunga hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Vita Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, lakini Mheshimiwa Vita Kawawa simuoni.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA.** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe mchango wangu kidogo katika Muswada huu ambao umekuja katika kipindi hiki ambacho dunia inazungumzia pesa haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu mbele yetu ili tuweze kuujadili na hatimaye iwe sheria na itumike katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kwa kutoa mfano mmoja si mzuri kidogo na unasikitisha ili kuonyesha *seriousness* ya Muswada huu. Wakati niko China, nilikuwa ninaishi na kijana mmoja ambaye aliletewa barua kutoka nyumbani yaani nyumbani Tanzania. Aliandikiwa na dada yake, anasema hivi, kaka yangu, nimepata barua kutoka kwa mpwao, akataja nchi moja ya Uarabuni huko, kesho ananyongwa kwa sababu amepatikana na dawa za kulevya. Kwa sababu aliambiwa kabla ya kunyongwa kuwa andika barua peleka nyumbani kwenu uwaeleze kwamba kesho unanyongwa. Tulikuwa pamoja, yule jamaa alilia sana. Lakini baadae alipata habari kwamba ni kweli yule kijana alinyongwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeutoa mfano huo, kuonyesha jinsi gani sisi tunavyofanya masihara katika pesa hizi haramu ambazo sehemu kubwa ni dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka mtaani, ukienda katika maeneo ya Kariakoo, utalia, siyo kusikitika, utalia. Unawakuta vijana mashababi, nguvu kazi ya nchi hii, wanadondokwa na udenda, tayari wameshabugia dawa za kulevya, pesa haramu, inasikitisha. Nenda Zanzibar, hali ndiyo hiyo hiyo, tena kule ndio kunatisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunapitisha Muswada huu hapa, ninachoomba mimi pamoja na vipengele vyote, sijui *clause* gani igeuzwe, iwekewe nini, lazima tuwe *serious* katika kutekeleza ama kutumia sheria hii na tukifanya mchezo, tutamalizika! Pesa za haramu zitaingia na vijana wetu watateketea na nchi hii itakosa nguvu kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi, wananchi wote wa Tanzania tuwe makini, tuamue sasa kwamba tunataka kuiondoa nchi yetu katika dimbwi hili la matatizo ya pesa haramu, dawa za kulevya na mengine yote. Vyombo vya dola, wananchi wenyewe na mimi nataka kukubaliana na Mheshimiwa Godfrey Zambi, hiki kitengo kipewe uhuru kamili, kifanye kazi yake vizuri, kisiingiliwe, ama sivyo hakuna chochote kitakachofanyika. Kazi yetu sisi itakuwa ni kuzungumza vizuri tu kama ninavyozungumza mimi hapa. Lakini tukitoka hapa, mambo ni yale yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaangamia. Pesa haramu zimeingia muda mrefu sana katika nchi hii, wote tunafahamu na ndiyo maana tunasema kwamba huu Muswada umechelewa. Lakini tunashukuru kwamba umeshaletwa mbele yetu. Sasa hapa basi tuongeze kasi ya kuhakikisha kwamba huu Muswada unafanya kazi vizuri. Hii tabia kwamba unakwenda kueleza, nenda mahali fulani utakuta hili, asubuhi unasema ala kumbe wewe ndiye unayenichoma, tuiache. Unapokabidhiwa madaraka haya, unapopewa dhamana hii ya kulinda wananchi, basi uwalinde kweli wananchi. Kama inaonekana kwamba wewe huwezi kuwalinda wananchi, unapenda sana kazi hiyo, basi tuwaondoe, maana nasema hivyo, kila mmoja tunafahamu hapa, maana ili sheria hii iweze kufanya kazi kama nilivyosema mwanzoni, lazima wote sisi tushiriki. Wengine tunawajua, tunakula nao, tunatembea nao na tunawapa sifa kwamba wewe bwana jasiri kweli kweli, wewe tajiri kweli kweli na wakati mwingine tunakwenda kuomba misaada kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaangamia, siyo mchezo. Watu milioni 36 si wengi hata kidogo na kila siku tunaambiwa nguvu kazi inazidi kupungua. Tunapungua kwa UKIMWI, fedha haramu kupitia dawa za kulevya na mengine, tunapungua, malaria yanatuua, kifua kikuu kinatuua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tusifanye mchezo…

**NAIBU SPIKA:** Sema kabisa UKIMWI wewe unaficha Kifua Kikuu.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema na UKIMWI pia. Naomba sana pamoja na vipengele vyote ambavyo vitawekwa lakini watu ambao watahakikisha sheria hii inafanyakazi ni Watanzania wote kwa ujumla wetu. Tusichomane.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ya ile ya Mheshimiwa Amina Chifupa kusema niko tayari kufa, hayuko tayari kufa yule, lakini alichokuwa anasema ni hivi tuna tabia ya kuchomana, ndiyo! Wewe una nia nzuri kabisa ya kuitetea nchi yako, una uzalendo. Sasa hivi kuna utaratibu huu wa mtandao unatumiwa *message* ahsante tutaona, maana yake ni kwamba ameshachomwa tayari. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naomba Serikali, najua Serikali ina pua pana, masikio marefu, mikono mirefu, hawa ambao watakuwa na tabia ya kuwachoma wenzao na wao washughulikiwe. Isipofanya hivyo suala la fedha haramu, dawa za kulevya katika nchi nyingine wana mtandao unaoshindana na Serikali. Nimeona mwenyewe kwa macho yangu, vita vinapiganwa watu wanaoendesha biashara ya fedha haramu, dawa za kulevya kunakuwa na kazi ngumu kweli. Sasa na sisi tusifanye mchezo lazima tuwe *serious*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ya kusema utoe ushahidi wa kutosha, ushahidi wa kutosha wa nini wakati haya mambo yanafahamika dhahiri kabisa. Sheria hii ifanye kazi tu. Kama ingekuwa tunapitisha hapa hapa ikatiwa saini hapa hapa maana leo tutapitisha halafu baadaye tutamwachia Mheshimiwa Rais, anaweka mkwaju pale. Basi kama ingeanza kutumika leo hii tunatoka hapo nje mamia kwa maelfu ya watu wangeshikwa mara moja ndiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza kwa uchungu ningeweza kutoa mifano mingi tu hapa lakini muda hauniruhusu, kuonyesha kwamba hii *money laundering* (fedha haramu), dawa za kulevya tusifanye mchezo hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu kuhusiana na Muswada huu wa kuzuia fedha haramu. Tunaposhughulikia fedha haramu lazima pia tufahamu chanzo

cha upatikanaji wa fedha hizo. Sasa ni nini kinaanza fedha haramu au upatikanaji wa fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu katoa mfano kati ya kuku na yai kinaanza nini. Kuna ugumu sana hapa kufahamu. Lakini fedha haramu ndani yake pia, panapoanzia ni kwenye rushwa. Kwa hiyo, hapa hatuna budi kulisemea suala la rushwa katika Muswada huu wa fedha haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa ni kikwazo kikubwa kwa kukuza uchumi na kufuta umaskini. Rushwa inaumiza maskini na inanyanyua gharama za maisha ya maskini. Fedha za haramu zinapatikana kwenye rushwa kwa njia mbalimbali kama vile kuzitaja *(to name the FIUs, public procurements)* na kadhalika kwa sababu tu ya *interest* za watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nchi yetu bado tuna tatizo katika sheria ya rushwa ambapo ndiko kunakozalishwa fedha haramu. Sisi wote tunafahamu kupiga vita rushwa inachukua muda na inaweza kuwa *risk* kwani watoa rushwa wana kundi lenye nguvu sana. Kama *interest* yao inatishwa wanakuwa hatari sana. Wana mbinu mbalimbali za kuangamiza mpigania haki au mpiga vita rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuacha rushwa kuendelea ni hatari zaidi, inadidimiza maskini, wakati matajiri wanatoa rushwa kwa kuhalalisha vilivyokuwa haramu, maskini inambidi atoe rushwa kwa ajili ya kupata huduma muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa lazima itambulike kwa nchi yetu ni moja ya njia ya kuzalisha fedha haramu. Makampuni mengi wanaamini kutoa rushwa kwao ni gharama ya biashara zao. Wanaamini pia kuwa rushwa inakubalika kwa sababu inaongeza ufanyaji wa biashara zao na mauzo ya *products* zao. Lakini mzigo huu wote anayebeba ni mwananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia taasisi kubwa zinazotegemewa na nchi zinavyoyumba na kuyumbisha uchumi wa nchi yetu. Sababu kubwa ni rushwa na matokeo yake huzaa pesa haramu. Hivyo tunapopitisha Muswada huu tuangalie kwa undani pia sheria za kutekeleza uzuiaji wa uzalishaji wa fedha haramu kupitia kwa njia ya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona niseme hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nichukue nafasi hii ya kukushukuru kwa kunipa nafasi hii fupi na mimi niseme machache kuhusiana na Muswada huu ambao umekuwa ukizungumzwa tangu wakati wa semina na leo umeteremka hapa bondeni ili ujadiliwe na sisi Wabunge na hatimaye kuupitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nina tahayari kidogo kusema kwamba niunge mkono Muswada huu mia kwa mia. Lakini kwa sababu ya jambo lenyewe ni zito

na linaingia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, linataka kuwasaidia vijana wetu na Watanzania kwa ujumla, hali kadhalika linataka kutoa sura mpya kwa Bunge letu Tukufu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, basi sina budi niseme kwamba nami naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya mazungumzo marefu na Waheshimiwa Wabunge waliopita kwa sababu suala la fedha katika Tanzania ni la Muungano, Mheshimiwa Naibu Waziri, ambaye ndiyo muwasilishaji wa Muswada huu katika Bunge hili, baadaye angekuja kunisaidia kunieleza kwamba suala hili kwa upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano kwa maana ya Zanzibar hivi kitengo hiki kitakuwa kinafanyakazi vipi na kitakuwa kinasaidia vipi hatimaye tuondokane na ile lugha kwamba Zanzibar ndiyo mkondo au ndiyo uchochoro au ndiyo *corridor* ya haya mambo ambayo tunataka tuyazuie katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu ikiwa tunazuia upande mmoja, upande mmoja unavuja itakuwa haitusaidii kitu. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, angekuja atusaidie kwa sababu katika pekuapekua yangu siona hapa *unless* kuniambia kwamba kwenye suala hili basi kule Zanzibar kutakuwa na kitengo chake au kutakuwa na jambo jingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nikasema hivyo, nimesema hivyo kwa sababu wanaofanyakazi hizi ni mahodari sana kuangalia wapi ambapo wanaweza wakapenya na hivi sasa hivi ninavyokuambia si hasha ikiwa upande mmoja wa Jamhuri kwa maana ya Zanzibar ikiwa ndiyo inatumika sasa katika suala hili, kwa nini hivi sasa ukiangalia Zanzibar katika ujenzi wa Mahoteli, mahoteli yameshamili sana. Bahati mbaya hoteli zote zilizoko kule zinaitwa *club*. Sasa unapozungumza suala la *club* maana yake hakuna mtu ambaye anaweza akaingilia mambo ya pale ndani ya hoteli ile kwa vitu vinavyofanyika pale. Kuna watu wanasafiri kutoka Roma wanakuja zao Zanzibar katika mahoteli yetu mbalimbali kwa hiyo wanasafiri katika sehemu mbalimbali, wakifika pale wanapojua ni kuingia kwenye hoteli zile wakafanya shughuli zao wiki moja halafu wakaondoka, hakuna taarifa inayojulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kinachoingia pale hakitazamwi. Begi la mtalii huyu linatoka *Kiembesamaki Airport* halisimami mpaka hotelini chumbani, hakuna mtu anayeliangalia. Kama litakuwa linaangaliwa litakuwa linaangaliwa kikakawaida tu. Kweli tunajua pale *airport* kuna mbwa wanaangalia lakini kwa utalaam wa watu hawa katika suala hili la dawa za kulevya mbwa siku hizi wameshakuwa hawawezi tena kunusa dawa za kulevya. Kwa sababu na hawa waliotajwa walishajua kitu gani kinafanya mbwa asiweze kugundua kwa sababu na hawa walitajwa walishajua kitu gani kinafanya mtu asiweze kugundua. Kwa hiyo, inakuwa ni rahisi. Sasa namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri, aje kuniambia kuna utaratibu gani ambao umefanywa ili Zanzibar nayo iingie katika mkondo wa suala hili ili kuzuia Tanzania isiingie katika hatari hiyo kwa pamoja?*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine, wenzangu tangu asubuhi wanazungumzia sana suala la dawa za kulevya na tunazungumza suala hili kwamba ndiyo linasababisha fedha haramu. Mimi nilichotaka kusema Muswada huu umekuja wakati mbaya sana. Kwanza umekuja katika Awamu ya Nne ya Serikali ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania. Lakini umekuja katika Awamu ya Nne, miongoni mwetu tunahusika na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasiwasi sana maana tujitazame maana tumo ndani humo sote hivi hakuna mke anayeshughulika na mambo haya, maana tuulizane wote tupo pamoja hapa, hakuna mke anayeshughulika na mambo haya tunayozungumza ndani Bunge, hakuna mtu mwenye mume anayeshughulika na mambo haya? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuanze kujiuliza sisi wenyewe kwanza halafu tutafute wengine, ndiyo maana nikasema umekuja wakati mbaya sana. Hofu yangu ni kwamba tutafika mahali tushindwe kufanya hii kazi ndiyo wasiwasi wangu. Lakini ningemwomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri, atakapounda kitengo hiki basi awe chekeche zuri mno, maana asije akaunda kitengo hiki ikawa hawa walioundwa ndiyo *number one*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watakaoteuliwa mwenzangu mmoja akasema achaguliwe Katibu awe mzuri, sasa na Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Wizara yake na Serikali, hao watakaochaguliwa, wachaguliwe katika chekeche wachukuliwe kwenye chungio kubwa lakini chungio lenyewe liwe na tundu dogo hawezi kupita hata mbu. Vinginevyo tutakuwa tunachagua kitengo ambacho ndani ya kitengo kuna wenyewe. Kazi itakuwa haifanyiki. Huu ndiyo wasiwasi wangu kwa sababu sasa hivi Tanzania kwa suala hili la madawa ya kulevya tuko vibaya sana. Tumeji-*involve* na mambo haya ndani ya Jamhuri ya Muungano kwa bahati mbaya tuko katika *categories* mbalimbali, maana hapa ndugu yangu mmoja kazungumza kule Zanzibar ukienda utakuta watu wanatoka udenda, mwanaume sababu anatoka udenda lakini sasa tumtazame huyo anayetoka udenda yukoje mtu wa aina gani, yuko *class* gani, maana kuna *class* nane basi hii ya mwisho. Lakini tumtazame huyu *number one* huyu ni nani, ndiyo maana nikasema hatumo humu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nikauliza maswali haya nikasema lazima Mheshimiwa Waziri awe mwangalifu katika suala hili. Hili suala zito. Lakini kwa sababu limeletwa ndani ya Bunge letu Tukufu lazima tulifanyie kazi na hapa ndiyo ninapoiomba Serikali iwe kali mno katika suala hili. Naiomba Serikali iweze kuchukua msimamo kama ilivyochukua msimamo wa majambazi, basi na suala la unga lichukuliwe hatua hiyo hiyo. Tuone vyombo vyote vya dola vinabadilika, vinabadilika kweli kweli, kama vilivyobadilika kweli kweli katika suala la majambazi na katika suala hili basi wasibadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inawezekana narudia tena, tusioneani haya, kama itawezekana tuambizane Waheshimiwa na nyie mno, kama inawezekana Mheshimiwa anasema hapa ingekuwa pana uwezekano hii orodha iliyotoka huko siku nyingine tukifunga Bunge hapa zinaweza zikalia kamba nje hapo, hii ndiyo hatari iliyokuwepo hapa. Sasa hili jambo zito, tunalizungumza lakini zito. Sasa tusilizungumze kwa masihara tuzungumze kikweli kweli. Tunaposoma magazeti mapadri sijui wanatuambia sisi Wabunge basi na nyie Wabunge jitokezeni kabisa maana ilishaandikwa

kwenye magazeti, tujitokeze kabisa tujiweke uwanjani kwamba na sisi tumo iko kwenye magazeti. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa siku nyingine kuna ukweli, siku nyingine hakuna ukweli. Sasa kama uko ukweli basi ndiyo tuanze kufanya *warm up* tufanya *warm up* kweli kweli si jambo dogo hili, si la masihara. Hii sawa sawa na ile lugha tunayoambiwa sasa hivi Waheshimiwa hapa tulipofika katika awamu ya nne sawa sawa na kwamba tunatafuta shuka asubuhi, maana tumelala, tumesahau shuka tunaitafuta asubuhi kumeshakucha. Sasa hii haiwezekani, ni ngumu. Tusitafute shuka asubuhi, ilikuwa tuitafute usiku tulipolala, kumeshakucha sasa hivi hatari kubwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nimeingia wasiwasi na suala hili lakini bado nasema naunga mkono hoja na naiomba Serikali iwe kali na anayehusika ili kufanya vizuri basi asipewe mwanya wa kuweza kupenya ili wengine wasiendelee na suala hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu sana katika kutatua tatizo la fedha haramu. Jambo linaloshangaza sana ni kwamba hakuna *political will* yaani utashi wa kisiasa.

Wakati Tanzania ilipokumbwa na tishio kubwa la ujambazi Serikali ilitamka wazi na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alisema hatuwezi kuwaachia majambazi watambe wanavyotaka na kweli ujambazi ule ukakoma kama upo ni vibaka na wakorofi tu. Sasa kama lile lilifanikiwa hili la fedha haramau (chafu) na dawa za kulevya lina utata gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali kama ina nia njema basi Mheshimiwa Rais wetu atoe tamko tuone kama kweli wazungu wa unga watatamba. Jambo linaloshangaza zaidi ni kuwa wahusika (polisi) wametueleza mbinu zote zinazotumika kupata fedha chafu lakini kuna kigugumizi cha kuwakamata. Sasa nashindwa kuelewa ni kwa kuwa hawana meno ya kuwakamata au tukishapitisha Muswada huu ndio watapata meno? Lakini pia nakubali kuwa wahusika wakuu ni vigogo na hivyo itakuwa vigumu kuwanasa. Kwa kweli kama tunapenda nchi hii, ni vyema basi vigogo hao wajiuzulu ili kazi zifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa kuwa *itelligence* ya Tanzania ni kali na inatisha kama *KBC* ya Urusi au *CIA* ya Marekani lakini tunashindwa kuelewa ni kweli hawawafahamu wahusika au na wao wamenunuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa kuna baadhi ya nchi zinazoongozwa na makundi ya Mafia na wadau wa dawa za kulevya kama ilivyokuwa Afghanistani, Colombia na kaadhalika. Tunataka na Tanzania iwe hivyo? Inavyoelekea tunaenda huko kwa sababu tunashuhudia wafanyabiashara wakichangia mamilioni kwa mabilioni ya fedha kwenye vyama vya siasa. Hivi kwa akili ya kawaida fedha hizi zinatoka wapi na baadaye atapata nini? Haiwezekani mtu achangie hivyo eti kwa kuwa

ni mpenzi tu wa chama, kwanza fedha hizo anazipata wapi na atarudishiwaje? Kama si jambo la siri hata kidogo kuona kampeni za siasa zikigeuzwa mtaji kwa watu na mwananchi yoyote sasa hivi ukimwomba kura anakudai chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inanikumbusha sana jinsi Mwalimu Nyerere alivyokemea na kuwakemea wale waliokuwa na mtazamao huo huo wa rushwa hususan fedha chafu na alisema hawa watu wanaopewa fedha kutoka nje kwa ajili ya uchaguzi watazilipaje? Tunaomba tukumbuke maneno ya Mwalimu Julius Nyerere ili Taifa letu lisiangamie.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni hili la mikataba ya ajabu ajabu mfano wa *IPTL, Richmond* na kadhalika. Nchi imewekwa pabaya lakini wahusika hawafanywi chochote wanaendelea kujinafasi. Kuna suala la majengo ya Serikali yanayouzwa, gharama ya viwanja vya Masaki, Msasani si chini ya milioni 500. Lakini cha ajabu pamoja na nyumba watu wamenunua kwa milioni 50 hadi 100. Hivi huu si ufisadi na ubadhirifu wa mali ya uma? Lakini cha kusikitisha zaidi wanaouziwa wengine wala sio *genuine* na hata kama wanastahili wanawauzia matajiri waziwazi Serikali inatizama kimya. Kwani Serikali haikutambua kuwa itaendelea kuajiri?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wala si ajabu kuona mtoto wa *20 years* anaendesha *Range Rover* ya shilingi 200,000,000/=. Sasa kama mtoto anaendesha hiyo baba na mama wana aina gani na kwa Mtanzania halisi thamani hii inafanana na vipato vyao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii ni nzuri sana lakini taabu kubwa ni utekelezaji wake. Naamini sheria zilizokuwepo zinakidhi ila tu usimamiaji na utekelezaji umekuwa mgumu sana hivyo naamini sheria hii itasaidia sana yale yote yaliyokuwa yamekwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kuhusu watoa taarifa ya wahalifu ni vyema Serikali iwaenzi pale taarifa zinapokuwa za ukweli na pawe na usiri mkubwa kwani watu hawa ni *mafia,* wanaweza hata kuua ikibidi, hivyo Serikali ihakikishe kuna *a lot of confidentiallity,* vinginevyo itakuwa kutwanga maji kwenye kinu na hivyo wataendelea kutamba. Nakushukuru sana.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakupongeza wewe kwa kuongoza Bunge leo na kusimamia vizuri pia kutoa nafasi kwa wachangiaji wa maneno na wengine sisi tunaochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni mzuri kuchangiwa na kwa upande wangu naomba Serikali iwe na uwezo mkubwa kuangalia kuhusu fedha haramu kwani ni mtandao mkubwa na hawana huruma kwa mtu au Serikali kwa hiyo na Serikali nayo iwe kali kwa vitendo ili kudhibiti mtandao wa fedha haramu ndani ya Tanzania yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha haramu na mtandao huu utawaudhi, bado kwao hawaufahamu. Naomba sana wapewe mafunzo (semina) kila Mkoa au Wilaya ili kuepukana na vitendo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi la polisi na vyombo vingine vinavyohusika wapewe uwezo na zana za kutendea kazi na vifaa vingine. Kutoa pongezi kwa zawadi kwa wale ambao watafanya kazi nzuri na kwa kufanikisha kuwakamata au kutoa habari *(information)* ya biashara haramu au fedha haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pawe na Sheria ya kumlinda mtu anayetoa habari, kwa sasa bado sheria ina upungufu. Vitendo vingi vinaendelea kwa sababu watu kuogopa na kujilinda kwa usalama wao. Bado naomba Serikali iwe na mikakati zaidi isiwe kama msemo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Magogoni na kwa niaba yangu naomba kuunga mkono Muswada huu upitishwe. Ahsante sana.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1983/1984 kulifanyika operesheni ya kuwasaka wahujumu uchumi. Baadhi ya watu waliogundulika kuhodhi mali nyingi Pamoja na akiba kubwa ya fedha kwenye mabenki, mali na fedha nyingine zilizuiliwa zisichukuliwe kutoka kwenye benki. Baadhi ya majengo na mali vilitaifishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza baadhi ya majengo yaliyokuwa yametaifishwa yalirejeshwa kwao. Wengine walilipwa gharama ya mali yao iliyokuwa imetaifishwa. Je, Muswada huu hauna maono kama ule wa operesheni ya wahujumu uchumi wa mwaka 1983/1984?

Je, tamko la sisi Waheshimiwa Wabunge kuhusu mali tulizo nazo linasaidia kudhibiti uhalifu wa aina hii unaoainishwa kwenye Muswada huu? Naunga mkono hoja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga Muswada huu. Kwanza nakupongeza Mheshimiwa Waziri kwa Muswada huu na ni mzuri sana kuhusu mambo mengi yanatokea sehemu nyingi sana kuhusu fedha hizi haramu wananchi wanyonge wanakandamizwa kuhusu hizo fedha haramu na ofisi nyingi wanapenda kutumia fedha ndipo atakufanyia kazi kwa mfano Mahakama, Ofisi ya Ardhi, Polisi, Hospitali, kipindi cha kampeni fedha nyingi zimetumika hizo na hii inasababishwa na sisi wenyewe kuwalea, anakamatwa siku m oja anaishia kutoka nje, akitoka Serikali inamhamisha wanampeleka sehemu nyingine je, kumhamisha kutazuia kutumia hizo fedha haramu? Tunaomba mtu yeyote akibainika amekamatwa achukuliwe hatua sio kumlea. Hivyo inasababisha huo mchezo kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine eti ukishamwona unaripoti ukisha ripoti kesho akatoka anataka kukuua au akuumize. Mara nyingi watendaji wa Mahakama na Polisi, wananchi wanawakamata yanaishia mezani. Je, Serikali inayo mikakati ya kulinda watu hao? Majambazi kama huko polisi wanakamatwa na silaha siku mbili

unamkuta ametoka nje hivyo inatuaibisha sisi Watanzania. Naomba hili jambo litolewe macho. Naomba kuunga mkono hoja hii ahsante.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi nchi pokezi *(recipient countries)* za fedha haramu huwa zinahusika baada ya hatua ya *lazering step* yaani baada ya hatua ya *intergration.*

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana ikawa vigumu kwa nchi hizo kubaini moja kwa moja kama fedha hizo chanzo chake ni biashara haramu ya dawa za kulevya au biashara nyingine zozote haramu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nchi haziko makini zinaweza pia chini ya udhibiti wa fedha haramu nchi hizo zikarudisha fedha halali ambazo zingeweza kuchangia kwa kiwango kikubwa kukuza uchumi wa nchi husika na hivyo kupoteza wawekezaji. Serikali na vyombo husika lazima viwe makini sana katika hatua hii ya tatu ili iweze kubaini kwa uhakika *(beyond reasonable doubt)* kwamba fedha hizo ni haramu kweli.

Kuhusu Benki Kuu, kwa kutumia *Circular No. 8* wasiwe *speculative* kwa raia wa Tanzania ambao wana nia ya kuwekeza katika Sekta hii ya fedha. Maswali kama huyu amepata wapi fedha za kuanzisha Benki yakimfikia mlengwa yanakatisha tamaa kwa yeyote mwenye nia ya kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo, inaonekana ni rahisi mgeni kutoka nje kuaminika haraka na chombo hiki kuliko mzalendo wa nchi hii. Inawezekana hao hao wageni wakawa na vyanzo haramu na wakaja hapa kwa sababu nchi hii ni ya amani kwa hiyo ni *condusive* kwa kufanya biashara ya fedha. Kwa nini kuwa *doubt* Watanzania wenzao?

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya udhibiti wa biashara ya fedha haramu ya mwaka 2006, naunga Muswada mkono kwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hakutakuwa na mkakati thabiti wa kudhibiti maovu yatendekayo na uvunjaji wa sheria hii, athari zifuatazo zitajitokeza:-

(a) Kukamatwa na asiyehusika;

(b) Kuvunja nguvu kazi Kitaifa;

(c) Kijenga moyo wa utapeli;

(d) Ujambazi kukithiri kuwa ana pesa; na

(e) Kuua kizazi imara endelevu Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa lifanyeje! Kutoa fungu nono kwa atakayetoa taarifa kwa siri sana, katika akaunti anayetoa taarifa, baada ya uchunguzi yakinifu kuwa katoa taarifa sahihi kwa taifa na taifa kukiri kuwa taarifa hiyo ilikuwa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, siri kubwa itunzwe na Ofisi husika patakapotolewa taarifa. Kama atatoka nje ya nchi na atangazwe mara moja ili kukanusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu nadhani kunahitajika elimu ya kuwaelimisha wananchi juu ya athari au madhara yanayojitokeza kutokana na vitendo hivi haramau. Biashara ya ngozi za binadamu, vyombo vya habari wawezeshwe Kitaifa ili hili walielimishe kupitia vyombo vyao kulikemea itasaidia.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa kuleta Bungeni Muswada wa fedha haramu kwa kweli ni wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kuchangia hoja hii kwa kuwachambua wafanyabiashara wakubwa kwa kukumbatiwa na viongozi wakubwa ambao unapelekea nchi kupoteza vyanzo vingi vya mapato kwa kukubali kununuliwa na wafanyabiashara ili mambo yao yapite na kusaini mikataba mibovu ili mradi tu wanapata rushwa itayowapatia utajiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mfanyabiashara/wafanyabiashara wakubwa wanaingiza bidhaa *(import/export)* na kusafirisha bidhaa, lakini ni hao hao wanafanya shughuli za uwakala wa mzigo *(clearing and forwarding of goods)* kwa kweli kwa kupitia mianya hii wanainyima nchi kupata mapato makubwa na kupindisha sheria kwani huyu mfanyabiashara ni mbabaishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali kuwa wafanyabiashara wanaojishughulisha na biashara ya uingizaji wa bidhaa wasiruhusiwe kuwa mawakala wa uingizaji na usafirishaji wa mizigo. Kwa hayo, napenda kuunga mkono hoja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli uhalifu wa Kimataifa umeongezeka dunia nzima umehamia pia maeneo matulivu kama Tanzania, mfano ni wizi kwenye mabenki, wizi wa mabilioni ndani ya mabenki huongeza kwa haraka mzunguko wa fedha haramu ndani ya nchi na huongeza kwa haraka mfumuko wa bei yaani *inflation.* Fedha haramu zinapitia *Bureau De Change* zilizopo hapa nchini. Fedha haramu zipo sana kwenye maeneo hasa ya ujenzi wa *apartments.*

Mheshimiwa Naibu Spika, *apartments* zimefumka kila upande Dar es Salaam na zinamilikiwa na kikundi kidogo sana cha Watanzania. Mimi nahisi kuna fedha haramu hapa. Mtu ananunua nyumba ya Serikali milioni 40 badala ya milioni 300 lakini baada ya muda anajenga nyumba hapo ya milioni 500. Je, hii siyo fedha haramu?

**NAIBU SPIKA:** Wale waliokuwa wameomba kuchangia wote wamepata nafasi na wote mnataona kwamba mwingine kasema iwe Mbunge, awe mume wangu, awe mke

wake, wote washughulikiwa na nyie wengine mnasema wapo. Ni kweli usimuonyesha mwenzio kidole kabla ya kujisafisha mwenyewe. Kwa hiyo, nadhani *whether* Muswada utasainiwa kesho, keshokutwa Serikali ipo itafanyakazi yake.

Kwa hiyo, nadhani hii ari, msiseme kwa utani maana yake hii kama ni vita kwa wote basi, kwa hiyo, mkubali hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo nitamuita mtoa hoja aweze kujibu hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, sasa naomba kutoa hoja kwa kujibu yale yaliyojitokeza katika Bunge lako Tukufu. Awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale waliochangia kwa maandishi. Naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge hawa kwa majina kama ifuatavyo:-

Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Adam Malima, Mbunge wa Mkuranga na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa William Ngeleja, Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo na mwisho Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mbunge wa Kilombero, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mbunge wa Songwe, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mbunge wa Vunjo, Mheshimiwa Maria Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi pamoja na Kambi ya Upinzani, kwa kuunga mkono Muswada. Ninaahidi kwamba Serikali itayafanyia kazi ushauri na mawazo mazuri yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi pamoja na Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nianze kujibu hoja mbalimbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo, kulikuwa na hoja kwamba kipindi

kilichowekwa kwa kutoa taarifa za mashaka kuhusu fedha haramu ndani ya kipindi cha saa 24 ni muda mfupi kutokana na hali halisi ya mawasiliano. Pamoja na kwamba kifungu cha 17 cha sheria kimetoa ndani ya saa 24 kwa mtoa taarifa kutoa taarifa kwa *Financial Intelligence Unit* kuhusu taarifa yenye mashaka ya fedha haramu kifungu hicho hicho kinatoa fursa kwa mtoa taarifa kutafakari kabla ya kutoa taarifa husika ndani ya saa 24. Maneno *after forming that suspicion and wherever possible* yanamwezesha mtoa taarifa kutafakari kwanza na kujenga hisia ya mashaka kabla ya kutoa taarifa ndani ya saa 24. Hivyo basi, kitendo cha kutoa taarifa ndani ya saa 24 kitafanyika baada ya mtoa taarifa kutafakari kwanza. Kwa hiyo, hizo saa 24 anazo yeye.

Aidha, kwa upande wa taasisi, Serikali inaamini taasisi nyingi zina mfumo wa mawasiliano na kuwezesha kutolewa kwa kutolewa kwa taarifa za papo kwa papo ikiwemo mabenki na taasisi za kifedha kama ilivyotafsiri *reporting person* ni nani ikiwa ni taasisi, ikiwa ni mtu binafsi yote anayo fursa ya kufanya hivyo. Taasisi kama nilivyosema hapo wanayo njia kuwasiliana popote pale ikiwa ni benki ikiwa ni *TRA* na mengine mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba motisha itolewe kwa wafanyakazi wa *FIU* na kwa watoa taarifa. Kimsingi Serikali inakubaliana na hoja ya wafanyakazi wa *FIU* kupewa motisha ya kimaslahi kwa kuzingatia unyeti wa kazi zao. Serikali italifanyia kazi suala hili kama ilivyo kwa vyombo vingine vya aina hii na kuhusu motisha kwa watoa taarifa utaratibu utawekwa ili watoa taarifa waweze kupata motisha kutegemea na unyeti kwa taarifa zitakazotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja Serikali kuitunga sheria ya kuwalinda watoa taarifa. Serikali imepokea ushauri wa kuwa na sheria mahsusi wa kulinda watoa taarifa kama pale tulipokubali katika Kamati ya Fedha na Uchumi na kama vile tulivyokubaliana wakati tunazungumza katika semina siku ya Jumamosi. Hata hivyo, mkakati huu unahitaji maandalizi ya sheria, miundombinu na kadhalika. Aidha, kwa kuanzia chini ya marekebisho yaliyofanywa katika kifungu cha 22 kama mlivyotushauri katika Kamati ya Fedha na Uchumi na katika semina kifungu cha 22 cha sheria, mashahidi watakaotoa ushahidi unaohusiana na makosa haya ya fedha haramu yaani *informers* na watoa taarifa watapewa kinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nne kwa ujumla iliyojitokeza nyingine ni kwa ushirikiano kati ya Serikali na wadau katika utekelezaji wa sheria hii. Serikali imepokea ushauri huu kuhusu umuhimu wa kushirikisha wadau katika utekelezaji wa sheria hii ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha watendaji wa *FIU,* wana jamii wana harakati na pia kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa sheria hii. *(Makofi)*

Pia kuna hoja kwamba watoa taarifa kutumia vibaya mamlaka yao kwa kuwakomoa watu. Kifungu cha 4 cha sheria kimeweka bayana majukumu ya *FIU* ikiwa ni pamoja na kupokea taarifa na kuzifanyia uchunguzi wa kiintelejensia kabla ya kuwasilisha taarifa kwa vyombo husika kwa hatua zaidi.

Hivyo basi, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba taarifa zitakazowasilishwa *FIU* zitafanyiwa uchambuzi wa kina na kwa intelejensia kabla ya vyombo husika kuchukua hatua. Kama mliona kwamba hiyo *FIU* yenyewe ina watu ambao ma-*TTPC Plenary,* hao ndiyo waliohusika katika vyombo mbalimbali kutayarisha Muswada huu na hao wote ndiyo watahusika katika chombo hiki cha *Financial Intelligence* kutokana na sekta hizo ambazo zimehusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu haki ya usiri kwa wateja kuhusiana na masuala ya biashara ya fedha haramu, sheria imezingatia haki ya usiri kwa wateja. Sheria kama ilivyo inaondoa haki ya usiri kwa mtu au taasisi, pale tu mtu huyo au taasisi husika itakapobainika kushukiwa kwamba inahusika na suala la fedha haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeainisha bayana katika ibara ya 30 kwamba maslahi ya Taifa yatazingatiwa kwanza kabla ya maslahi binafsi kama alivyotukumbusha Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, wakati anachangia katika hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya dhamira ya Serikali kutekeleza sheria hii, kwa kuwasilisha Muswada huu Bungeni Serikali imedhamiria kutekeleza sheria hii ipasavyo. Aidha, kama Mheshimiwa Naibu Spika, alivyoelezea, Bunge pia lina wajibu wa kusimamia na kuhakikisha utekelezaji wa sheria hii, hivyo ni matumaini ya Serikali kwamba Waheshimiwa Wabunge, mtakuwa mabalozi wa kuhakikisha kwamba sheria hii inatekelezwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kuhusu kipindi cha ajira cha miaka mitano kwa wafanyakazi wa *FIU* ni kifupi. Kifungu cha 7 (3) cha Muswada kimefanyiwa marekebisho kutokana na ushauri wenu katika Jedwali la marekebisho ambapo wafanyakazi wa *FIU* wataajiriwa kwa kipindi cha miaka mitano na wale watakaoonyesha ufanisi mzuri wanaweza kuteuliwa kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kuhusu utaratibu gani utatumika kuhakikisha watumishi *FIU* hawafichi mali zao kupitia watoto, mke au ndugu zao. Utaratibu wa kuhakiki mali za watumishi wa *FIU* utakuwa kama ilivyo hivi sasa katika Sheria inayosimamia maadili kwa watumishi wa umma ambapo mali za wafanyakazi wa *FIU* pamoja na ndugu wa karibu kama mke, mtoto, nazo zitahakikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba sheria isitumike kukimbiza wawekezaji wa nje na pia kuwatisha wawekezaji halali wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaafiki umuhimu kwa kuoanisha utekelezaji wa Sheria hii na taratibu za uwekezaji zinazosimamiwa na *TIC* na vyombo vingine ili kuhakikisha kuwa wawekezaji halali wa nje na ndani hawabughudhiwi. Aidha, wawekezaji wengi ndani ya nchi wanapendelea mazingira ya uwekezaji ambayo yanafuata taratibu bora za umilikaji wa mali, utawala bora na udhibiti wa mabenki dhidi ya fedha haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kuwepo utaratibu wa usajili wa namba za simu za mkononi. Serikali imepokea ushauri huu wa Waheshimiwa Wabunge kuhusu suala hili kama njia mojawapo ya udhibiti wa utambulisho wa wateja. Naamini Wizara husika inalichukuwa hilo na hivyo litafanyiwa kazi na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwamba *FIU* kuwa chini ya Wizara ya Usalama wa Raia badala ya Idara chini ya Wizara ya Fedha, Kifungu cha 4 cha Sheria kimetamka bayana kwamba *FIU* itakuwa ni chombo kinachojitegemea *(autonomacy)* chini ya Wizara ya Fedha. Chombo hiki siyo lazima kiwe na Ofisi ndani ya Wizara ya Fedha, kitakuwa na *independent identity* ambayo bado Wizara ya Fedha itawajibika kusimamia ili kukiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kwa mfano masuala ya bajeti ya *FIU.* Aidha, kimeweka bayana kwamba wafanyakazi wa *FIU* watatokana na wafanyakazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na wachunguzi katika nyanja mbalimbali ambazo taarifa zitapokelewa. Kulikuwa na hoja ya usimamizi wa maduka ya fedha *(Bureau De Change).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 maduka haya yanapaswa kutoa huduma za papo kwa papo za kununua na kuuza fedha. Maduka ya fedha hayaruhusiwi kwa mujibu wa taratibu kupokea na kutuma fedha nje ya nchi. Hii ni kazi ya mabenki na taasisi za fedha. Benki Kuu huyasimamia maduka haya kwa kupokea taarifa zake *(office suverelence)* mara kwa mara na kuyafanyia kazi na kuyafanyia uchaguzi *(all site inspection)* kila mwaka. Pia hufanya *target inspection* pahali panapokuwa na taarifa za ukiukaji wa taratibu. Maduka ambayo hayafuati taratibu hutozwa faini na mengine kufutiwa leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba Waandishi wa Habari kuwa sehemu ya watoa taarifa na kutoa mafunzo kwa Waandishi wa Habari kuhusu dhana ya fedha haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaamini kwamba Waandishi wa Habari ni kioo cha jamii na kwamba umma wa Tanzania utaelimishwa kupitia kwa wanahabari. Hivyo basi Serikali itaandaa utaratibu wa kuwaelimisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na waandishi wa habari kuhusu dhana hii ya biashara ya fedha haramu. Aidha, kuhusu waandishi wa habari kutambuliwa kama watoa taarifa. Sheria imempa mamlaka Waziri wa Fedha kuongeza orodha ya watoa taarifa pale atakapoona inafaa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya kutaifisha mali za wahalifu zitokanazo na fedha haramu. Suala la utaifishaji wa mali za wahalifu zinazotokana na makosa mbalimbali ikiwa ni pamoja na biashara ya fedha haramu limebainishwa katika vifungu vya Sheria ya *Proceeds of Crime Act,* Sura Namba 256. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na wasiwasi mkubwa umejitokeza wa kwa nini Serikali haiwachukulii hatua watuhumiwa wa biashara ya dawa za kulevya. Ni kweli kwamba tatizo la dawa za kulevya lipo. Serikali imelivalia njuga tatizo hilo na limechukua hatua kadhaa katika kushughulikia suala hili kama ifuatavyo:-

Mmejionea wenyewe katika semina siku ya Jumamosi, hatua mbalimbali zinazochukuliwa katika kufuatilia jambo hili na akakuonyesheni mbinu mbalimbali za kutafuta hizi dawa za kulevya. Lakini kwa faida yenu Waheshimiwa Wabunge nitatoa baadhi ya takwimu ambazo mtajua kwamba Serikali imekuwa ikichukua hatua katika jambo hili. Naanzia mwaka 2003, jumla ya watuhumiwa 293 walikamatwa na jumla ya kilo 5.8 za *heroine* na *Cocaine,* watuhumiwa 5,399 walikamatwa na kilo 733,200.1 na watuhumiwa 410 walikamatwa na kilo 12,002.63 za mirungi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2004 jumla ya watuhumiwa 355 walikamatwa na kilo 14.6 za dawa za *heroine, cocaine, anvetamine* na *mandrax.* Watuhumiwa 3,749 walikamatwa na kilo 964,070.38 za bangi na watuhumiwa 265 walikamatwa na kilo 9,650.98 za mirungi. Mwaka 2005 jumla ya watuhumiwa 387 walikamatwa na kilo 85.943 za dawa aina ya *heroine, coceine* na hashishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watuhumiwa 3,929 walikamatwa wakiwa na kilo 122,534.6 za bangi na watuhumiwa 2,689 walikamatwa na kilo 1,122 za mirungi. Kuanzia Januari hadi Septemba, 2006 jumla ya watuhumiwa 21 wamekamatwa na kilo 28.2 za *coceine, heroine* na *mandrax.* Watuhumiwa 3,583 walikamatwa na kilo 1,070,727 za bangi na watuhumiwa 364 walikamatwa na kilo 1,534.74 za mirungi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya sheria hii kupitishwa itakuwa ni chachu ya kushughulikia tatizo ya dawa za kulevya nchini. Tunaomba wananchi na Waheshimiwa Wabunge kama watakavyoonyesha watoe ushirikiano kwenye vyombo vya dola ili kukabiliana na tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, alikuwa na wasi wasi kwamba upande wa pili wa Tanzania yaani Zanzibar watahusishwaje katika chombo hiki. Tukiangalia ukurasa wa 52 wa hii *FIU* utakuta kwamba kuna hii *FIU* katika Wajumbe wake kuna *representantive* wa *Ministry of Finance* wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kuna *representatives* kutoka *Attorney General Chamber's Zanzibar* na tena kama ilivyopendekezwa katika Kamati ya Fedha na Uchumi kwamba upande wa *DCI,* Usalama wa Raia afadhali vile vile awepo mwakilishi kutoka Usalama wa Raia wa Zanzibar, hivyo kazi hii itafanywa kwa ushirikiano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa kuwa wana chombo kimoja cha kufanya kazi hii na kama mbwa sasa hafai, tumeambiwa panya wapo, tutajaribu panya buku. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la juu ya watu wanaowachomea wenzao *(tipping off)* kwa mtu yeyote asiyepasa kufahamu kwamba kuna tuhuma dhidi yake. Kifungu chini ya Sheria ambacho kimefanyiwa marekebisho na hata utaona kwamba faini hapo imezidishwa kutoka shilingi milioni 500 kwa Taasisi hadi milioni moja na vile vile kifungo kisichozidi miaka 10 lakini kisichopungua miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna mchango ulivyokwenda ni dhahiri kwamba Waheshimiwa Wabunge wanaunga mkono Muswada huu na kwamba wamesisitiza tu kwamba Sheria hii ichukue mkondo wake na kusiwe na upendeleo nao na

yote waliyoyapendekeza nimehakikishia kwamba tumeyaingiza katika Muswada huu kama ilivyopendekezwa katika Kamati ya Fedha na Uchumi na pia kama walivyopendekeza katika Semina tuliyoifanya siku ya Jumamosi tarehe 11 Novemba, 2006 .

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu wa Mwaka 2006 *(The Anti-Money Laundering Bill, 2006)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

Kifungu cha 3 katika *Section* ya *Predicate Offences* wakati Kambi ya Upinzani inachangia, inazungumzia hayo mambo. Kitu ambacho mimi kidogo kinanitia wasiwasi, Mheshimiwa Waziri ajaribu kunipa maelezo ni *issue* ya *illegal fishing, illegal mining.* Ni wakati gani wale watu wanaovua wadogo wadogo wanakuwa *illegal fishers* au wachimbaji wadogo wadogo wanakuwa *illegal miners* ambao wanaharibu mazingira kwa kuchunga wanakuwa pia ni wahalifu *under environmental crimes*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hili kwa sababu uzoefu kwa mfano, Sheria ya *Organised Crime* na *Subotage on Economics,* mara nyingine sheria hii imetumika kama vile kuwaonea watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa hali kama hii ambapo hakuna tafsiri iliyo kamili kisheria ya mchimbaji au ya mvuvi au ya mchungaji na adhabu hizi za miaka 10 tutajaza jela ngapi katika nchi yetu. Mimi nashauri vitu kama hivi vinahitaji kuwekewa tafsiri iliyo sahihi kabisa. La sivyo tunaifanya Sheria ambayo ni *very serious.* Sheria ambayo wote tunaiunga mkono inakuwa ina-*deal* na *tributaries* vitu vidogo vidogo na inaumiza watu ambao kusema kweli hawa siyo *target* au makusudi ya Sheria hii. *(Makofi)*

Mimi nafikiri makusudi ya Sheria hii ni kuwakamata watu waliobobea katika mambo haya na siyo mvuvi mdogo mdogo. Ningependa maelezo kwa hilo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa madhumuni ya Muswada huu na pale tuliposhauriwa na wanakamati wenyewe, *illegal fishing* au *pouching* haikukusudiwa hawa wavuvi wadogo wadogo na wavuvi wadogo wadogo, mara nyingi hawana kwamba wao wana mapesa mengi ya kwenda kufanya mambo ya *money laundering*. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mimi naona siridhiki na jibu hilo. Mheshimiwa Waziri akiniambia katika *Regulations* ataweka *limitation* au *clarification* hili naweza nikakubali. Lakini baada hii Sheria kuondoka katika Bunge hili ikaenda kwa wenyewe ambao ni mapolisi wengi wala hawajaenda hata shule ya Sheria. Watakaposoma jambo hili na wewe Mheshimiwa Waziri hatujui utakuwa wapi, labda utakuwa *President, no body knows,* hautaweza kufikiwa ya kuweza kuulizwa Mheshimiwa Waziri ulipokuwa unasema *a small fisherman* hana hela nyingi. Maana yake ni nini. *I think* ukinieleza kwamba utaweka *limitation* katika *regulations,* hilo mimi naweza kukubali kwamba je, kuna kinga kwa watu hawa wadogo wadogo?

**MWENYEKITI:** Akiwa *President* ndiyo mambo yatakuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria itakuwa na *regulations* ambayo Waziri atakuwa anazipitia mara kwa mara na ndiyo maana hata pale tuliposema fedha kiasi gani, zitolewe kama ni zawadi ya mtu motisha au alipwe kiasi gani. Kwa sababu *time of scale* zina-*change* kila tunavyokwenda. Kwa hivyo na hiyo itakuwa inarekebishwa kila wakati unavyoona kwamba hapa lazima ifanywe hivi, kutakuwa na *regulations.(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 10
Kifungu cha 11

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 14

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 15

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 15(a) nilikuwa naomba ufafanuzi tu kwamba katika mabenki mengine imetokea kama ni kawaida benki kufungua akaunti kwa jina la mtu na wakati mwingine mtu maarufu. Halafu pesa zikaingia huko, zikatumika kisha inapojulikana hizi pesa mbona ziko huku anaulizwa yule anayehusika anasema mimi sihusiki na kumbe akaunti ile ipo pale kwenye ile benki. *(Makofi)*

Sasa kwa kuwa tunapitisha Sheria hii matukio ya namna hii tutayafanyaje kama benki husika itakuwa imefungua akaunti, na akaunti kweli ipo. Tunafanya nini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Kwa ruhusa yako Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, wewe ulikuwa *BOT* unajua kwamba katika *bank supervision* zile *transactions* zina tofauti kidogo tu lazima wachukuliwe hatua zinazohusika.

Kwa hiyo, hata hao ikiwa kama imekuwa ni *fraud* benki itachukua, *BOT* itachukua hatua inazohitaji kwa kufuata kanuni walizojiwekea kwenye *bank supervision. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Au Mheshimiwa Mbunge ulikuwa na ushauri wowote?

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwenye eneo kama hili tungekuwa wazi kabisa kwamba benki yoyote, kwangu mimi kwa mfano uliotoa ni benki inayoaminika kusaidia kutenda mabaya.

Sasa benki inapokuwa imeaminika kisha ndani mle ikawa ndiyo sababu ya kufungua akaunti ambazo zinatumika kufanya mambo mabaya, mimi nadhani tungekuwa

wakali juu ya hili tukawa *very specific* kwamba benki zisiruhusiwe kwa namna yoyote ku-*facilitate transactions* ambazo ni chafu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, maana ametoa ushauri wake yeye.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo anayoyasema Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, kuna *two definitions* ya *bank, a small letter* na *BANK in capital letter.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BANK in capital letter* tumeainisha makusudi kwa sababu hizi Sheria ziko katika *Banking and Financial Institution Act* na tulifanya hivyo makusudi kwamba *any time* ikitokea makosa kama hayo *go back to the bank with capital letter BOT* na *bank in small letter* ni hizi nyingine benki nyingine *STANBIC* au *Stadard Chartered, I think that shall be. (Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 21

*(Kifungu kilichootajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 22

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu wa Mwaka 2006**
***(The Anti-Money Laundering Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu *(Anti-Money Laundering Act, 2006)* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama wengine walikuwa na wasiwasi, lakini wote wameafiki. Kwa hiyo, Muswada wetu utasubiri hatua nyingine kupelekwa kwa Mheshimiwa Rais aweke saini yake na hapo ndipo kazi itaanza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema Muswada umejadiliwa, umepitishwa na umeungwa mkono na wote. Mezani kwangu sina matangazo yoyote yale. Isipokuwa asubuhi nilieleza kwamba tulikuwa na shughuli ya kumpongeza Mheshimiwa Dr. William Shija, kwa uteuzi wake kuwa Katibu Mtendaji Mkuu katika Taasisi ya *Commonwealth Parliamentary Association (CPA). (Makofi)*

Kwa hiyo, Dr. William Shija, amepata dharura kwa hiyo hataweza kuwepo, kwa hiyo, shughuli ile haitakuwa kesho kama ilivyopangwa mpaka wakati mwingine. Kwa hiyo, ukiondoa hiyo sina tangazo lingine. Naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.32 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne,
Tarehe 14 Novemba, 2006 saa tatu asubuhi)*